MADA

# UHAKIKI WA FANI KATIKA *UTENZI WA SWIFA YA NGUVUMALI*

TOLA KOFA C50/P/8024/2006

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

**KITIVO CHA SANAA, IDARA YA ISIMU NA LUGHA**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

University of NAIROBI Library

0370407 9

**JULY 2009**

# UNGAMO

TASNIFU HII NI KAZI YANGU BINAFSI NA HAIJATOLEWA KWENGINE KWA MAHITAJI YA SHAHADA KATIKA CHUO KIKUU CHOCHOTE

**TOLA KOFA** **C50/P/8024/2006**

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi tulioteuliwa na Chuo Kikuu.

**DKT. KINEENE WA MUTISO**

**DKT. RAYYA TIMAMMY**

## TABARUKU

Naanza tasnifu hii kwa kuwatabarukia mke wangu Terezia Hamaro, wanangu Mugava Kofa na Maro Kofa. Mmefanya kazi yangu ngumu kuwa rahisi.

# MUHTASARI

Fani ni jumla ya vipengele vya kimtindo au kisanaa vinavyotumiwa kuwasilisha ujumbe. Katika tenzi vipengele vinavyojitokeza ni mtindo, muundo, toni, msuko, mandhari, wahusika, wakati, matumizi ya lugha na vipengele vingine vya kisanaa.

Tumeigawanya tasnifu hii katika sura nne. Sura ya kwanza inaeleza dhamira yetu kwa kufafanua dhana za somo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu ya kuchagua somo, yaliyoandikwa kuhusu somo, upeo na mipaka, msingi wa nadharia, nadharia tete na njia za utafiti. Sura ya pili inachanganua dhana ya fasihi simulizi, maana ya ushairi, chimbuko la ushairi, maendeleo ya ushairi, athari za wageni, mashairi huru na lugha ya ushairi.Sura ya tatu inafafanua vipengele vya kimtindo, matumizi ya lugha na vipengele vya kisanaa. Sura ya nne inafananua nadharia tete tano.

Kwa ufupi, nadharia tete ya kwanza inasema kuwa mtunzi ametumia msamiati akilenga hadhira ya kisasa. Maneno kama *keshi* (20), *saini* (204), *baiskeli* na *motukari* (277) n.k ni maneno yanayotuonyesha taathira za msamiati wa Kiingereza. Hawa ndio wageni waliofika mwisho baada ya Wareno na Waarabu ambao athari zao pia zinapatikana kwenye msamiati wa watu wa Kilwa. Neno *malaya* la Kiswahili lina asili ya neno *malay* la Kireno, yaani mtumishi wa kike anayetoka nchini Malay. Neno *mvinyo* la Kiswahili limetoholewa kutokana na neno *vinho* la Kireno. Pia neno *msabiki* (24), *akaqimu* (42) n.k ni maneno yaliyotoholewa kutokana na msamiati wa Kiarabu, Kwa hivyo, mvurugo huo ulioikumba lugha ya ushairi wa Kiswahili unadhihirisha kuwa hadhira hii imeingiliana na wageni kabla ya, wakati wa na hata baada ya uhuru. Hali hii ya maingiliano inadhihirishwa kutokana na utohozi wa msamiati wa wageni; hii ina maana kuwa hadhira hii ni ya kisasa.

Ya pili inasema kwamba baadhi ya wahusika hubadilisha toni kulingana na hadhira. Anapoongea na wachawi wenzake, Shambi hutusi, hukaripia na huamrisha. Mtunzi anasema:

124.Bwana Shambi kabaini

*Wewe Binti Ramadhani*

*Ama kweli majununi*

*Tuwane radhi jamia*

Anamtukana Binti Ramadhani. Anamwita majununi; mtu asiye na akili timamu; punguani; mtu mwenye maneno ya kipumbavu. Lakini akiongea na wazee na vijana hubadilisha toni. Anasema:

199. *Sasa utenge uzuri*

*Kwa haki na dasturi*

*Tupate vijana wawili*

*Wa kuchukua barua*

Hapa anajinyenyekeza kwa hadhira. Hii ndiyo maana tukasema kwamba baadhi ya wahusika hubadilisha toni kulingana na hadhira.

Nadharia tete ya tatu inasema kwamba matumizi ya lugha ya mtunzi yanabeba dhamira anayokusudia. Anasema:

11. Wa kwanza nitasema

Bwana Shambi bin Dima

Ndiye makata huruma

Na kinara alipewa.

Maana ya neno *uchawi*; ni ufundi wa kutumia dawa au vitabu maalumu vya uganga ili kuleta madhara kwa viumbe kama binadamu kwa kutumia vifaa vya kurogea. Mtunzi anaposema *ndiye makata huruma*, Shambi na wachawi wenzake hutumia vifuvu kama sahani la kupakulia chakula. Anatusawiria ukatili wa wachawi hao hasa wa Shambi ambao unamtawaza na kuwa kinara wa kundi hilo la wachawi. Hii ni sitiari.

Ya nne inasema; mtunzi anatumia vipengele vya fani ambavyo hukidhi muktadha wa uchawi. Anatwambia:

14. Nne Binti Ramadhani
Asiye siri moyoni
Hata (h) umo makundini
Shakka wakimfanyia

Taswira anayotupa mtunzi ni kwamba Binti Ramadhani haweki siri moyoni. Hapa tunaangaziwa dhamira ya usaliti kwa sababu dhana hii ya siri ndiyo mhimili wa uchawi. Wachawi ni watu wenye siri lakini mmoja wao akifichua siri hiyo basi hawatatimiza lengo lao kiufanifu. Pia, mtunzi anatumia mbinu elekezi kutuhamasisha juu ya mtanzuko utakaotokea kwa sababu ya kuregea kwa msimamo wa mmoja wao. Binti Ramadhani anasema:

49. *Jana niliota njozi*
*Unanitoka mchozi*
*Nimepakata magozi*
*Na nyama asioliwa*

50. *Nami haswa njozi zangu*
*Si badiri kichwa changu*
*Lazima yawe matungu*
*Na mbere yatatokea*

Mtunzi anasema kwamba Binti Ramadhani hutiliwa shaka na wachawi wenziwe kwa kuwa hana siri. Anatumia mbinu ya njozi kutueleza msimamo wa Binti Ramadhani katika muktadha wa uchawi.

Na ya mwisho inasema kwamba mtunzi anatumia vipengele vya fani ili aisawiri jamii anamoishi. Beti za 49 na 50 tulizonukuu kwenye nadharia tete ya nne zinatuonyesha

kwamba jamii hii ya Kilwa inaamini mambo ya uchawi. Dhana hii ya uchawi inatimizwa wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani. Kwa hivyo dhana za jamii hii ni changamano. Wengine hufuata dini ya Kiislamu kikweli na wengine husaliti dini hii. Njozi ni kipengele kinachotabiri mambo yanayoweza kumsibu mhusika. Binti Ramadhani anasema (50): *Nami haswa njozi zangu, Si badiri kichwa changu, Lazima yawe matungu, Na mbere yatatokea.* Anatabiri mgogoro utakaotokea baina yao na hadhira. *Na nyama asioliwa* ni tashihisi. Anahuisha nyama hiyo, yaani maiti ya Salima; *asioliwa*. Watu wa Kilwa hawali nyama ya binadamu, na hata wachawi pia.

Kwenye utenzi huo mtunzi ametumia sitiari, tashibihi, taswira, takriri, mazida, tabdila, inkisari, tashihisi, balagha, tabaini, usambamba, litifati, taharuki, mbinu rejeshi, mbinu elekezi, chuku, njozi, kejeli, jazanda n.k. Baadhi ya mbinu hizo zinaibua athari zinazotokana na maingiliano ya karne kadha ya Waswahili wa pwani na wageni waliozuru upwa huo. Pia zinatusawiria dhana ya kuwa lugha katika ushairi ni pevu, ya mkato na hubadilika kiwakati na kimaeneo ya kijiografia.

## SHUKRANI

Kazi hii haingemalizika kama si hisani na juhudi za watu mbalimbali. Si rahisi kuwaorodhesha wote maana ni wengi. Iwapo sitawataja wote naomba msamaha. Namshukuru Mungu kwa kunipa moyo wa kurudi shuleni katika umri wangu wa miaka sitini na zaidi na kunipa uvumilivu hadi sasa. Pili nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Kineene wa Mutiso na Dkt. Rayya Timammy kwa uelekezi wao mwafaka. Ukarimu na usaidizi wao umenikuza kimawazo.

Vile vile nawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Isimu na Lugha kwa usaidizi wao tangu Shahada ya kwanza (2001) na hii ya pili (2006- 2009). Ningependa kuwashukuru mke wangu Terezia Hamaro na watoto wangu Mugava Kofa na Maro Kofa. Uvumilivu na usaidizi wao umenifaa sana katika kukamilisha kazi hii.

Pia ningependa kuwashukuru na kuwapongeza wanafunzi wenzangu kwa kunisaidia wakati ninapokwama katika harakati hizi za kusoma. Hawa ni pamoja na Bi. Noreen Mwalili, Bibi Miriam Makanga, Bibi Betty Karimi, Mabwana Reuben Kisiroche, Kenneth Nyaosi na wale wote waliokuwa katika idara ya Fasihi. Hawa walijukumika na kuhakikisha kuwa nimefuzu. Nawatakia heri na baraka maishani mwenu.

Hatimaye namshukuru Bibi Faith Miringu, Bibi Nancy Okello na Bwana Nichodemus Omedo wa Kenya Polytechnic University College kwa kuichapa kazi hii kwa ustadi. Uvumilivu wao umekuwa mhimili wa kazi hii. Kwenu nyote ambao nimewataja na wale ambao sikuweza kuwataja nawatakieni maisha mema. Asanteni nyote.

## YALIYOMO

MADA

UNGAMO ... i

TABARUKU ... ii

MUHTASARI ... iii

SHUKRANI ... vii

YALIYOMO ... viii

**SURA YA KWANZA**

1.0 UTANGULIZI ... 1

1.1 SOMO LA UTAFITI ... 2

1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI ... 3

1.3 SABABU YA KUCHAGUA SOMO ... 4

1.4 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO ... 5

1.5 UPEO NA MIPAKA ... 22

1.6 MSINGI WA NADHARIA ... 22

1.7 NADHARIA TETE ... 24

1.8 NJIA ZA UTAFITI ... 25

1.9 HITIMISHO ... 25

**SURA YA PILI**

2.0 UTANGULIZI ... 27

2.1 FASIHI SIMULIZI ... 27

2.2 MAANA YA USHAIRI ... 38

2.3 CHIMBUKO LA USHAIRI ... 40

2.4 MAENDELEO YA USHAIRI ... 43

2.5 ATHARI ZA WAGENI ... 71

2.6 MASHAIRI HURU ... 74

2.7 LUGHA YA USHAIRI ... 76

2.8 HITIMISHO ... 94

**SURA YA TATU**

3.0 UTANGULIZI ........................................ 95
3.1.0 MTINDO ........................................ 95
3.1.1 LAHAJA ........................................ 96
3.1.2 MSAMIATI WA KIARABU ........................................ 98
3.1.3 MSAMIATI WA KIINGEREZA ........................................ 98
3.2.0 IDHINI YA MSHAIRI ........................................ 99
3.2.1 MAZIDA ........................................ 101
3.2.2 INKISARI ........................................ 102
3.2.3 TABDILA ........................................ 103
3.3.0 TAMATHALI ZA USEMI ........................................ 104
3.3.1 TASHIBIHI ........................................ 105
3.3.2 TAKRIRI ........................................ 107
3.3.2.1 TAKRIRI MANENO ........................................ 107
3.3.2.2 TAKRIRI PINDU ........................................ 109
3.3.2.3 TAKRIRI WAZO ........................................ 110
3.3.3 SITIARI ........................................ 110
3.3.4 TASHIHISI ........................................ 112
3.3.5 BALAGHA ........................................ 114
3.3.6 TABAINI ........................................ 115
3.3.7 USAMBAMBA ........................................ 116
3.3.8 TAHARUKI ........................................ 118
3.3.9 MBINU REJESHI ........................................ 120
3.3.10 MBINU ELEKEZI ........................................ 122
3.3.11 CHUKU ........................................ 123
3.3.12 NJOZI ........................................ 124
3.3.13 KEJELI ........................................ 126
3.3.14 NAHAU ........................................ 127
3.3.15 LITIFATI ........................................ 128
3.3.16 TASWIRA ........................................ 129
3.4.0 MUUNDO ........................................ 130

3.4.1 BETI....131
3.4.2 MIZANI....131
3.4.3 VINA....133
3.5 TONI....134
3.6 MSUKO....136
3.7 WAHUSIKA....142
3.8 MANDHARI....147
3.9 WAKATI....151
3.10 HITIMISHO....153

**SURA YA NNE**

4.0 HITIMISHO....154
4.1 UTANGULIZI....154
4.2 MASUALA MUHIMU....156
4.3 MAPENDEKEZO....158
MAREJELEO....159

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Katika kazi hii, tumeangalia kipengele cha fani kwenye *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* uliotungwa na Hasani bin Ismail mwaka wa 1968 na kuhaririwa na Leinhardt katika mwaka huo huo. Utenzi huu unasimulia juu ya wachawi wanne ambao ni pamoja na Shambi bin Dima ambaye ndiye kiongozi wao, Binti Jizi, Binti Ramadhani na Binti Hanifu dada yake Salima ambaye anatolewa mhanga ili kijiji chao kifanyiwe zinguo. Kupotea kwa Salima kunatokea kule pwani katika kijiji kiitwacho Mteniyapa. Kisa hiki kinatokea wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani ambapo dhana ya uchawi hasa kwa wakati huu wa mwezi mtukufu inapingana na maadili ya kidini. Zinguo si baya lakini kafara hii ina gharama kwa wachawi hawa na hata kwa wanakijiji kwa jumla.

Tumesema kwamba si wahakiki wengi ambao wamechanganua lugha, tamathali za usemi na mbinu nyengine kwa undani sana. Mpaka sasa baadhi ya mbinu ambazo zinajitokeza hazijachanganuliwa. Athari za maingiliano ya wageni na wenyeji wa upwa wa Afrika Mashariki ni kubwa sana. Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali,* Abdulaziz (1968) anachunguza muundo na arudhi ya wanamapokeo; naye Mungai (2005) analinganisha fani ya *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* na *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*; kwa hivyo hawakuzamia vipengele vingi vya fani. Tunapoangalia ufafanuzi wa Mungai wa sitiari anasema tu juu juu kwamba sitiari ni mbinu inayofananisha vitu viwili lakini hakuainisha aina tofauti tofauti za sitiari na jinsi zinavyotumika kwenye utenzi huu. Katika kutumia sitiari mtunzi anatumia maneno kama *kipimo cha aibu zake, zinapata kilo mia*; na *uzito wa aibu zake, zitapata hamsumia* n.k. Mungai hakufafanua sitiari kama hizi. Pia Mungai hakuainisha mbinu zozote za takriri. Takriri hujitokeza katika viwango kadha. Kuna takriri katika kiwango cha irabu, konsonanti, silabi, neno, sentensi, ujumbe n.k. Anapolinganisha fani katika tenzi hizi mbili anakita ufafanuzi wake zaidi kwenye *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* ambao ni kama asilimia sabini ilhali ufafanuzi wa *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* ni kama asilimia thelathini. Kimsingi Mungai hakuwa na muda wa kutosha wa kufafanua fani katika utenzi huu. Nia yetu ni kuzamia utafiti kwa undani zaidi.

## 1.1 SOMO LA UTAFITI

Msomaji anaposoma shairi la kimapokeo, kinachomvutia ni ule mpangilio maalumu wa mistari inayolingana na ambayo hupangwa kwenye beti; mistari yenye kuleta wizani maalumu; miisho ya vina vipatanifu; mizani zinazolingana kiidadi na maneno yenye kuleta maana mpya. Nia yetu katika kazi hii ya kuhakiki *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* ni kufafanua viunzi vya lugha kwa kuzingatia fani kama inavyojitokeza na kuhimili maudhui.

Utafiti wetu unajikita kwenye kuchunguza fani na jinsi mtunzi anavyovitumia vipengele hivyo ambavyo ni pamoja na wahusika, mandhari, mtindo, muundo, wakati, toni, msuko na matumizi ya lugha kwa sababu tumegundua kwamba utafiti uliofanywa hapo awali na Abdulaziz (1968) na Mungai (2005) umetilia maanani vipengele vichache sana katika fani. Kuelewa shairi kunategemea sana kuelewa fani, kwa sababu fani ndiyo inayobeba maana katika shairi la kimapokeo.

Pili, tenzi nyingi za Kiswahili hutumia lugha inayoambatana na desturi na utamaduni wa Waswahili. Msomaji ambaye hana usuli wa Uswahilini hutatizika kutokana na msamiati wa kipwani. Kwa hivyo tunafafanua msamiati na mbinu za fani ambazo zimetumiwa katika utenzi huu kwa sababu fani ina jukumu la kupitisha ujumbe kwa msomaji. Hivyo, tunahakikisha kwenye utafiti wetu kuzamia na kufafanua vipengele vingi zaidi vya fani ili wasomaji wengi zaidi waweze kuathirika na kazi ya utenzi huu. Katika uchanganuzi wetu tunajadili jinsi msanii anavyofaulu kurembesha lugha kutokana na ufinyanzi wa fani. Mtunzi pia anatumia utohozi wa maneno ya Kiarabu, Kiingereza n.k ili akidhi arudhi ya vina na mizani. Je, mbinu hii inajitokeza kulingana na ufinyanzi wa lugha ya mshairi au la? Pia katika kuleta upatanifu wa vina na mizani mshairi anatumia mbinu ya mazida, inkisari na tabdila. Huu ni ukiushi ambao mtunzi huutumia kukidhi mwelekeo fulani katika lugha. Je, anafaulu kuangazia maudhui kwa kutumia mbinu hii? Haya na mengineyo kama matumizi ya tamathali za usemi ndiyo matatizo tunayokabiliana nayo ndani ya tahakiki hii.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Nia yetu ni kuchanganua fani ya *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* tukionyesha udhaifu, ufanifu na uamilifu wa kila kipengele chake kwenye muktadha wa matumizi yake. Tunajaribu kufanya utafiti wa kina ili tuweze kutoa changamoto kwa wahakiki na wasomaji wengine. Tunajaribu pia kuonyesha jinsi lahaja ya Kilwa inavyomwathiri msanii huyu na kubainisha ni kwa kiasi gani fani inafaulu kama sanaa. Utafiti wetu unanuia pia kubainisha mwelekeo wa mtunzi wetu Hasani bin Ismail.

Ushairi wa Kiswahili, kama zilivyo tanzu zote za fasihi, jinsi tunavyojibidiisha kuuelewa ndivyo tunavyovuna matunda yake. Ushairi hutueleza juu ya mambo ambayo hatujapambana nayo ana kwa ana. Hatujakutana wala kuwasiliana na mtunzi. Hatujui mikabala yake maishani. Ili tuelewe mambo anayotuzungumzia, lazima tuelewe lugha yake, matamanio yake, mtazamo wake na utamaduni wa jamii anamoishi. Tunapokutana na Hasani bin Ismail mwisho wa utenzi huu tumeshapata fununu juu ya msimamo wake maishani kutokana na beti tulizosoma. Anatupa historia ya usanii wake. Anatudhihirishia kwamba babu yake ndiye mpanzi wa utunzi wake. Mama yake anamkabidhi kazi aliyowekewa na babu yake. Kutoka hapo anaendelea na usanii huo.

Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* msanii anatupa matarajio ya kutaka kujua zaidi kuhusu mganga huyo kwa kutumia anwani hiyo. Tunachunguza mbinu za msuko, mbinu rejeshi, mandhari, toni, wakati na litifati ili tuweze kuelewa fikira na hamasa za wachawi hao.

Washairi pia hutumia wahusika wa kila aina. Tunachunguza wahusika wachungaji, katili, ombaomba, na wahubiri ambao hufanya mambo kulingana na dhamira ya msanii na kazi yake. Kwenye ushairi wa Kiswahili, wahusika huwa na hisia za chuki au kupenda, ukatili au wema, utajiri au umaskini na hali zote ambazo hupatikana maishani. Mara nyingi msanii hutumia mbinu ya mandhari na wakati kuumba wahusika wake. Wahusika wengine hujengeka kwa ajili ya mahusiano na wahusika wenzao, tajiriba zao, shughuli zao, utamaduni wao na makaazi yao. Kwa hivyo, ushairi hutueleza juu ya watu, vitu, na mandhari. Mandhari haya huwa ya kimaumbile au ya kubuni. Msanii humweka mhusika kwenye mandhari fulani ili tuone jinsi anavyoathirika. Kwa hivyo, nia yetu ni

kuchunguza mtindo wa mtunzi huyu na jinsi anavyotumia lugha ili atusawirie wahusika wanaowakilisha desturi, maadili na utamaduni wa watu wa Kilwa.

Dhana nyengine ambayo tunachunguza ni toni ya shairi. Lugha ya msimulizi huzua hisia za masikitiko, huzuni, furaha, tisho au ukatili kulingana na maneno yake. Mbinu kama kejeli, chuku, maswali ya balagha, kinaya n.k hujenga unasaba baina ya msimulizi na msikilizaji au hubomoa ukuta huo kwa sababu ya toni ya msimulizi au shairi.

Kwenye utenzi huu msanii anatumia mbinu zote hizi kwa madhumuni fulani. Lengo letu ni kubainisha na kudhihirisha kama Hasani bin Ismail amefaulu kunawirisha maudhui katika utenzi huu kwa kutumia mbinu hizi za fani kisanaa. Anatumia mbinu kama inkisari, mazida na tabdila kwa lengo maalumu. Je, amefaulu kuwasilisha ujumbe wake kwa kutumia mbinu hizo? Ametunga utenzi huu muda mfupi tu baada ya uhuru wa Tanzania. Je, maingiliano ya watu wa Kilwa na wageni hawa yanaathiri utamaduni, dini na lugha yao? Je, anaonyesha katika fani lahaja zilizopenyeza kwenye ushairi wake?

Mbinu nyengine ambazo tunazichanganua ni *tamathali za usemi*. Mbinu hizi ni sitiari tashbihi, tashihisi, maswali ya balagha, tabaini, usambamba, taharuki, mbinu rejeshi, mbinu elekezi, chuku, njozi, kejeli, litifati, taswira, tasfida n.k.

## 1.3 SABABU YA KUCHAGUA SOMO

Kama katika kazi zozote za kisanaa utenzi huu una sifa mahsusi ambazo hazina budi kuchunguzwa kama zinavyochunguzwa kwenye tenzi nyengine. Pia tunaamini kuwa kuna mengi kuhusu fani ambayo hayajafanyiwa utafiti wa kutosha kwa sababu hakuna uhakiki unaoweza kudaiwa kwamba umekamilika. Wahusika wachawi hufanya mambo yao kando ya hadhira wakati wa usiku. Je, mtunzi huyo amefanikisha matukio kwa kutumia mbinu hizi zinazotuhamasisha tuchunguze fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*? Huu ni utenzi wenye vipengele vingi vya kifani vya hali ya juu na hivyo vinatufanya tuvutike tutake kuvichambua. Dhana tunazochunguza ni mtindo, muundo, wahusika, toni, mandhari, wakati, msuko na matumizi ya lugha. Tunachunguza mbinu zote hizo za fani kama zinavyojitokeza na kutathmini matumizi yake, na kama mtunzi huyu amefaulu au la.

## 1.4 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO

Katika uchunguzi wetu, tumegundua kuwa hakuna utafiti wa ndani uliofanyiwa utenzi huu. Wataalamu wengi wa fasihi na isimu hawakutalii kwenye fani ya utenzi husika. Hata hivyo, mhakiki Abdulaziz (1968) anashughulikia maumbo kama vina, mizani, mishororo, beti na lahaja ya Kilwa. Anasema kuwa beti za utenzi huu zina mishororo minne minne yenye vina vya aaax, bbbx, cccx n.k. Anaongeza kusema kwamba a,b na c hubadilikabadilika lakini x haibadiliki maana ndicho kina cha kibwagizo. Kuhusu mizani anasema, hutofautiana kutoka shairi hadi jengine lakini kwenye shairi lolote lile mizani haibadiliki. Kwa kawaida kila ubeti huwa na mizani nane katika kila mshororo kama inavyojitokeza kwenye utenzi huu, lakini mtunzi huyu anakiuka kaida ya vina hapa na pale. Anafanya hivi makusudi ili apate wizani shairi linapoghaniwa. Inawezekana kwamba hataki kupotosha maana kwa kujikita kwenye vina na mizani. Anatupa mifano ifuatayo:

201. Wa pili Hamadi Ramadhani
Kijana mwenye imani
Ngawa aswi chuoni
Lakini kaelekea

263. Wala hapatoki mtu
Mkubwa au mtoto
Yaliyo hapa mazito
Polisi upesi kimbia

Ubeti unaotangulia, mshororo wa kwanza una mizani kumi, wa pili nane ,wa tatu saba na kibwagizo nane. Ubeti unaofuatia mshororo wa kwanza una mizani nane, wa pili nane, wa tatu nane na kibwagizo tisa. Kwa hivyo, ubeti unaotangulia mizani zinatofautiana kiidadi badala ya nane za kawaida. Pia mshororo wa tatu wa ubeti wa kwanza una mizani saba badala ya nane. Katika ubeti wa pili kina cha mshororo wa kwanza ni *-tu* badala ya *–to*. Abdulaziz anasema kwamba mtunzi huyu ameambaa zile kanuni ambazo haziupi ushairi wa Kiswahili nafasi ya kulegeza sheria hizo kwa sababu humlazimisha mtunzi kuteua maneno ambayo hayaingiliani na wizani; ilimradi mizani zitii sheria za

utenzi na kuwa nane katika kila mshororo. Anasema kuwa mtunzi huyu anatumia simo zinazochukuana na hadhira yake. Anatumia neno *zagao* ili atusawirie shamrashamra zinazotingisha kijiji hicho. Pia anatumia neno *zigozigo* kutudhihirishia athari kali iliyokuweko. Anatumia uradidi wa neno *zigo.* Huu ni mzigo mkubwa wenye kumkalifisha mbebaji wake. Neno *chokochoko* ni kashifa. *Pesepese,* iliyotapakaa. *Fufufu*, tele tele.

Anaendelea kusema:

> Mtunzi huyu ametumia sana lahaja ya Kilwa; lahaja ya Kiamu haikujitokeza sana kama desturi ya ushairi wa wanamapokeo. Ni sehemu ndogo sana tunapokutana na lahaja hiyo kama *pamoya* na *wanayua* badala ya pamoja na wanajua ya Kiswahili sanifu.

Akituangazia dhana ya litifati, Abdulaziz anamnukuu msanii akisema:

237. Walipofika wakasema:
*Yuko wapi Salima?*
Dadaye kasimama:
*Huyu hapa kajifia.*

Anasema kwamba, kwa ustadi wake wa kuwadukiza wahusika kwenye mazungumzo yao moja kwa moja na hadhira, mtunzi amefaulu kubainisha mwelekeo wao, na kutudhihirishia uwajibikaji wao kikamilifu. Hapa Abdulaziz anamsifu mtunzi huyu kwa kutumia mbinu hiyo ya litifati. Hata hivyo hakuzamia kwa mapana mbinu nyengine za tamathali za usemi, msuko, mandhari, wakati, wahusika, toni na matumizi ya lugha kama yanavyojitokeza.

Mungai (2005) naye analinganisha fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* na *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Mbinu kama tamathali za usemi hakuzichanganua kwa wingi ilhali zinajitokeza sana. Anatueleza juu juu mbinu kama msuko, wahusika na uhusika wao, mandhari, wakati na toni. Kuhusu toni anasema (38).

Toni hujitokeza katika shairi lolote. Aina nyingi za toni hujitokeza ama za huzuni, huruma, masikitiko, kuamrisha, furaha, kuchanganyikiwa, ukatili, kilio au hali zingine nyingi.

Anasifu aina nyingi za toni bila ya kutoa mifano mingi. Anatufichulia aina moja tu ya toni: *Tisho*. Anasema (104):

> Masharti haya ya kujitoa mwenyewe kama atamkosa mmoja wa aila zake yanatisha mhusika huyu na hata hadhira.

Si mhusika mmoja anayetishwa katika utenzi huu. Hapa anatuonyesha tisho la Binti Jizi anapomwambia Binti Hanifu kwamba:

23. *Awe mtoto wako*
*Ao ni ndugu yako*
*Isiwe jilani yako*
*Siye anayetakiwa.*

40. Binti Hanifu mwambie
*(H)apo atoe nduguye*
*Ao yeye afidie*
*Sisi tutampokea.*

Mungai anatutolea mfano mmoja wa toni, na ni mhusika mmoja tu anayetishwa. Binti Ramadhani anatishika na pia anahuzunika (116 – 123). Shambi mwenyewe pia anatishika (219 - 224). Bwana Mwenye (142) anamtisha Binti Ramadhani. Vile vile mwathiriwa Salima pia anatishika (82). Mungai hatuelezi jinsi hadhira inavyotishika katika beti hizo. Liwali pia anatishika (251 – 254). Hadhira pia inatishika (280 – 285). Hiyo ni aina moja ya toni lakini mifano anayotoa haijazi chungu. Vile vile anasema (104):

> Kiongozi wa wachawi, Bwana Shambi ana toni ya kuamrisha, kutishia, na yenye matusi.

Hapa hatuonyeshi toni hizo zote zinakojitokeza. Pia hatufichulii uthabiti wa Shambi na ukatili wake. Hatuonyeshi kejeli ya Binti Ramadhani ambaye ingawa anajua

yanayomkumba Salima anajitia kimbelembele (168) cha kuanza kutia ubani kwanza ndipo shughuli za kumtafuta Salima zianze. Pia, baada ya kumtafuta Salima na kumkosa tunapata toni ya kukiri kwa Binti Ramadhani anaposema (181): *Waume wamenizunguka. Akili imepotea.* Wachawi wenzake walimhamisha mwathiriwa bila yeye kujua.

Kuhusu wahusika Mungai anasema (38):

> Kila mhusika huwa na umuhimu mkubwa sana katika kazi ya sanaa. Huingizwa katika kazi ili kutimiza malengo maalum ya msanii, kwani bila hivyo, huenda baadhi yao wakaonekana kama waliozuka kiajali tu.

Mtunzi amechukua muda kwenye utangulizi (10- 14) kutujulisha wachawi hawa. Kwa hivyo swala la kuzuka kiajali halijitokezi. Binti Ramadhani pia anawakanya wenzake (52, 53) wasimvunje Shambi kauli. Kisha anawaambia: *Wala yasiwe kivumo.* Hapa mtunzi anatudhihirishia kuwa Binti Ramadhani hana msimamo, na ni yeye anayewasaliti wenzake.

Kutokana na nukuu hizi tunapata dhana za usambamba, ukinzani na kutojukumika. Binti Ramadhani hataki kumwudhi Shambi ingawa tena hataki kushirikiana na wachawi hawa kumtoa Salima mhanga. Tunapata ukinzani wa kimaana.

Mungai ni mtafiti mahiri katika kazi ya sanaa hasa fani, lakini inaonekana hakuwa na muda wa kutosha wa kufafanua baadhi ya vipengele hivyo vya fani. Hakuvitolea maelezo mengi. Upungufu kama huo ndio unaotutia mshawasha wa kutaka kubainisha *yaliyoandikwa kuhusu somo* na kuchangia zaidi mada hii. Tungependa kujaribu kuziba baadhi ya mapengo waliyoacha wataalamu hawa kwa kuhakiki vipengele vya fani vinavyojitokeza kwa upana zaidi. Kwa mujibu wa dhamira hii tunaangazia zaidi fani na vipengele vyake na namna matumizi yao yanavyosukuma mbele maudhui.

Hakuna mhakiki ambaye amezamia kuhakiki utenzi huu kwa mapana. Aidha katika mapana yake pia, utenzi ni utanzu ambao haujashughulikiwa sana kitahakiki. Wataalamu wengi wa fasihi na isimu wanaliambaa jukumu hili, lakini Kineene wa Mutiso amezamia sana maudhui na fani katika tenzi za *Mwana Fatuma*, *Siri li-Asirali*, *Hamziyyah* na *Fumo*

*Liyongo*. Kwa mfano, tukichukua *Hamziyyah,* mhakiki huyu anatupa historia ya utenzi huu. Anasema (2005) :

> Hamziyyah ndiyo tafsiri ya zamani zaidi katika lugha ya Kiswahili. Ni kazi za mwanzomwanzo kutungwa kwa Kiswahili.

Anatuarifu kwamba ni utungo wa ukawafi ambao Waislamu huikariri wakati wa Maulidi ya Nabii Muhammadi. Anatueleza asili ya neno *Hamziyyah* kuwa kila ubeti wake kwa Kiarabu unaishia na herufi *Hamza.* Anatujuza juu ya umaarufu wake na msamiati wake kuwa ni Kingozi na haupatikani kwenye kamusi ya kisasa.

Katika maelezo yake kuhusu fani mhakiki huyu anatupa maelezo haya:

> Fani ni jumla ya mbinu za kisanaa ambazo hutumiwa katika kuwasilisha ujumbe au maudhui katika fasihi. Mtindo hujumlisha vipengele vyote vya lugha. Vipengele hivi vya mtindo ni kama vile msamiati, tamathali za semi, miundo ya sentensi, aya, beti n.k. Viungo vyengine vya fani ni lugha, umbo, muundo, wahusika, mandhari, ploti, mtindo, wakati na toni. Shairi na hususa utenzi, huwa na mgawanyiko wa beti, vipande, mishororo au mistari, lugha ya kitamathali, wahusika, mizani au silabi na idadi yake, urari wa vina, kujitosheleza, urefu, bahari, kibwagizo n.k.

Kuhusu matumizi ya lugha, anasema kuwa lugha iliyotumika zaidi ni Kingozi na lahaja za kaskazini. Baadhi ya maneno ya Kiswahili cha zamani ni kama vile: *Alambile;* alisema, *amsilepo;* alipomaliza, *aduwimbi;* adui mbaya n.k. Kuhusu lahaja ya kaskazini hasa Chimwiini maneno kama kwetu huandikwa *kwechu;* badala ya /t/: *mtaanga* badala ya mchanga, *mtuuzi* badala ya mchuzi. Msamiati huu hutumika katika Kimvita, Kitukuu na Kisiu. Yako matumizi ya aina kadha; *kurima;* kulima, *zeema;* wema, *chileemba*; kilemba n.k. Pia anatupa lahaja za Kipate na Kiamu. Nchi; *nti,* mchanga; *ntanga,* maji; *mai,* vijiwe; *zijiwe,* vikosi; *zikosi*, kujuta; *kuyuta,* viumbe vyake; *ziumbeze,* vitani; *zitani,* kwisha kwake; *kwisakwe* n.k. Maneno mengi ya Kiarabu yametumiwa. Mengine

yametoholewa na kutafsiriwa kwa Kiswahili. Maneno hayo ni kama *biri;* kisima, *dhatul;* nafsi, *hal;* vipi? *Khawufu;* hofu, *sama;* mbingu, *ulumu;* elimu, *yaumu;* siku n.k.

Akigusia tamathali za usemi, anasema (53):

> ...ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika kiwango hasa cha maana na hata mpangilio wa maneno, ili kuleta msisitizo au maana mpya. Mbinu hii huleta maana mpya au msisitizo na humwezesha mwandishi kusema asemayo kwa njia inayoacha athari kwenye sikio la wasomaji au hadhira yake. Tamathali za usemi ni kama takriri, ritifaa, tashibihi, chuku, tashihisi, jazanda, taashira, semi, balagha, kejeli, tabaini, usambamba n.k.

Anasema kuwa wakati mwingine palipo na sitiari huenda pakawa na taashira, jazanda na hata istiari. Balagha pia hufuatana na chuku au kejeli. Vile vile kuna ukiushi ambapo mtunzi hakuyaendeleza maneno ipasavyo. Mbinu nyengine ni mazida, inkisari na tabdila.

Katika mbinu ya mazida mtunzi hurefusha maneno ili atosheleze idadi ya mizani. Kwa mfano: *Ikafuatatana;* ikafuatana, *maishara;* ishara, *sabatini;* sababu, *ulisitirile;* ulisitiri, *wamtolezele;* walimtoa n.k.

Nayo mbinu ya inkisari huwa katika viwango vya kimofolojia na kifonolojia. Maneno hufupishwa ili mizani zipungue katika neno. Kwa mfano; *akusenyeyo;* aliyokusanya, *alize;* aali zake, *alo;* aliye, *amzazile;* alipomzaa, *apeteo;* alipopata, *atukule;* alichukua, *dhambize;* dhambi zake n.k.

Kuhusu mbinu ya tabdila mtunzi hubadilisha sauti fulani ili kupatikane wizani hasa mwishoni mwa kipande cha mshororo. Hali hii hujitokeza msanii anapotaka kuwe na uwiano au tofauti fulani wa kina. Kwa mfano:

5. Dhatil ulami zaliwazo kwa alalimu
   Al-ghaibu ndako na masimu ya Adama

Badala ya neno Adamu analibadilisha kuwa *Adama*. Maneno mengine ni *dhulama;* dhalimu, *Isilama;* Waisilamu, *Jahanama;* Jehanamu, *Kauma;* Kaumu, *mangi;* mengi, *Tabasuma;* tabasamu, *Nuri;* Nuru, *waajama;* wanafahamu, *nasabu;* nasaba n.k.

Nayo mbinu ya takriri hujitokeza pale ambapo mshairi ana nia ya kusisitiza wazo ili msomaji apate athari katika ujumbe unaosawiriwa. Mshairi hurudia konsonanti, irabu, silabu, neno au hata sentensi nzima. Kwa mfano:

154. Mwelupe kulama na jaishi *kutekateka*
Pindi ghairipo ukutano maso kinama.

Hii ni takriri ya neno *teka.* Analirudia na kuwa *kutekateka* ili msomaji aone athari ya hali ya Mtume. Uradidi mwingine ni takriri za konsonanti na Irabu:

12. Napendezwa tena uso wako *u*ngawa Jua
*U*funikwao ni *u*siku *m*welupe *m*wema

88. *W*onte *w*o *w*atano *w*asibiwa kwa *ndw*ele kuu
Na kuhilikika auniye ni *ndw*ele jama

419. Tende uwezao ya amali za zema hwenda
*Mi*chende *mi*checho ikaangusha *ma*chunda *me*ma

Hapa tunapata takriri ya silabi, konsonanti na irabu kama zilizoandikwa kwa italiki.

Nayo mbinu ya ritifaa, msimulizi huhutubia hadhira ambayo haiko. Mbinu hii hujitokeza sana wakati wa maombolezo. Vitu ambavyo havipo husimuliwa na kusifiwa kana kwamba vipo. Kwa mfano:

437. Kubali faswiha ya aliyotamka *dhwadi*
Ikima kayenda wivu kwayo dhwau ikima

Mtarjumi Aidarusi anaongea na Mtume Muhammadi ambaye haonekani; pia:

444. Haki miyongoni mwa ayazo na kulemewa
Kuliko swifazo hakuhusu kulanga mema.

Hapa pia mtunzi anaongea na Mtume Muhammadi ambaye haonekani.

Katika mbinu ya tashibihi msanii hulinganisha vitu au hali mbili kwa kutumia maneno; *kama, mithili, mfano wa, fanana na, sawasawa na, kulingana na* n.k. Kwa mfano:

3. *Walimathilila* sifa zako kuliko watu
*Ja* maa yaliyo *kumathili* ndani nujuma.

Hapa msanii anamlinganisha Mtume Muhammadi na mambo ya ajabu ajabu.

Mbinu ya sitiari nayo hulinganisha vitu viwili kwa njia ya moja kwa moja bila ya kutumia vilinganisho. Kitu kimoja huambiwa ni kitu kingine. Kwa mfano:

4. *Uwe ndiwe Tala* ya fahila na mayonjia
Nuru khazilawi ila mwako Nuru si njema.

Mtunzi anamlinganisha Mtume na nuru. Maumbile ya Mtume, na yale ya nuru ni tofauti. Msanii hulinganisha vitu viwili ambavyo havina ushabihiano kimaumbile na wala kitabia. Hapa tunapata taswira ya utukufu wa Mtume ambao hung'ara kama nuru. Taa ni kifaa ambacho humtoa mtumiaji wake gizani. Waislamu hutoka gizani wakifuata njia ongofu za Mtume Muhammadi. Yeye ni nuru. Yeye ni taa ambayo humlikia watu wakiwa gizani.

Chuku nayo ni sifa ambayo jambo hukuzwa kupita kiasi. Hutiwa chumvi. Kwa kawaida mbinu hii haitumiwi kwa nia mbaya. Kwa mfano:

24. Alimzalile atukule kitwakye juu
Nakutukuwa ni muishara ya kula mema.

Alipozaliwa kichwa cha Mtume Muhammadi kilielekea mbinguni. Hii ni ishara ya ufalme wa Mungu. Hii ni chuku.

Pia tunaambiwa:

25. Matoye kuyenga uwinguni na maloleo
    Ya ambao lake tukufu na ya adhima.

Alipozaliwa nyota zenye mianga zilimkaribia na kuangazia pale alipo na pande zote za dunia. Hii ni chuku.

Mbinu nyengine ni tashihisi. Kitu hunafsishwa na kuwa na umbo, tabia au hisia za binadamu. Kwa mfano:

46. Mola tumiliza zamanize ya kuletwakwe
    Zimondo kulinda na kudule pakakadama

47. Kitokoza jini makoloni ya kusikiza
    Kama tokozwao mbwa mwitu watunda nyama.

Mungu alimtumia vimwondo waliolinda njia ambayo majini hupitia. Baadhi ya vitu hivi ni kama vile miti, wadudu, ndege na wanyama. Vitu hivi huongea na kutenda mambo kama binadamu. Humsujudia Mtume Muhammadi. Vina akili hata zaidi ya wanadamu. Kwa mfano ndovu anakataa kuiharibu *al-ka'bah;* hivyo amevunja amri ya bwana wake ambaye hana hekima kama yeye.

Taswira nayo ni picha ambayo humtokea msomaji akilini mwake. Picha hii hujitokeza kutokana na maelezo anayoyapata katika kazi ya fasihi. Msomaji hupatwa na mguso kupitia kwa picha hiyo. Humwezesha kuhisi, kugusa, kunusa, kusikia na kuona yanayoelezwa. Msanii hutumia lugha kutuchorea picha wazi tukaweza kuviona vitendo vyenyewe mpaka tukasahau kuwa hiyo ni kazi ya kubuni. Taswira pia hutokana na mbinu nyengine kama vile semi, maelezo, ishara, tashibihi, balagha, takriri, sitiari n.k. Kwa mfano:

27. Zilungu za yumbe zikawona zilizo Rumi

Kawaona alo nyumbaniwe Maka Mukima.

28. Palidhihirile miujiza kwa muswaniwe

Isositamana kulikoye mato mazima

Mwangaza huo uliwawezesha watu wa Makka kuona jumba la Mfalme Kisra. Mabonde yote ya Makka yakang'ara. Watu waliweza kuona vilima vilivyokuwa mbali sana. Tena majumba makubwa ya Shamu yalionekana kwa sababu ya nuru ya Mtume Muhammadi.

Makka na Roma ni mbali sana, lakini watu wa Makka waliweza kuyaona makasri ya Kaisari. Warumi hali kadhalika waliweza kuona Makka vizuri. Taswira hizi zinatuibulia nguvu za Mwenyezi Mungu. Taswira zinaweza kuwa za kimaelezo au za kiishara. Kwenye utenzi huu taswira nyingi ni zile za miujiza iliyotokea tangu mimba, utotoni na maishani mwa Mtume Muhammadi. Msanii anatuchorea picha hizi juu ya yale yaliyotokea kabla ya kuzaliwa kwake, wakati alipozaliwa na baada ya kuzaliwa kwake. Hata wakati wa kunyonyeshwa miujiza mingi ilitokea.

Nayo taashira ni mbinu ambayo neno, kitu au tukio huficha maana au hisia mahsusi. Hujitokeza kama ishara, kidokezo, dalili na neno ambalo huwakilisha kitu ambacho hakitajwi moja kwa mjoa. Wakati wa kuzaliwa kwake tunaona ishara nyingi. Kwa mfano:

12. Napendewa tena uso wako ungawa Jua

Ufunikiwao ni usiku mwelupe mwema.

13. Usiku wa kuzaliwa na sikuye ambayo

Kwamba pawele sururi na fahari ya dini thama.

14. Pakafuatana na biashara za mbilingano

Kwamba lizaliwa Mustwafa pamele zema.

15. Ukalewalewa ukumbingwa wake Kisra

Ni miujizao kwamba kali wako kunama.

16. Pakuswiri sapo kule nyuma moja moto
Zijalile ghamu kwa kuzima na baa zima.

Uso wako ni kama jua lijitokezalo baada ya giza kali, ni wenye kupendeza. Uso wako una Nuru ifukuzayo giza totoro. Uso wako wa ajabu ulifukuza giza zito la usiku.

Ndani ya nyumba za Mafursi mioto ilizimika na kukawa huzuni tupu. Mafursi hawa walikuwa wakiabudu mioto hiyo kwa muda wa miaka elfu moja. Mito na chemchemi za Mafursi hao zilikauka. Falme nyengine duniani ziliporomoka. Hizi ni ishara za ushindi wa Uislamu dhidi ya dini nyengine duniani.

Maswali ya balagha pia yanajitokeza. Mbinu hii humtanabahisha msomaji lakini hayahitaji majibu kwa sababu yanafahamika. Msanii anatumia mbinu hii ili kusisitiza ujumbe anaotaka kuupitisha. Maswali ya balagha hufafanua zaidi wazo alilonalo msanii na kutuonyesha msimamo wake. Vile vile humshawishi msomaji. Huamsha nadhari yake na kumtia mshawasha juu ya kile kinacholengwa na maswali hayo. Mtunzi huuliza maswali hayo ili awachochee wasomaji wake waweze kufikiria zaidi juu ya jambo analolielezea. Kwa mfano:

1. Hali wakwelaye kukwelako mitume yonte
Uwingu usiwo kulotewa ni moya sama?

Mtunzi anauliza ni kwa namna gani mitume wengine wa Mwenyezi Mungu wangeweza kupaa hadi mahali alikofika Mtume Muhammadi? Pia anasema:

20. Nyani furahia mwana Hawa kwamba tukule
Mimba yake Tumwa au yake fadhili njema?

Nani aliyemweleza mama Hawa ambaye ni mama wa kwanza wa Mtume Muhammadi afurahie mimba hiyo? Na halafu mama Amina ambaye ndiye aliyemzaa? Haya ni maswali ya balagha.

Mbinu nyengine inayojitokeza ni kejeli. Mtunzi humtweza mtu au hali fulani kwa kutumia msamiati unaotia mtu uchungu. Kwa mfano:

218. Enyi wenye zuo tuyuzeni kula zilipo
Kuthalithi au kudhihiri walo wa nyuma?

Enyi wasomi wa Taurati na Injili ni vipi kuwa na miungu watatu katika Mungu mmoja? Hii ni kejeli.

Pia mbinu hii hujitokeza msanii anaposema:

219. Hapakuwa chuo na akida mbili zambazo
Nakushika yambo liso naswi viwe si vema.

Mtunzi anasema kuwa kulingana na Wayahudi, Mtume Muhammadi hakuleta kitabu kitakatifu. Katika beti hizo mbili msanii anawapiga vijembe wafuasi wa Agano la Kale na Agano Jipya kwamba dhana zao hazimo kwenye vitabu hivyo. Mbinu hii ya kejeli imetumika sana hasa pale anapolinganisha dini ya Kiislamu na dini nyengine za Ukristo na Uyahudi. Anawakejeli au kuwabeza wafuasi wa dini hizo mbili. Kulingana na mtunzi huyo, dini iliyoasisiwa na Mtume Muhammadi ndiyo inayofaa kufuatwa na watu wote duniani. Anasema:

267. Kajiwa na kheli yongoyawo kwendeya vita
Wana kuyongoya utamboni farasi njema

Anasema wakati Mtume Muhammadi alipokwenda vitani kupigana, Mayahudi walikuwa wakiendesha farasi wao kwa mikogo na kujishaua. Walikuwa na hakika kuwa wangeshinda, lakini kwa sababu ya unafiki wao, walishindwa vitani na wanaume wenye nguvu zaidi.

Mbinu ya mwisho ambayo tungependa kuiangazia ni usambamba. Mhakiki anasema kuwa, huu ni urudiaji wa muundo wa kisintaksia kwenye virai, vishazi au sentensi. Anamnukuu mtunzi akisema:

12. Napendezwa tena uso wako ungawa Jua
Ufunikiwao ni usiku mwelupe mwema.

Mshairi anapendezwa na uso wa Mtume Muhammadi ambao ni kama jua linalofukuza giza la usiku. Hapa tunapata dhana ya *giza* na *nuru.* Huu ni usambamba.

Kuhusu muundo mhakiki huyu anasema:

> Muundo ni umbo la jinsi kitu kinavyoundwa na kuleta uhusiano baina ya vijisehemu mbalimbali vya kazi ya kifasihi ili kuunda kazi nzima.

*Hamziyyah* imeundwa kwa beti nyingi na kila ubeti una mishororo miwili. Imegawanywa kwenye sehemu tatu yaani utangulizi wa mtarjumi, kazi asilia iliyotungwa kwa Kiarabu, na kimalizio chake.

Msuko nao ni mbinu ambayo mtunzi hutupa mpangilio wa matukio, mgogoro, matarajio, visababishi na matokeo. Kipengele hiki cha msuko ni cha vitushi ambavyo si vya moja kwa moja. Mpangilio wa matukio hauna mfuatano maalumu. Ingawa msuko wenyewe ni changamano, unaeleweka kwa urahisi. Visa vingi vinarudiwarudiwa. Msomaji anaweza kuanza na sehemu yoyote na kuelewa yaliyomo.

Mandhari ya utenzi huu ni ya mazingira ya utendaji au ya usimulizi. Yanatusawiria sehemu ya Makka alikozaliwa Mtume Muhammadi; mito na chemchemi, vituo vya kupumzikia vya Mahujaji, Madinah alikohamia, Misri na mandhari ya mbinguni ambako alipaa na kukutana na Mwenyezi Mungu uso kwa uso. Pia anatupa mandhari ya sehemu mbalimbali ya kivita ambako kulikuwa na mapambano kati ya Waislamu na Makafiri.

Wahusika wanasawiriwa kimatapo. Kuna wahusika binadamu kama Mtume Muhammadi mwenyewe, Khadija, Halima, Amina, wazazi wa kwanza Adamu na Hawa, Abu, Jahali, Suraka, Yahudi, Ali, al–Hasan, al–Husain, Makalifa na Masahaba wa Mtume

Muhammadi. Kundi la pili ni la wahusika ambao si wa kawaida kama vile Mwenyezi Mungu, Malaika, Majini na Mashetani. Kundi lingine ni la wahusika wanyama kama ngamia, farasi, kondoo, punda, mbuzi na ndege kama njiwa; wadudu kama vile mchwa, buibui; miti, mito, bahari, jangwa na chemchemi. Wahusika wote hao wanatenda matendo ya kibinadamu. Kundi la wahusika binadamu linakinzana kwa sababu ya dini. Kundi jema linaongozwa na Mtume Muhammadi, na lile la waovu linaongozwa na Shetani. Mtunzi anatupa sifa za Mwenyezi Mungu, Mtume Muhammadi, Malaika, wanawake wote kwa jumla, Masahaba wanne ambao ni Abu Bakr, Uthman, Umar na Ali. Hawa walishika hatamu za uongozi baada ya Mtume Muhammadi. Pia akatupa sifa za vitu ambavyo havina roho kama vile miti na mawe vilivyoweza kumtolea ushuhuda na kumwunga mkono. Kwa hivyo, ingawa yeye ameshughulikia fani katika *Hamziyyah*, ufafanuzi wake wa msamiati wa Kiarabu umetusaidia kuchunguza fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*.

Mulokozi (1999) ambaye naye ameshughulikia tenzi za *Inkishafi*, *Fumo Liyongo* na *Mwana Kupona* kimaudhui na kifani anaingia kwa undani sana na kuzua msisimko mpya katika tenzi. Tukiangazia juhudi zake za kuhariri *Mwana Kupona,* Mulokozi (vi) anatupa maelezo na historia ya Waswahili. Anasema:

> Kipindi cha kwanza ni kile cha ustawi wa miji, utamaduni na tawala za Waswahili. Kipindi cha pili ni kile cha utawala wa Wareno na upinzani wa wananchi dhidi yao. Kipindi hiki kilimalizwa na maingilio ya Dola ya Oman. Kipindi cha tatu kilianza wakati wa kuasisiwa na utawala wa Waarabu wa Oman na kumalizwa wakati wa maingilio ya ukoloni wa Kiingereza na Wadachi. Utungo huu wa *Mwana Kupona* ulitungwa baada ya utawala wa Oman uliojaa migogoro ya kisiasa. Unawakilisha utamaduni na mawaidha ya kipindi hicho.

Mhariri huyo anatueleza maisha ya mtunzi, miswada ya utenzi huo, muhtasari wa utenzi na mjadala uliozushwa na utenzi wenyewe.

Kuhusu maudhui, anasema kuwa yanasisitiza haja ya kuzingatia mafunzo ya dini ya Kislamu, kumtii Mungu na Mtume wake, kutenda na kupenda kama inavyotafsirika kidini, kumtii muwewe na kuishi naye kama dini inavyoagiza. Anatupa maelezo kuhusu mila, desturi na jadi ya Waswahili. Anasema:

> Kwa kuwa mtunzi anatokana na tabaka tawala
> hakuwa Mswahili wa kawaida. Yeye anatokana
> na tabaka lilokuwa na watumwa.

Kuhusu fani anasema (115):

> *Mwana Kupona* si utenzi unaojipambanua sana kisanaa. Mpangilio wa mawazo yake unalegalega; kuna kujirudiarudia kwingi; baadhi ya beti zinazopaswa kuwa mwanzoni ziko mwishoni.

Anatueleza kuwa lugha ya mtunzi ni lahaja ya Kiamu. Vile vile hakutumia sana lugha ya picha kama tashibihi, sitiari na taswira. Tunapata kwa uchache lugha ya picha kama *hirizi, koja* na *kidani* au *kifungo*. Hirizi ni kinga ya binti yake ambayo ingemlinda dhidi ya matatizo wakati atakapoolewa. Kidani cha lulu ni picha ya mtungo mrefu wenye thamani. Matumizi ya lugha hiyo ya picha inasawiri hali iliyokusudiwa kwa ustadi sana. Kwa mfano mtunzi huyu anasema:

> Semani mite ya nganu
> Mutii waume zenu…

Analinganisha uchanga wa kimawazo na umri wa wale wanaousiwa na miche ya ngano ambayo bila matunzo mazuri inaweza kuangamia. Akimalizia mhariri huyu anasema:

> Mtunzi huyu hutumia lugha ya kawaida.
> Hatumii msamiati wa kutatanisha.
> Sitiari na taswira hazimshangazi msomaji.

Vile vile mhariri huyu ametoa maelezo ya kila ubeti kwa kufafanua matumizi ya lahaja ya Kiamu. Ufafanuzi wake wa msamiati wa Kiamu katika *Mwana Kupona* na athari zinazoikumba lugha na utamaduni wa Waswahili kwa sababu ya maingiliano ya wageni hawa na wenyeji umetusaidia sana. Tunakubaliana naye kuwa Mwana Kupona hakuwa "Mswahili halisi" maana anaongea juu ya maswala ya utabaka: 20. Sitangamane na watumwa illa mwida wa khuduma.... Dhana hii ya utabaka inajitokeza pia kwenye *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* (154). Athari za lahaja ya Kiamu pia zinajitokeza.

Ingawa tenzi zinahusishwa na ukale wa lugha na ugumu wa msamiati, maudhui yake yanasisimua. Ugumu huu unatokana na kufumbata lugha ya Kiarabu, jambo ambalo huleta utata kwa msomaji ambaye haelewi lugha hiyo. Katika kupunguza utata huu, wahakiki wengi wanafaa kuzifanyia uchunguzi na uhakiki katika mapana yake. Kazi nyingi za Kiswahili na Kiingereza zinashughulikia fani siyo tu katika ushairi bali kwenye fasihi kwa jumla. Kazi hizo ni pamoja na mwongozo wa Vuzo (1986) wa riwaya ya *Nyota ya Rehema* ya Mohammed, mwongozo wa King'ei (1987) wa tamthilia ya *Mashetani* ya Hussein, mwongozo wa Mohammed (2001) wa tamthilia ya *Kilio cha Haki* ya Mazrui na mwongozo wa Mwita (2003) wa riwaya ya *Walenisi* ya Mkangi. Kabla ya kuanza kazi hii tumesoma kazi nyingi ili tupate maarifa kutoka kwa tahakiki nyengine ambazo zinaweza kutusukuma mbele. Tunaposoma kazi za watalaamu wengine kama Abdulaziz (1979) na Mungai (2005), hatuoni kuwa wamefanyia tenzi uchunguzi wa kutosha. Uhakiki wao hautoshi kwa sababu wameacha viungo vingi katika fani. Kwa hivyo nia yetu ni kujaribu kuziba mwanya ambao umeachwa kwa kuhakiki fani na vipengele vyake kama vinavyojitokeza katika kazi hii.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA

Tunajaribu kuchunguza vipengele vya fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Vipengele hivi ni pamoja na lugha, muundo, mtindo, wahusika, mandhari na wakati, na jinsi vipengele hivi vinavyojitokeza katika utenzi huu. Hatutachunguza maudhui ila tu pale ambapo tuna haja ya kufafanua fani.

## 1.6 MSINGI WA NADHARIA

Nadharia tunayotumia ni ile ya umuundo, ambayo inahusishwa na mwanaisimu Mswisi ambaye amehusisha ukuaji wa nadharia na isimu kwa kiasi kikubwa. Wahakiki wengi wameathiriwa na mtazamo huu wa kinadharia kama chombo muhimu kwa vile hutoa mwongozo bora wa utafiti. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) na Mbatiah (2001) wamesema kuwa kazi ya kifasihi haina urejelezi wa nje. Kimuundo kazi ya kifasihi inaangaliwa kama mfumo wa ngazi ya pili unaotegemea mfumo wa ngazi ya kwanza ambao ni lugha. Baadhi ya Wanaumuundo hawatilii maanani muundo wa nje wa kazi. Mmoja wa hawa ni Ferdinard de Saussure ambaye anaamini kuwa fasihi, hasa ushairi una viwango mbalimbali kama sauti, wizani na sarufi. Kila kiwango kinaweza kuchunguzwa peke yake au kwa ujumla wao. Jukumu hilo linahitaji mhakiki ajifunge kwenye kazi hiyo bila utafiti wa nje. Kwenye kazi hiyo mfasiri au mwandishi hana hisa. Anapochunguza matini kwa kuangalia sehemu mbalimbali za viwango hivyo vya kazi na jinsi vinavyounda muundo mzima, huwa anatekeleza jukumu lake kama mhakiki. Anastahili kuchunguza vipengele vinavyojitokeza kimuundo na wala si kutoa fasiri ya kazi hiyo. Viwango hivyo vya lugha huzaa mfumo wa lugha hiyo. Kwa kuwa hairejelei kazi za nje inatufanya tuwazie hali yake ya lugha.

Mfumo huo hautilii maanani dhamira ya msimulizi au mtunzi. Mtazamo huo huficha mfumo wa uashiriaji. Viashirii vina maana zaidi kuliko viashiriwa. Kwa mfano, mtu akisema: *Fulani ni mbwa.* Mhakiki anafaa atuangazie sitiari hiyo kwa kuchunguza tabia ya mbwa. Tabia ya mtu huyo hufichika nyuma ya tabia ya mbwa. Inatuhitaji tuchunguze tabia ya mbwa kwanza ndipo tujue tabia ya mtu huyo. Muundo huo wa lugha unapuuza tabia ya kiashiriwa; *mbwa.* Hapa maana inayozushwa na muundo huo unamvutia msomaji zaidi kuliko kiashiriwa. Wanaumuundo wanatilia shime kiashirii kuliko kiashiriwa. Kwao, maudhui katika kazi ya fasihi si muhimu. Wanaamini kwamba kazi hiyo hasa ushairi hutokana na kanuni maalumu ambazo ni lazima zifuatwe. Maana haitokani na msimulizi, mtunzi au msomaji. Unasibishi wa maana huhusishwa kwenye muundo kuliko kile kinachorejelewa. Yule mtu anayefananishwa na mbwa ni muhimu zaidi kimaana kuliko mbwa mwenyewe.

Kwa upande mwingine Wanaumuundoleo wanapinga mtazamo wa Wanaumuundo. Vinara wa upingaji huu ni pamoja na Jacques Derrida, Julia Kristeva, Micheal Foucault, Jacques Lacan, Louis Althusser na wengineo. Kitovu cha mawazo ya umuundoleo ni kizalia cha mtazamo wa Ferdinard de Saussure. Kulingana na wahakiki hao, lugha inabeba nafasi kubwa katika jamii sababu ufasiri wa kibinafsi ndio nguzo ya uhakiki. Lugha ndicho kiungo cha jamii ambacho hubainisha matatizo, harakati zao na kujieleza kwao. Kwa hivyo, nadharia hii inaona kuwa lugha na matumizi yake ndicho kilele cha muundo. Ufasiri huu wa kibinafsi unatuelekeza kuamini kuwa ni wa kijamii. Dhana hii hukuzwa wakati wa harakati za jamii kama vile siasa, uchumi na mawasiliano na inashikilia kusema kwamba maana huelezwa na msimulizi. Wanaumuundoleo hawa wanapinga wazo la Fedinard de Saussure kwa kujikita kwenye ishara za kimaandishi au kiuzungumzi. Wanaamini kuwa maana hutokana na msimulizi binafsi. Hawa wanadai kuwa maingiliano na mazungumzo katika jamii huzua maana kutokana na muktadha wa jamii hiyo kwa sababu huwahusisha wazungumzaji binafsi. Wanasema kuwa ishara moja huwa na fasiri nyingi katika jamii. Wanapinga kuwa ishara moja haiwezi kuwa na fasiri nyingi. Kwa hivyo, kiashiriwa *mbwa* kinaweza kuwa na maana mbalimbali kulingana na ung'amuzi wa jamii hiyo. Wanaeleza kuwa maana ya kiashiriwa hupuuzwa na kutengwa wakati wa mazungumzo hayo. Wazo hilo linatiliwa nguvu na Jacques Derrida ambaye anasema kuwa maana ya kiashiriwa hubadilika kulingana na muktadha katika mazungumzo ya jamii. Anapinga mtazamo wa Saussure unaopendekeza kuwako kwa mhimili katika kazi yoyote. Wazungumzaji huongea mambo yanayopatikana au kutopatikana, wayajuayo na wasiyoyajua, maalumu na ambayo si maalumu. Kwa hivyo, mhimili wa kazi ya kifasihi hubadilika au hutengwa wakati wa mazungumzo.

Kimsingi wanamuundo hawatilii maanani msanii wa kazi ya kifasihi wala dhamira yake. Athari za nje ya makala hazina mchango mkubwa katika kazi ya kifasihi. Umuundo unaangaliwa na wahakiki wengi kama nadharia inayotokana na fani. Katika nadharia ya kimuundo, vina na mizani hutumika sana kwa sababu huonyesha uhusiano wa sauti na maana katika shairi. Maneno ya kawaida huundwa upya kutokana na sauti hizi na kuibua maana mpya ambayo humwathiri msomaji. Mbinu ya usimulizi pia inatiliwa maanani, maana visa vidogovidogo huoanishwa na kuibua kisa kikubwa. Katika *Utenzi wa Swifa*

*ya Nguvumali* tunapata uhusiano wa wahusika kifamilia ukivurugwa na dhamira ya zinguo. Kwa hivyo tunajaribu kubainisha zaidi mbinu mbalimbali zinazotumiwa katika kubuni hadithi na matukio kwa kuchunguza fani.

Wanaisimu wengi wanaitazama fani kama sanaa ya sauti na maneno kuliko kifaa kinachoakisi jamii. Ilhamu yao hujitokeza kwenye ushairi wenyewe na wala sio mshairi husika. Wanajikita kwenye maana ya kazi maalumu wala si chanzo au athari zake kwa msomaji. Fani ina sifa maalumu ambazo huipa kazi ya kifasihi upekee wa kutambulikana kama kazi ya kifasihi. Nia yao ni kuchunguza sifa za fasihi ambazo huzitofautisha na taaluma nyinginezo kama historia, sosholojia n.k. Fani hufanya vitu vya kawaida katika maisha vionekane vipya. Pia hufafanua mambo au maneno na kuyakuza ili yawe wazi zaidi. Tunachokisema ni kwamba lugha ya kishairi hutofautiana na lugha ya kawaida kutokana na matumizi ya mbinu zake mbalimbali kama vina, mizani na wizani. Mbinu hizo huzua maana mpya katika maneno.

Isimu inatuelekeza kuwa lugha ina vipengele tofauti tofauti ambavyo hatimaye huunda mfumo wa lugha husika. Kwa hivyo wazo la kutafuta maana nje ya kazi hiyo halipo. Lugha yenyewe hujitosheleza kupitia kwa fani. Utoshelevu huo hujitokeza kwa uwazi wakati fani ikitumika vilivyo. Katika fani, wakati mwingi mtunzi hukiuka kaida za kueleza maana katika maneno, vifungu vya sentensi na sentensi zenyewe. Ukiushi huo hutokana na matumizi ya jazanda, chuku, urudiaji, ulinganishaji n.k. Mbinu hizo ndizo tunazochunguza kwa sababu huweka mkazo kwenye unasibishi wa maana ambao hueleza maana inayohusishwa na neno hilo, na wala si kile kinachoashiriwa. Nadharia hii inatathmini fasihi kwa kuchunguza fani kiisimu na jinsi fani inavyotekeleza jukumu lake ili ilete maana. Nadharia ya umuundo inajitokeza sana kwenye utanzu wa ushairi na hiyo ndiyo maana tumeichagua.

## 1.7 NADHARIA TETE

Nadharia tete huhusishwa kwa kuelezea mawazo aliyonayo mhakiki kabla ya kufanya utafiti.Hujitokeza pale ambapo mhakiki huwa na ujuzi wa mambo fulani akilini kutokana

na mikabala ya jamii ya kila siku. Mikabala hii humfanya apekue, achunguze na kupata fununu za aina aina kutokana na mazingira yanayomkabili. Kwenye utenzi huu mtunzi anatueleza juu ya dhana ya uchawi wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani. Dhana hii ya uchawi inapingana na ile ya dini ya Kiislamu hasa wakati huu wa mwezi wa Ramadhani. Swala la *zinguo* ambalo linachochea ukatili wa wachawi hawa kwa kumtoa Salima mhanga linatuangazia utamaduni wa watu wa Kilwa kwamba, wakati wa kilimo hufanya zinguo. Nadharia tete hazina mhimili kwa sababu mhakiki hutoa kanuni za kijumla ambazo si yakinifu. Zinahitaji kuthibitishwa. Anatusawiria jamii hiyo kwa kutuonyesha wahusika wema dhidi ya waovu kwenye mazingira ya utamaduni wa Kiislamu. Hii ina maana ya kwamba nadharia tete hazizuki kwenye ombwe tupu. Hushikamanishwa na hali mahsusi inayojitokeza kwenye mazingira fulani ya jamii. Nadharia tete hizo ni kama zifuatazo:

1. Mtunzi ametumia msamiati akilenga hadhira ya kisasa.
2. Baadhi ya wahusika hugeuza toni kulingana na hadhira kwa sababu ya malengo maalumu.
3. Matumizi ya lugha ya mtunzi yanabeba dhamira anayokusudia.
4. Mtunzi ameteua vipengele vya fani ambavyo vinakidhi muktadha.
5. Kwa kutumia fani mtunzi amefaulu kuisawiri jamii anamoishi ya wahusika wema na waovu katika mazingira ya kidini dhidi ya mazingira ya kijumla.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu umetegemea sana maktaba. Tumeusoma *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* kwa undani ili tuuelewe zaidi. Tumejaribu kusoma kazi za watunzi wengine na waatalamu mbalimbali wa ushairi hasa wa tenzi. Tumesoma kazi ambazo zinafanana na kufaa kututolea mwongozo bora wa kushambulia na kuhakikia fani. Njia ya pili tunayotumia katika utafiti wetu ni mahojiano. Tumewahoji baadhi ya waatalamu wengine wa fasihi; hasa wa mashairi na tenzi uso kwa uso kwa ajili ya kupata mwongozo zaidi.

## 1.9 HITIMISHO

Katika makala ya Geoffrey N.Leech (1969): *A Linguistic Guide to English Poetry;* tunaambiwa; *...hakuna tamathali za usemi zinazovutia zaidi kuliko sitiari...* Hayo ni maneno ya James Harris akinukuliwa na Ralph Quirk. Lakini kwenye utangulizi, mnukuzi huyo naye anasema: *Kuna mbinu zaidi ya sitiari zinazoshughulikiwa katika lugha ya ushairi...* Hata hivyo tunajaribu kutumia vipengele vya misingi ya uhakiki wa fasihi, hasa vya fani katika ushairi wa Kiswahili.

Lugha ya ushairi huvunja kimakusudi kanuni za lugha kwa njia nyingi; nyengine huwa wazi na nyengine huwa fiche. Njia zote mbili huhusisha ukiushi kwa lengo maalumu. Tunazichunguza zote hizo kwa makini na jinsi zinavyojitokeza. Mjumi, hasa msanii wa mashairi, hufurahia mbinu ya *idhini ya mshairi* bila kujali historia ya jamii. Hii ina maana kwamba anaweza kutumia lugha ya kale au lugha inayotawala jamii katika kipindi hicho anachoandikia. Yote hayo yanachukuliwa kama sifa za usanii. Kwa mfano, kejeli, maswali ya balagha, sitiari na mbinu nyenginezo zina mizizi yake katika lugha ya kila siku ya jamii. Mbinu hizo zinaweza kuchunguzwa kwenye matumizi ya muktadha zinakojitokeza kila siku.

Mpaka baina ya lugha ya ushairi na lugha ya mazungumzo ni finyu. Kwa hivyo, haihalisi kuweka mpaka baina ya dhana hizi mbili. Jambo linalojitokeza kinaganaga ni muundo wa beti, mishororo, mizani na vina.

Katika kudondoa mbinu za fani kwenye utenzi huu, labda hatutazimaliza zote, lakini zile tunazopambana nazo tunajaribu kuzichambua. Sifa tunazopambana nazo kwenye tahakiki za wale waliotutangulia pia tunazidi kuzichunguza. Sifa hizo ni matumizi ya lugha ambayo yanajumuisha tamathali za usemi, lahaja mbalimbali, idhini ya mshairi anapozidisha, kupunguza na kupangua tahajia, silabi na kugeuza muundo wa neno, kirai, kishazi au sentensi. Pia tunachunguza mtindo na vipengele vyake ambavyo ni pamoja na muundo, toni, msuko wahusika, mandhari na wakati.

Katika tasnifu hii tunachukua jukumu la kukubaliana au kuhitilifiana na wahakiki hao waliotutangulia. Iwapo hukumu yetu ina kichapo cha ziada tunawaomba msamaha kwa sababu msamiati na lugha ya Kiswahili kwa jumla ni nyumbufu. Watumiaji wa lugha huchubua lugha kwa sababu ya athari za kimaeneo, umri, jinsia na mandhari yanayowakabili. Mitazamo ya watumiaji hao wa lugha huathiriwa na mikumbo ya mikabala ambayo Achebe (1973) anaiita *mapambano ya kila uchao.* Sisi pia tumo ndani ya mapambano hayo. Tofauti na lugha ya nathari ambayo hutumika kwa mjazo na mapana kwenye insha, hadithi na tamthilia, mashairi mengi hutumia lugha ya mkato lakini tambuzi. Hutekenya fikira na hisia zetu na kuakisi matarajio na mapendekezo yetu. Msanii hutumia neno moja au zaidi yanayojirudia au yasiyojirudia kiruwaza. Baada ya kuyasoma na kuyafahamu mashairi hayo, hutufanya tujichunguze na kutupa msukumo fulani. Hapo hutufanya tuzingatie upya dhana, mtazamo, msimamo, mwelekeo na fikira zetu maishani. Kwa mujibu wa maelezo hayo, pengine hukumu yetu dhidi ya mawazo ya wahakiki hao haitakubaliana hapa na pale. Tunachowaomba ni kwamba *pasiwe na kivumo wala malumbano* ikiwa hayo yatatokea. Tuwasiliane ili turekebishe masiala yoyote yatakayoibuka kwa sababu, hakuna tahakiki au mhakiki anayekamilika.

# SURA YA PILI

## 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tunashughulikia dhana ya fasihi simulizi kwa kijumla kwa vile ushairi kwanza ulianza kama ushairi wa kimapokeo kabla ya kuandikwa, swala la maana, chimbuko la ushairi wa Kiswahili, maendeleo yake katika vipindi mbalimbali ambavyo ni majilio ya Waarabu, Wazungu, Waarabu tena na sasa, athari za wageni, mashairi huru na lugha ya ushairi. Ushairi ulibadilika kulingana na maingiliano ya wenyeji na wageni hawa.

## 2.1 FASIHI SIMULIZI

Hii ni aina ya fasihi ambayo msimulizi hupitisha ujumbe kwa msikilizaji kwa njia ya mdomo. Binadamu hutumia maneno kuangazia tajiriba zao za kila siku. Hutumia maneno kuelezea asili yao, imani zao, desturi na tamaduni zao. Anaweza kuelezea mambo haya kwa kutoa hadithi, methali, nyimbo au vitendawili. Simulizi hizi huwa na maadili. Katika hadithi ya kumwonyesha mtu mwingine kuwa ulafi si mzuri mtu anaweza kumwambia mwengine kwa njia isiyo wazi. Anaweza kumtambia hadithi ya yule fisi ambaye anaalikwa kwenye hafla mbili tofauti wakati mmoja. Kwa kuwa hataki kukosa vinono vya pande zote mbili, fisi huyo anapasuka msamba na kufa. Hadithi kama hii inatufafanulia athari za ulafi, na vile vile inatusisimua na kutuburudisha mbali na kutupa mawaidha. Mawaidha kama hayo pia hujitokeza kwenye kipengele cha fani cha methali kama: *Mtaka yote hukosa yote;Njia mbili zilimshinda fisi; Ukitaka kuruka agana na nyonga* n.k. Jamii hupitishiana yale wanayoyaona, wanayoyafikiria na kuyasikia kupitia kwa fasihi sumulizi. Kwa ufupi binadamu hupitishiana au hubadilishana mawaidha, uchunguzi, hisia na masiala fulani katika jamii. Wanapowasiliana hutumia fani ambayo huzua hisia za kumbukumbu fulani. Tunapomwona fisi kwenye bustani ya wanyama tunamchunguza ili tuthibitishe ukweli wa hadithi hiyo ili hata sisi tujihadhari tusipasuke msamba.

Kwa hivyo, fasihi simulizi hukanya, hutupa wasia na hutupa kumbukumbu ya mambo tunayoona, kufikiria na kuyasikia. Kupitia kwa fasihi simulizi binadamu hujua desturi zao, imani zao, asili yao na tamaduni zao kwa jumla. Huelewa hisia zao, mienendo yao na falsafa ya maisha yao kutokana na tamaduni zao. Tamaduni hizi hujengeka kutokana na maisha ya kila siku ya jamii maana tamaduni hizo hubadilika kwa sababu ya majilio ya mambo mapya.

Nyimbo ambazo ni kipengele kimojawapo cha fasihi simulizi huwa na majukumu kadha wa kadha. Hutungwa na msanii kwa kuteua maneno kulingana na hali iliyopo. Katika matanga, mtunzi huteua maneno yanayofariji wafiwa kwa kumsifu marehemu. Wakati wa arusi, nyimbo za pongezi na mawaidha hutungwa ili kuwaonyesha maharusi hao kuwa asasi hiyo wanayosherehekea huweza ikaporomoka iwapo mmoja wao hatamthamini mwenziwe. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Kitumbua kimeingia Mchanga* ya Mohammed (2000), wanawake wanataka thibitisho kama Hidaya bado ni bikira au la. Kwa niaba ya wanawake wote mmoja anauliza (60): *Shahada mara tatu… Kitumbua kimeingia mchanga au hakikuingia?* Wale wengine wanajibu: *Hakikuingia, kinangojea kuliwa tu*! Hili ni thibitisho kuwa Hidaya alijitahidi. Hakuharibiwa usichana wake. Ni bikira. Hapo wimbo sasa unasikika:

*Bwana anakula sororo*
*Sororo kwa manyamanyama*
*Bwana anakula soro…*
(Vigelegele)

Waimbaji hawa wanatumia fani. Wanatumia jazanda katika wimbo huu ili kutuhakikishia kwamba Fikirini anamwoa Hidaya akiwa bado bikira. Kutokana na wimbo huo maisha yao ya ndoa yanaanza vizuri.

Nyimbo pia hutumika katika kumbembeleza mtoto mchanga. Mtoto huyo huweza akapata kumbukumbu kuwa anapoimbiwa wimbo fulani basi chakula hakiko mbali au anatarajiwa alale. Hutuathiri kwa maudhui yao. Hutumia sitiari nyingi. Kwa mfano, mtu

akielezwa juu ya athari za *machozi ya simba* yaani *chang'aa*, kwanza anapata picha ya simba akilia na machozi yake kutiwa kwenye chupa, kisha akafikiria kuwa simba ni mnyama mkali, basi hapo kumbukumbu za ukali na ubaya wa chang'aa humwangazia. Kwa hivyo, fasihi simulizi hutoa mafunzo pia. Dhana hii ya kutumia mdomo katika fasihi simulizi ni muhimu sana kwa sababu maneno hutamkwa na hutenda kwa kutumia lugha. Katika sanaa kama uchoraji kipengele muhimu ni kalamu zenye rangi tofautitofauti; uchongaji wa vinyago hutumia gongo la mti; ufinyanzi wa vyungu hutumia udongo. Lakini katika fasihi simulizi fanani hutumia lugha kuumba hadithi, vitendawili, methali, nyimbo, misemo na kuigiza matukio fulani. Ni kipengele hiki cha usimulizi kinachohifadhi sanaa hii; ingawaje teknolojia inaihifadhi kwenye vitabu, kanda za video na redio na santuri.

Fasihi simulizi ni kazi za sanaa za binadamu zinazowasilishwa kwa mdomo na kiutendaji. Zinatuimarisha na kutuangazia historia ya jamii, hueneza elimu, siasa, uchumi n.k. Hufuata mpangilio maalumu. Katika ngano, fanani huanza na neno maalumu; *paukwa*. Kisha sehemu ya pili ambayo ni hadithi yenyewe hufuata. Sehemu ya tatu ambayo hufuatwa na maneno maalumu kama; *waliishi kwa amani milele* n.k humalizia hadithi hiyo; kwa hivyo, mtunzi hutumia lugha kisanaa. Hueleza mambo mbalimbali katika jamii na huzua hisia za chuki, vitisho, udhaifu, furaha, hofu na huzuni za binadamu. Kazi hizi hutuangazia shughuli za kila siku, kazi zao na familia zao. Hutuelezea mahusiano ya binadamu na binadamu wenziwe. Kutokana na kazi hizi binadamu hufunzwa, huonywa, huburudishwa, hufurahishwa na hupata maadili. Humpa nafasi ya kujirekebisha ili awe mwanajamii bora, pia humpa ilhamu ya kuboresha mazingira yake kwa ajili ya vizazi vijavyo. Ingawa kazi hizi huburudisha na kustarehesha, huwa na uzito zaidi katika jamii. Husherehekea maajabu kama maua na mimea, milima na mabonde, mito na majangwa, lugha na ufasaha wake n.k. Humtanabahisha achunguze jazanda za maisha yake na uwezo wake wa kufurahia au kupuuza mazingira hayo. Mada anazozizungumzia msanii hutuangazia yale yanayombana rohoni mwake. Maana ya maisha yanayowasilishwa na mwanafasihi huambatana na fikira, ujumbe, falsafa na dhamira ya kazi hiyo. Umaanisho huo pia hutupigia tochi itikadi na ukweli wa maisha. Fasihi simulizi inafanana na maisha halisi

kwa sababu msanii hutoa mwelekeo unaoweza kufananishwa na maisha yanayoshabihiana na ya jamii. Kazi hii huwa kioo cha yale mambo yaliyoko na yanayowezekana ili maisha yawe bora zaidi. Msanii hueleza mambo kama yanavyomfunulikia. Hutumia sanaa amsadikishe msomaji ayakubali na kufumwa rohoni na yale anayoyaona kwenye kazi hiyo.

Lengo letu katika tasnifu hii ni kuangazia jinsi vipengele vya fasihi vinavyojitokeza kwenye utenzi huu. Mtunzi huyu anatumia fani kuwasilisha ujumbe. Uteuzi wa msamiati wake unasukuma ujumbe huo mbele. Lugha imepangwa ili itoe umbo na muundo tofautitofauti, na fani zinatumiwa ili zituangazie taswira na kuibua hisia za aina kadha. Sajili hutumiwa kwa makusudio yake. Lugha, sauti, methali, vitendawili, nyimbo na visa ndani ya visa hutusawiria sifa na tabia za wahusika ambao hutuangazia hisia zao ili tuhuzunike, tufurahike, tushangae au tuburudike. Huingiliana kwa mpangilio fulani ili walete taathira kwenye hisia za hadhira. Hadithi huwa na mshikamano mwafaka. Matumizi ya lugha huibua hisia za kukosa matumaini na kukata tamaa. Mtunzi katika fasihi simulizi huwa na lengo la kunawirisha mapenzi, chuki, uhasama, uovu, huzuni, usalata na uzandiki katika maisha. Uhusika wa wahusika hao humfanya mhakiki atoe makisio ya tabia zao kwa sababu maisha halisi ya jamii yamejaa makisio.

Kwenye utenzi huu tunahakiki mbinu za lugha zinazojitokeza. Baadhi ya mbinu hizo ni takriri katika viwango vya irabu, konsonanti na silabi, hasa vina. Pia tunachunguza toni ambayo huzua huzuni, furaha, sikitiko n.k. Tunachunguza usambamba unaojitokeza kwenye takriri ya virai, vishazi na sentensi ili tuweze kuona ufanifu wa msisitizo anaokusudia kwa uyakinifu au ukanusho wake. Pia tunachunguza sitiari ambazo huleta ulinganisho wa moja kwa moja na kutupa taswira fulani. Je, msanii ametumia tasifida kwa nia ya kupunguza makali ya matamshi ya msamiati unaoelezea miko katika jamii? Je, ametumia tashihisi ambazo zina uwezo wa kuhuisha vitu visivyokuwa na uhai na kuvipa sifa za vitu vyenye uhai? Baadhi ya wahusika kwenye utenzi huu hutumia kinaya, yaani huongea mambo kinyume cha makusudio yao. Vilevile, kejeli imetumika kwa wingi. Wahusika wengine huwapiga wenzao vijembe. Kisha maswali ya balagha yanajitokeza kwa wingi ili msomaji ahamasike na kutafakari ukweli ulipo.

Baadhi ya wahakiki huhulutisha dhana kama maumbile na kuyanasibisha na mazingira na utamaduni wa jamii. Ubinadamu hujumuishwa na muktadha wa mazingira na utamaduni. Hapa tunachunguza sifa za binadamu kwenye mazingira na utamaduni maalumu. Dhana zote hizo huunganishwa na fasihi simulizi. Methali huunga visa; ngoma huchezwa zikifuatana na nyimbo zenye mafundisho; mteguaji na mtegaji wa vitendawili hukamilishana. Fasihi simulizi ni kitovu kinachoeleza harakati za jamii. Katika utenzi huu kitovu hiki kinasawiriwa na msanii kwa lugha na matumizi ya tamathali za usemi.

Dhana ambayo tunaifafanua zaidi ni nyimbo ambazo ndizo mwanzo wa ushairi simulizi. Nyimbo hizi hujitokeza kwenye miktadha tofautitofauti. Kuna nyimbo za kubembeleza watoto, mapenzi, matanga, siasa, harusi, vita, kafara n.k. Jamii nyingi za Kiafrika huimba nyimbo katika shughuli zote hizo. Hata wakati wa uzalishaji mali pia nyimbo huimbwa ili zisahilishe dharubu ya kazi. Kutokana na nyimbo hizo jamii huomboleza, huburudika, hupana moyo, na kupitishiana taarifa za siri. Wakati wa ngoma watu hucheza kwa dhati wakifurahia mahadhi na mdundo wa ngoma. Tunachothibitisha ni kwamba utendaji wa lugha hujitokeza kwenye fasihi simulizi. Utendaji huo unahusisha msanii na hadhira yake. Hapa inabidi tuchunguze utunzi wa msanii na msisimko unaojitokeza kwenye hisia za hadhira, na jinsi uwasilishaji huo unavyoleta maana. Fasihi simulizi ina nafasi pevu katika kutimiza shughuli za jamii, mahusiano yao, na uzushi wa kitabaka katika jamii hiyo. Dhana hii haijitokezi kimapokeo pekee bali huzingatia matumizi ya lugha kisanaa katika jamii na maisha yao ya kila siku kwenye nyanja za siasa, uchumi, dini na itikadi zao. Utendaji huu huleta taathira katika jamii. Lugha kama kitovu cha utendaji hujitokeza kwenye uchanganuzi wa mahusiano baina ya muundo, amali na maana ya miktadha ya lugha tendaji. Dhana hii inaibuka katika ngoma, nyimbo, hotuba na miigo mingineyo. Kwa hivyo, swala la umapokeo linachukuana na usasa kwa sababu zote zinanawirishwa na fasihi simulizi. Hivi ni kusema usanii wa mtunzi huzua utendaji wa jamii kutokana na matumizi ya lugha. Tamko lolote la msanii huleta utendaji. Swala la utendaji hujikita katika falsafa ya lugha. Fasihi ya jamii hutuangazia utamaduni wa jamii hiyo. Hutuangazia historia ya jamii kama chanzo chake. Tunachokisema ni kwamba fasihi simulizi huelimisha na kuburudisha kupitia lugha na msuko wa vitushi ambavyo hutuangazia migogoro baina ya wahusika katika kazi ya fasihi. Wakati mwingine,

migogoro hiyo hujikita kwenye akili ya mhusika mmoja. Katika usimulizi, mgogoro huwa na nafasi kubwa kabisa. Wahakiki wengi hutambua umuhimu wa migogoro hii ambayo hujitokeza kwa njia mbalimbali. Mivutano hii ni mhimili ya kuifanya hadithi kuwa na taharuki. Kazi nyingi za fasihi hukuzwa na wasanii kwa kuleta migogoro.

Tukizingatia fasihi simulizi kama utamaduni wa jamii, tunaona dhahiri jinsi utandawazi unavyoathiri hali ya uchumi na biashara, teknolojia inayoleta vyombo vingi vya mawasiliano na uhamiaji wa watu kwenye maeneo ya nchi za Afrika. Harakati zote hizo zinapiku nguvu za utamaduni wa Mwafrika. Kwa ajili hiyo mwelekeo wa fasihi simulizi ya Kiswahili unavurugwa; utamaduni unaathirika pakubwa. Ni muhimu kuzingatia athari hizi kwa mapana. Lugha ikiwa mhimili wa utamaduni wa jamii, inafaa ichunguzwe zaidi. Pili fasihi simulizi hutumia lugha kufafanua vizingiti katika maisha ya jamii. Kazi zinazotokana na fasihi andishi ndizo zinazokalifisha mwelekeo wa fasihi simulizi ambayo ndiyo mbabe wa fasihi andishi. Dhana hii haijapewa kipaumbele kama inavyohitajika. Hakuna mikakati inayoshugulikia utambulikanaji wa utanzu huu. Utamaduni wa jamii unaengaenga kwa sababu ya kudhoofika kwa nguzo hii ya fasihi simulizi. Wakati umewadia wa kuipa dhana hii umaarufu wake unaostahili.

Tumesema hapo awali kuwa ushairi wa Kiswahili ni nyimbo ambazo hazikufuata mdundo wowote. Ushairi huu uliimbwa ili kuelezea hisia alizonazo msanii. Ushairi huwa na taathira za pande mbili; za msemaji na za msikilizaji au hadhira. Kazi hii hutoa msisimko, huzindua na kumwathiri mlengwa. Kule Uswahilini ushairi simulizi ni wa zamani sana na hauna tarehe. Haukuandikwa kwa sababu jamii hiyo haikujua kusoma wala kuandika. Hata kama wangejua kuandika wangevuruga dhana ya ushairi huo maana dhima yake ni kuimbwa. Lugha iliyotumiwa ina ukale wenye busara; kwa hivyo, kwenye lugha hiyo tunapata lindi lililojaa hekima; ingawa lugha hiyo huburudisha, kulikuwa na mafundisho ndani yake. Nyimbo hizo huimbwa kulingana na sherehe zinazolengwa. Si sawa kuimba nyimbo za matanga kwenye harusi; na wala haiyumkiniki kuimba nyimbo za uvuvini kwenye harusi. Kila sherehe ina nyimbo zake kulingana na muktadha. Hapa tunapata vitendawili vinavyoitwa *kifunga nyama* ambavyo hufanywa kwa njia ya ushairi. Ngonjera pia hufanywa kishairi. Washairi huwa na malumbano kwa kuonyeshana

ubingwa wa kimafumbo na tambo za aina kadha. Hukumbushana juu ya maadili yanayosahaulika. Pia dhana ya majigambo hunawirishwa na ushairi huu. Tunapata mashujaa wakisifiwa kwa ushairi. Tunapata vichekesho, mawaidha, maombolezo kwa kutumia jazanda, tamathali za usemi n.k.

Wakati wote huo, ushairi wa Kiswahili haukuwa na malumbano juu ya swala la arudhi mpaka ulipoanza kuandikwa kwa hati za Kilatini katika karne ya kumi na tisa na ishirini. Uzushi baina ya wanamapokeo na wanamapinduzi unafafanuliwa na K.Amri Abedi kwenye dibaji ya *Kielezo cha Fasili* ya Shaaban Robert(1968) anaposema;

> Basi si ajabu kamwe beti hizi za Sheikh Shaaban zikawa chanzo cha kufufua utunzi uliosahauliwa wa Liongo. Na kuna kundi la tatu ambao wasingetaka aina zozote mpya za mashairi kuanzishwa ghairi ya hizi zilizokwisha kuwako, maana wanadhani ya kuwa kuzua kipya katika ushairi ni kuvuruga, ijapokuwa wanaridhika na vipya vingi ambavyo babu zao hawakupata kuvitononoka. Fasili ya 12 ya kitabu hiki ambayo ubeti wake wa kwanza unasema:
>
> *Nashikilia ukale, ambapo hapana budi*
> *Na huacha vile vile, iwapo haunifidi.*
> *Nitabadili milele, siwezi kuwa abidi*
> *Wa kutenda yale yale, kuizuia juhudi.*

Ubeti huu una mishororo minne yenye vina vya ndani ambavyo ni *–le* na vina vya nje ambavyo ni – *di.* Kila mshororo una mizani kumi na sita. Katika ubeti huo Shaaban bin Robert yuko kwenye njia panda. Anafuata arudhi ya wanamapokeo ingawa anasema: *Nitabadili milele, siwezi kuwa abidi, wa kutenda yale yale, kuizuia juhudi.* Hapa anakubaliana na wanamapinduzi.

Akiunga mkono mjadala wa Shaaban Robert wa wanamapinduzi, Mohamed (1984), ingawa anapinga ukale, anakubali kuwa uko. Kwenye dibaji yake ya diwani ya *Kina cha Maisha* anasema:

> Nimekuwa nikifuata ushairi wa Kiswahili kwa miaka mingi na kuuhisi kwamba kiwango chake cha kisanaa na kimaudhui hakikui wala hakibadiliki. Kutokua kwake kunatokana na dhana ya kuchukulia tu kuwa sifa kuu za ushairi wa Kiswahili ni vina na mizani, mwala na urari, kibwagizo na beti; na hasa zile zenye mistari minne (yaani tarbia).

Yeye ni mwanamapinduzi lakini anakiri kuwa ukale ulikuwako. Kulingana na mtunzi huyu anatubainishia kwamba kanuni hizi katika lugha ya kale zilikuwa muhimu, lakini zina ugumu fulani katika kuzieleza. Utaratibu huu hunyima nafasi mtunzi kujieleza kwa sababu ya pingu hizi za sheria za utunzi wa mashairi.

Senkoro naye anasema:

> *Tatizo* lilianza rasmi miaka ya mwisho ya sitini na mwanzoni mwa miaka ya sabini walipotokea *watundu* watatu; Ebrahim Hussein, Euphrase Kezilahabi na Jared Angira. Hawa waliandika na kusoma mashairi kwa lugha ya Kiswahili bila kujali kanuni zilizo *uti wa mgongo* wa ushairi wa Kiswahili kwa wanamapokeo. Baadaye waliungwa mkono na washairi wengine kama M.M. Mulokozi, K.K. Kahigi, na hivi karibuni Henry Muhanika na Theobold Mvungi.

Senkoro anatueleza kuwa wanamabadiliko hawa waliandika mijadala hiyo kutuonyesha kuwa si lazima shairi la Kiswahili libanwe na pingu za vina na mizani. Baadhi ya wanamapokeo hawakuingia kwenye malumbano hayo kwa sababu wanamabadiliko hao hawana vita na ushairi unaofuata sheria hizo kwa sababu nusu ya mashairi ya Mulokozi

na Kahigi (1973) kwenye diwani yao ya *Malenga wa Bara* yanafuata sheria za vina na mizani. Watundu hao walisema kuwa mienendo ya binadamu, wanyama, ndege na viumbe vyenginevyo inazidi kubadilika kwa sababu ya mazingira yanayobadilishwa na binadamu; hivyo basi si halali fani na ushairi wa Kiswahili kutounga mkono mabadiliko haya. Walisisitiza kwamba ushairi huu uyakubali mabadiliko haya na kuyashangilia. Mtazamo wa wanamapokeo wa kuutazama ushairi kama ufasaha wa lugha ...*maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata* unapingwa vikali na wanamabadiliko. Ubishi huu uko kwenye masiala ya urari wa vina na mizani kwa sababu ya *lazima* ya wanamapokeo. Kulingana na hawa, bila urari huo shairi la Kiswahili huleta maana.

Akilumbana na Mayoka, senkoro anaendelea kusema;

> Tatizo kubwa la Mayoka ni kuwa ametoa matamko ya jumla jumla mno kutokana na imani yake ya utakatifu wa ushairi. Kazi ya ushairi ya kuuzindua na kuuelimisha umma wa binadamu hutegemea maswala mbalimbali ya kijamii, hasa ya maslahi ya kitabaka. Katika mfumo wa kibepari, kazi ya ushairi mara nyingi ni ya kuwalaza na kuwapumbaza watu ili waendelee na ujinga wao kuhusu hali zao. Kazi za namna hii ni zile zinazoeleza uzuri wa maua na machweo ya jua; utamu wa nyimbo za ndege na za mawimbi ya bahari, pamoja na mambo mengine ya kindotondoto wakati ambapo mamilioni ya watu katika jamii hiyo hiyo wanaendelea kuteswa na kugandamizwa. Kazi za namna hii husifiwa sana na vyombo vya habari, majarida na wahakiki; na zile zinazojaribu kuwazindua na kuwaelemisha wanyonge zinapigwa vita vikali.

Hapa Senkoro anapinga kuweko kwa ushairi unaopumbaza na kuuzubaisha umma kama anavyodai Mayoka.

Muundo huu wa nadharia ya ushairi unaelezwa na Mayoka (1986) kwa kusema:

> Katika kitabu hiki, tungo kama za Kezilahabi, Kahigi, Mulokozi na wengineo watungao tungo tutumbi zisizokuwa na sanaa yoyote nimezitupa pembeni... mwundo wa mashairi yote yaliyomo kitabuni humu ni wa asili ya Kibantu. Kila utungo wa shairi umefungika upande wa mistari; *ni lazima kila ubeti wa shairi* uwe na idadi maalumu ya mistari; umefungika upande wa mizani; *ni lazima kila mstari uwe na idadi sawa ya mizani.* Mashairi yote yaimbwa; yaweza pia kusemwa au kusomwa tu. Tungo zisizotimiza yote hayo si mashairi (5).

Senkoro anasema kuwa muundo huu wa *lazima* anaousisitiza Mayoka ni wa sheria za kirasimu ambazo zinapingwa na akina Kezilahabi, Kahigi, Mulokozi na wengineo wanaoeleza kuwa si wa lazima. Anaendelea kusema kuwa huu ni udhaifu kuviita vipengele viwili au vitatu *uti* wa kazi hiyo. Ziko nyimbo nzuri nzuri ambazo hazifuati muundo huo wa vina na mizani katika fasihi simulizi na andishi ya Kiswahili. Anawaelekeza kidole watunzi wanaosisitiza mno muundo huo kuwa wana mtazamo wa kimwinyi waliourithi bila kuzingatia asili yake. Mtazamo huu unalenga tabaka hilo nyonyaji ambalo huweka sheria mbalimbali za kuulindia utamaduni wake. Utamaduni huu hutenganisha jamii na wao hujifanya kuwa ndio wenye hekima. Hawa huanza utunzi wao kwa dua na kujinyenyekeza kwa Mungu ilhali ni wanafiki. Anasema kuwa *sanaa ni uoanaji mzuri wa fani na maudhui katika kazi ya mwigo aifanyayo mtu*; *kazi ya sanaa hukua, hubadilika na hupigwa vikumbo na mikakati ya kijamii na kubakia historia tu. Tanzu hizi zikisimama kidete bila mabadiliko huchachuka. Hii ina maana kuwa kanuni katika sanaa huzidharau na kuzitoa uhai sanaa hizo* (7).

Katika utangulizi wa diwani ya *Jicho la Ndani* ya Mohamed (2002), Wamitila anakoleza wazo hilohilo la wanamabadiliko kwa kusema:

> Katika mashairi huru mwandishi anatukumbusha ukweli tunaoufahamu kama wahakiki: vina na mizani sio lazima katika ushairi kama ulivyo wizani. Licha ya kuwa mashairi haya huitwa huru, utunzi wake hauwi huru kabisa. Kuna sifa kadha

zinazodhibiti muundo wake na yamkini wapinzani wake wa awali walishindwa kuitambua sifa hii ya kimsingi.

Mhakiki huyu anatusawiria sifa za kiisimu na kimatini. Anasema kuwa sifa hizi hujitokeza kwenye minyumbuliko ya maneno, mishororo, na utaratibu wa ubeti. Katika diwani hii tunapata matumizi ya tamathali za usemi kwa wingi. *Mbinu ya fasihi simulizi pia inajitokeza kwenye mashairi kadha.*

Naye Abdilatif Abdalla(1973) anaueleza ushairi kuwa:

> Utungo ambao katika kila ubeti kuna ulinganifu wa vina *vitukufu* vilivyopangwa kimoja baada ya chenziye; wenye vipande vilivyo na ulinganifu wa mizani zisizo pungufu wala zilizo zaidi; na vipande hivyo viwe vimepangwa na maneno ya mkato maalumu na yenye lugha nyoofu, tamu na laini, lugha ambayo ni telezi kwa ulimi kwa kuitamka, lugha ambayo ina uzito wa fikra, tamu kwa mdomo wa kuisema, tumbuizi kwa masikio ya kuisikia na yenye kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ulivyokusudiwa.

Huyu anatilia maanani sifa za kiarudhi za wanamapokeo. Wataalamu wengi tulionukuu wanatuonyesha umuhimu wa kipengele cha lugha ingawa kwa mitazamo tofautitofauti. Wale wanaopinga juhudi za wanamapokeo hawaungi mkono ukuishi wa kanuni hizo za wanamapokeo. Malumbano yote hayo yanajitokeza katika karne ya ishirini. Lengo letu ni kuonyesha athari za fasihi simulizi katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* bila kutilia maanani malumbano hayo kwa sababu falsafa ya jamii ya Kilwa inajitokeza kwenye utenzi huo. Dhamira ya mtunzi pia inajitokeza kwenye fani ambayo tunaipigia tochi kwa undani sana.

## 2.2 MAANA YA USHAIRI

Ushairi ni utumizi wa lugha inayoeleza wazo la msanii kwa njia ya mkato. Mshairi huteua maneno hayo kuzua hisia za furaha, sikitiko, huzuni n.k. Kwa hivyo mkusanyiko wa hisia kama hizo mara nyengine humpa taabu msomaji ambaye hutaka kujua maana anayokusudia msanii. Kwa hivyo ni lazima msanii afanye uteuzi wa maneno kihodari ili maana anayolenga ijitokeze vilivyo. Katika shairi la 'Mrithi nini Wanangu?'katika *Kina cha Maisha* (1984) Mohammed anasema (17):

Sina Ngo'mbe    Sina Mbuzi
Sina Konde    Sina Bazi
Sina Leo    Sina Jana
Sina Zizi    Sina Shina
Sina Utu    Sina Haki.

Kwanza, angalia mizani mbili mbili katika kila neno. Mdundo unatokana na matumizi ya mizani hizi mbili mbili. Anatumia takriri kwa kurudia neno *sina* ili msimamo wake ujitokeze. Hali ya kukata tamaa inaambukizwa watoto wake. Dhiki hizi zinamwuma sana.

Kwa hivyo, katika kutuangazia lengo lake katika shairi mtunzi hutumia fani mbalimbali. Hapa anatuonyesha lengo lake kwa kutumia maneno yenye mizani mbili mbili. Vilevile anatumia dhana ya umbo; anatumia lugha teule na yenye mkato kutusawiria hisia zake.

Vile vile mtunzi hutumia maneno na sauti zinazopangwa kwa ujuzi. Mpangilio huo hujitokeza kama beti ambazo dhamira zake ni kusawiri mawazo, hisia au masiala fulani katika jamii. Ushairi unaweza kuimbwa, kukaririwa au kusemwa. Ushairi huwa na mpangilio maalumu kwa mujibu wa sheria zake hasa zile za wanamapokeo. Mashairi yanaweza kuandikwa au yasiandikwe. Tofauti ya dhana hizi mbili ni wakati wa utendaji. Mashairi yasiyoandikwa huwa na mvuto zaidi kwa sababu msanii anaweza kutia maneno ambayo hayapo kwenye shairi lake. Anaweza kurefusha shairi hilo kwa kuhusisha

hadhira ambayo anaielewa. Matarajio mengine ya hadhira humfanya mshairi ageuze mbinu za kughania shairi hilo. Anaweza akataja majina ya baadhi ya hadhira iliyoko. Pia shairi huweza likaghaniwa na watu wawili au zaidi ambapo mlumbi huanza na mwingine au wengine wakaitikia kwa kutumia kibwagizo. Mashairi mengine huhusisha makundi mawili yanayojibizana. Mashairi yasiyoandikwa hughaniwa mbele ya hadhira au kando. Kwa mfano watu wawili wapendanao huweza wakaimbiana nyimbo ili wajenge hisia zao, au msichana anaweza akamwimbia mpenzi wake akiwa peke yake wakati anapokwenda kuteka maji mtoni au kisimani. Kwa mfano, katika shairi la 'kutendana' kwenye diwani ya *Sauti ya dhiki* ya Abdilatif Abdalla (1973) msimulizi anasema (89):

Mwanamume : Kama bure utanipa, nipa sinisumbuliye
kama hutaki *takopa,* nikulipe baadaye
Hivi sasa cha kukupa, sina; kweli nikwambiye
Mtu huwa hakutupa, afaapo mwenziye.

Mwanamke : *Sina* kila siku *sina*, *sina* kwako maisha
Huna siku utanena; ninacho kanirambisha
Hiyo *sina* yako Bwana, sasa ishanichokesha
Nyege ni kunyegezana, kwangu huba zinkwisha.

Katika ubeti wa kwanza mtunzi anatumia vipengele vya fani kama *takopa* ambayo ni inkisari, *mwenziye* badala ya mwenzi wake; na katika ubeti wa pili anarudiarudia neno *sina* ili atuonyeshe uchoshi unaompata huyu mwanamke na , inkisari *kanirambisha;* badala ya *ukanirambisha.* Anatumia mbinu hizo kwa kukidhi mizani na kutuangazia maana teule anayotusawiria.

Mshairi wa fasihi simulizi pia, ana uwezo wa kutumia viungo vya mwili wake kama kukunja uso, kutumia miguu au mikono yake ili kusisitiza wazo fulani. Pia maleba na vifaa kama ngoma hufanisha sana shairi. Mavazi kama nguo iliyotengenezwa na ngozi ya

simba, kofia ya ngozi ya chui, bangili na vikuku hufurahisha hadhira, na tena sauti ya ngoma na pembe huongeza msisimko wa hadhira.

Mashairi huwa na majukumu makubwa kwa sababu maana ya shairi hujitokeza kutokana na mpangilio wake hasa katika mashairi ya kimapokeo. Matumizi ya lugha wakati mwingine huvutia maana huwa na beti zenye mistari yenye silabi zinazolingana katika mishororo yote, mistari hiyo inapangwa katika beti, huwa na wizani inayoleta mdundo unaofanana, na matumizi ya maneno hulenga maana maalumu. Katika lugha ya kawaida hatuongei wala kuandika hivi.

Kimsingi mtunzi huteua maneno na kuyapanga ili yavutie hisia za msomaji maana matumizi ya wizani na vina havitiliwi maanani katika matumizi ya lugha ya kawaida. Lazima tuelewe kuwa maudhui ya shairi hutokana na mpangilio wa maneno katika shairi. Shairi hutueleza juu ya masuala fulani, huathiri hisia, hujenga picha akilini mwetu na hutoa taarifa. Shairi hutueleza mambo ya kimsingi. Kwa hivyo, wakati tunaposoma shairi lazima tutambue namna mtunzi anavyotumia lugha teule, na kuwa lugha yenyewe haipatikani katika lugha tumizi ya kawaida. Mara nyengine tunavutiwa na shairi kwa sababu husisimua lakini tukitegemea hisia zetu wakati wa kulichambua tutachambua hisia zetu kuliko kuchambua yaliyomo kwenye shairi hilo.

## 2.3 CHIMBUKO LA USHAIRI

Ushairi ulianza na zile nyimbo ambazo zilikuwa zinaimbwa kwenye hafla kama matangani, unyagoni, mavunoni,n.k. Nyimbo hizo hazikuwa na utaratibu wa vina na mizani lakini baadaye manju walianza kufikiria na kutunga nyimbo zenye mdundo ambao unahitaji vipengele vya vina na mizani. Baadhi ya manju hao ni kama Fumo Liyongo ambaye aliishi katika karne ya kumi na nne. Mringwari ndiye Sultani wa Pate na alikuwa na njama za kumwua. Kule uhamishoni anaimba hivi:

Mwana wangu nakusimulia
Ya Liyongo Fumo na vishaka
Hana kufu huishi huria
Wamfanya Fumo wa wa nyika.
Knappert (1979:70).

Nyimbo zake hazikufuata sana arudhi ya vina na mizani. Katika wimbo huo, mizani ni kumi katika kila mshororo; vina vya mshororo wa kwanza na wa tatu ni patanifu, navyo vina vya mshororo wa pili na vya mshororo wa nne vimefanana.

Kwa muda mrefu nyimbo hizo ziliimbwa kutoka kizazi hadi kingine bila ya kuziwekea kumbukumbu ya kimaandishi. Baadhi ya nyimbo hizo zilipotea na nyengine kuzuka. Zile ambazo ziliendelea hadi wakati wa maandishi zilibadilika kwa sababu ya kutohifadhiwa kisawasawa. Hata hivyo zilikuwa na jukumu kubwa katika jamii. Zinaeleza juu ya maisha ya binadamu kuhusu harakati zake duniani. Zinaonya, zinakanya, zinatoa mawaidha na kumwelekeza njia nyoofu.

Nyimbo pia huburudisha na nyengine hutoa maonyo kwa jamii. Wakati wa kuimbwa, nyimbo hizo pia huwa na malengo mengine hasa waimbaji wanapojibizana. Mwimbaji wa nyimbo huibua hisia alizonazo moyoni mwake akijiambia na huku akijisikia mwenyewe.

Katika ushairi kuna aina kadha za tungo. Kuna nyimbo ambazo huimbwa na mtu binafsi au kundi la watu wakati wa shughuli fulani kama kulima, kuwinda au kuvuna; na kuna nyimbo ambazo zina maana ya utanzu mmoja na ushairi wa Kiswahili; na hizo nazo huimbwa. Ziko nyimbo za jadi kama hizi:

Tuyapokelezeke kwa wazee wao washamba
Washamba milele wake na waume sambasamba
Nti teule siyo yenye kumea mgomba.
Haji na wenzake (1981:50).

Huo ni wimbo wa utanzu wa ushairi ambao unafuata mpangilio wa vina vinavyopatana, lakini idadi ya mizani inatofautiana. Wimbo huo ni wa kijadi na unapokezanwa kutoka kizazi hadi kingine, na una mishororo mitatu; lakini ziko nyimbo za mistari miwili miwili kama huu ufuatao:

> Aniwekee mwao simtambui ni nani
> Mpigwade kwenda kwao mpigwa kwao huendapi?
>
> Haji na wenzake (1981:50)

Wimbo huo haufuati arudhi ya vina na mizani.

Mwimbaji anatumia mafumbo katika wimbo huu. Mtunzi huona kwamba maelezo ya uwazi hayawezi kuibua hisia zake sawasawa; kwa hivyo hutunga nyimbo ambazo maudhui yake hufichika kwenye mafumbo. Nyimbo hizo zilikuwa na maneno ya hekima ambayo yalibeba hisia za mtunzi, vile vile, zina miongozo kwa jamii anamoimba. Mtunzi hutumia lugha nzito.

Nyimbo hizo ziliimbwa barani mwote Afrika lakini kule Uswahilini ziliibuka zaidi katika eneo la pwani ya Afrika ya Mashariki tangu Rasi ya Gwardafui mpaka kusini mwa Rasi ya Galgado. Pia zilienea bara mpaka Uganda, Tanzania na Kongo. Vile vile, usafiri wa baharini wa wageni na wenyeji wa upwa huo ulisambaza nyimbo hizo kwenye visiwa vyote hadi Ngazija. Kwenye sehemu zote hizo nyimbo hizo ziliimbwa kwa kutumia lahaja mbalimbali kama vile Kiunguja, Kibajuni, Kipemba, Kingozi, Ki-mvita, n.k. Kimsingi, lahaja zote hizo ni za Kiswahili lakini misingi yake ni Kibantu.

Pia tunapata ushairi ambao huelezea historia ya jambo fulani au chanzo cha jamii fulani. Katika karne ya ishirini kulizuka ushairi huru ambao hautilii maanani ushairi wa jadi. Ushairi huo una maudhui mbalimbali kama vile maonevu kwa wanawake, uozo katika jamii, vita, ufisadi, n.k.

## 2.4 MAENDELEO YA USHAIRI

Mazrui na Syambo (1992:43) wanasema kuwa mbinu za vina na mizani katika ushairi wa Kiswahili zinatokana na mambo mawili; kwanza, nyimbo ni sanaa inayotegemea mdundo, na kila mdundo ukizidi wimbo nao huzidi kusisimua zaidi. Kwa sababu hiyo manju wa Kiswahili waliongeza mdundo kwa kuanza kutumia vina na mizani.

Ushairi wa Kiswahili ni usanifu ambao hutuangazia utamaduni wa pwani na dini ya Kiislamu. Utamaduni huo unanasibisha Waswahili na maingiliano yao na Waarabu. Hata *Hamziyyah* ambayo usuli wake ni Arabuni inasisitiza juu ya utamaduni wa dini ya Kiislamu. Mtafsiri wa utenzi huo anatumia msamiati wa Kiarabu na wa Kiamu kwa sababu wakati huo lahaja ya Kiamu ndiyo lugha ya usomi kule Lamu. Hata watunzi wa mwanzo mwanzo wa ushairi wa Kiswahili wana usuli wa Kipwani; na ni baada ya karne ya kumi na tisa ambapo watunzi wa nje ya mkoa wa pwani walipoanza kutunga ushairi wa Kiswahili. Ueneaji huo wa ushairi wa Kiswahili ulienda sambamba na ueneaji wa lugha ya Kiswahili nje ya pwani wakati wageni walipokuwa wakifanya biashara tofautitofauti kule bara ya Afrika ya Mashariki, Afrika ya Kati na Afrika ya Kusini. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ilitambaa bara kwa mujibu wa shughuli mbalimbali, huku ikikuza na kueneza ushairi wa Kiswahili.

Tukiangazia dhana ya ushairi, tunaona kuwa ushairi pia huibua hisia za kimapenzi. Mfano mzuri ni lile shairi ambalo Fumo Liyongo anamsifu mpenzi wake. Anasema:

Nitaanza kichwani
Ndugu zangu, sikieni
Ni hariri laini
Nywele zake za singa.

Masikio yake,
Yamsikizayo
Yametenda tao,
Kama kombe la nanga.

Uso wake mwana huyo
Umetengea kwa uzuri
Naapa sijaona
Kutoka mwanga hivyo.

Afumbapo macho
Hasa ayafumbuapo
Mtu akiwapo
Humtisha asiyatazame.

Lambert (1973)

Hapo Fumo Liyongo anamsifu mpenzi wake. Utungo huo haukufuata arudhi ya vina na mizani. Neno *hariri* lina maana ya nyuzi zinazotokana na viwavi vya nondo. Neno hilo lina asili ya msamiati wa Kiarabu. Msamiati kama *yamsikizayo, yametenda* na *umetengea* ni wa Kiamu. Neno *nanga* lina asili ya Kiajemi. Ni kifaa kinachotumiwa kusimamishia jahazi. Hapo tunapata athari kidogo za msamiati wa kigeni.

Vipindi vya ushairi ni vitatu. Kipindi cha kwanza ni kile cha ustawi wa miji, utamaduni na tawala za Waswahili ambacho kilidumu kwa miaka mia sita mpaka kikamalizwa na uvamizi wa Wareno. Wakati huo tunapata tungo kama *Swifa ya Mwana Munga, Chuo Cha Herekali, Utenzi wa Vita Vya Badri, Utendi wa Ayubu, Utendi wa Mikidadi na Mayasa, Siri li-Asrali, Ayi Wangu Wangu, Utendi wa Qiyama, Kasida ya Burudai, Al-Inkishafi, Dura Mandhuma* na *Utenzi wa Shufaka.*

Tenzi ni tungo ambazo maudhui yake hutuelezea mambo ya kihistoria na watu wake waliotenda mambo ya kutajika. Nyengine huzungumzia maudhui ya kidini na hutueleza mambo ya mashujaa kwa kina kirefu.

Nyingi ya tenzi hizo zina maudhui ya kidini. Lugha inayotumika ni Kiamu na Kiarabu. Maudhui ya kidini yanaangazwa na Seyyid Aidarusi Uthman (1652) ambaye ndiye aliyetafsiri *Hamziyyah* katika lugha ya Kiswahili katika ubeti wa 86, anasema:

Kamtosheleza Mola wake wamulumizio
Kwa ngapi udhua wa kaumu kuhizi mema.

Aidarusi alitafsiri *Hamziyyah* kwa lugha ya kale au Kingozi. Muundo wa shairi hilo ni mishororo miwili yenye mizani kumi na sita katika kila mshororo. Vina vya mishororo hiyo si patanifu. Maudhui ya utenzi huo na baadhi ya tenzi nyingine yanafanana kwa sababu yanaongea juu ya dini ya Kiislamu.

Tukichunguza lugha ya Muhamadi Kijumwa (1913) kwenye *Utendi wa Fumo Liyongo* lugha ni nyepesi zaidi kuliko ile ya *Hamziyyah.* Kwa mfano:

224. Make Liyongo hakika
Matanga aliyaweka
Watu wakasikitika
Kwa Liyongo kuifia.

225. *Liyongo silaha yetu*
*Kwa wut'e khasimu zetu*
*Alikuwa ngao yetu*
Wut'e wakinena haya.

226. Mui walisikitika
Hakuna wa kutosheka
Kwa Liyongo kutoweka
Imeanguka paziya.

Badala ya mama yake anasema *make;* kujifia, *kuifia;* wote, *wut'e;* kwa maadui wetu wote, *kwa wut'e khasimu zetu;* mji, *mui:* Vina vinabadilika katika kila ubeti, ingawaje vinapatana katika ubeti mmoja. Kina cha bahari ni *–ya* katika utenzi mzima. Kila mshororo una mizani nane.

Katika *Utenzi wa Swifa ya Mwana Munga* uliondikwa na Muhammad bin Sheikh (1531). Fumo Liyongo anamsifu Mwana Munga kwa wimbo ufuatao:

1. Pijani mbasi
Pembe za jamsi
Kwa cha mtotosi
Au Mwana Ninga.

4. Waye wa kileti
Wa mbeja wanati
Tupane sauti
Tumsifu Yanga.

9. Yake mashikio
Apulikiao
Yatendele tao
Kama kombe nanga.

14. Puaye ajabu
Zifungu hurebu
Ni sita hisabu
Mwenye kuziwanga.

Kwenye shairi hilo tunapata mishororo minne katika kila ubeti. Vina vyake ni patanifu. Vina hivyo hubadilika katika kila ubeti. Kina cha mshororo wa mwisho ni *–nga.* Kila mshororo una mizani sita.

Watunzi wanaofuata ni kina Bwana Mwengo wa Athumani aliyetunga *Utenzi wa Herekali* unaosimulia juu ya vita baina ya majeshi ya Mtume Muhammadi na yale ya Mfalme Heraklios. Bwana Mwengo naye anarithiwa na mwanawe Bakari wa Mwengo, mtunzi wa *Utenzi wa Katirifu* na *Utenzi wa Mwana Fatuma.* Naye Sayyid Abdallah bin Ali bin Nassir (1800) akatunga *Utenzi wa Al-Inkishafi.* Kwa kiasi kikubwa tenzi hizo pia zinafuata arudhi ya kimapokeo.

Tenzi za Kiswahili husimulia kitu kimoja kwa urefu sana. Tungo hizo mara nyingi hufuata arudhi. Tenzi huandikwa kwa sababu ya urefu wao. Maelezo yake hutiririka moja kwa moja, na hazimpi msomaji taabu sana ya kuzielewa. Lakini ushairi na nyimbo unaweza kutolewa papo kwa hapo kama mazungumzo.

Watunzi wa mashairi huelezea mambo ambayo wamefungua macho na kuyaona, wakakua nayo na kujihusisha nayo. Hiyo ndiyo sababu mashairi mengi ya kisasa yanaangaza juu ya harakati za ukombozi, siasa, uchumi, mageuko ya tamaduni na usambazaji wa imani ya dini kadha. Tukichunguza *Al-Inkishafi,* Seyyid Abdallah bin Ali anazindua jamii ili waone maovu ya binadamu. Anauzindua moyo wake kwa kusema;

64. Moyo nakwambia kwa watu sao
Kalamu ya Mungu iwapeteo
Nawe, kwa yakini kuwa kamao
Au una yako uyashishiye.

65. Moyo, taadabu, sipekete
Ata ya jauri haki ushike
Wendo wachokoke nawe wokoke
Moto wa Jahimu usikutwaye.

Mtunzi anakidhi sheria ya vina na mizani. Kila ubeti una mistari minne, na kila mstari una mizani kumi na moja. Mishororo hiyo haina vina vya kati.

Tenzi pia huwa na uamilifu wa kusifu, kuapiza, kutia ila, kujigamba, kutumbuiza, n.k. Tukichunguza *Utumbuizo wa Gungu,* Fumo Liyongo anasema:

1. Pani kiti nikae kitako
Tumbuize wangu Mwana Nazi
Tumbuize wangu mwanamke
Mupangua hamu na simanzi.

2. Husimama tini mwa mulango
Kwa nde kenda matembezi
Kiwa nde kangia shughuli
Kawaambia wakwe waandazi.

3. Kawaambia Sada na Rehema
Nywi endani musitaazi
Nywi endani tendani haraka
Muandae wali na mtuzi…

Lambert (1986:46)

Utungo huo una beti tatu. Kila mshororo una mizani tofauti tofauti. Vina havifanani. Mpaka sasa tunaangazia jinsi kipindi hicho cha kwanza kinavyotawaliwa na tungo za Fumo Liyongo. Wakati huo miji ya pwani ilikuwa ikijitawala yenyewe. Lugha katika tungo hizo haina athari nyingi za msamiati wa lugha za kigeni isipokuwa *Hamziyyah* na

*Al-Inkishafi* zina athari ya lugha ya Kiarabu na utamaduni wa dini ya Kiislamu. Hata maudhui ya tungo nyengine yanasawiri utamaduni na tawala za Waswahili mpaka wakati ambapo Wareno walivamia upwa huo wa Afrika Mashariki. Tungo za Fumo Liyongo zilihifadhiwa kwenye bongo za jamii mpaka zilipoanza kuandikwa karne kadha baadaye. Uandishi wa tungo hizo ulianza mwanzo wa karne ya kumi na tisa na ya ishirini. Mmoja wa watunzi hao ni Mohamedi Kijumwa aliyetunga *Utendi wa Fumo Liyongo* mwaka 1913. Utendi huo unatambua ukale wa maudhui ya kihistoria. Tungo hizo za Fumo Liyongo zinatuangazia kipindi cha ustawi wa miji ya upwa wa pwani na utulivu uliokuwako katika upwa huo. Baadaye miji ya Kilwa, Mombasa na Pate ilididimia kwa sababu ya ulafi wa Wareno hao ambao walivamia biashara zote katika Bahari ya Hindi.

Kipindi cha pili ni kile cha Wareno ambao baada ya kuwapiga Waturuki na Wagujerati mwaka 1509, na kuteka Malaka mwaka 1511, walitawala upwa mzima kibiashara hasa ile ya vikolezo. Wareno hao walipigwa na dola ya Omani. Kipigo hicho kinashangiliwa na mshairi mmoja kule Mombasa. Anasema;

Enda Manoeli ututukiziye
Enda na sahibu ujitutuziye.
Knappert (1979:18).

Ubeti huo unafuata kanuni za wanamapokeo za vina na mizani. Una mishororo miwili. Hauna vina vya ndani, lakini vina vya nje vinafanana. Kila mshororo una mizani kumi na mbili.

Huo ndio wakati ambapo umaarufu wa Muyaka ulianza kuvuma. Alipokuwa akisafiri hadi Pemba alimuaga mkewe hivi:

Kwaheri mwana kwaheri, nenda zangu Ngezi- Maji
Nimeazimu kusafiri kwa pepo za maleleji.
Kwa malenge na shuwari, natawakali Mpaji;
Baada ya dhiki faraji, hakuna lisilokuwa

Knappert (1979:142) na Abdulaziz (1979:108)

Wimbo huo unafuata arudhi za mizani kumi na sita katika kila mshororo. Una mistari minne; vina vya ndani na vina vya nje vinafanana. Alitunga mashairi yenye maana fiche. Baadhi ya mashairi yake huongea juu ya mpenzi wake ilhali anamsimanga Sultani wa Zanzibari. Kwa mfano:

Kitambi changu cha gomba nilichokupa hidaya
Kumbe hivi kujipamba ukenda ukizingiya
Sikujua kana kwamba kuwa yatakuwa haya
Hivi sasa nivulia unipe kitambi changu.

Huko wendako mwandani jua likimaliza kutua
Husikii muadhini kwa p'endo kukutukua
Mwambie enda ngomeni ja hiki atanunua
Usiate kukivua unipe kitambi changu.

Ikiwa nimekikopa thamani mwisho tatoa
Ada ya deni hulipwa nawe haya wayajua
Mt'umke mwenye pupa daima huvundikiwa
Minawe hatuna dawa nataka kitambi changu.

Nipa mwenyewe haraka isijeshuka nazaa
Sihadaiki Muyaka siwe wa kunihadaa
Kwanza sikuwa na shaka nikasema tutakaa
Na sasa umenifaa nipete kitambi changu

Abdulaziz (1979:174).

Shairi hili lina beti nne. Lahaja inayotumika kwenye shairi hili ni Kimvita. Maneno *cha gomba* yana maana ya kilicho kipya; *kuzinga,* kutembea; *tukua*, chukua; *mwenyi,* mwenye; *hidaya,* zawadi; *iwa,* iwe; *huvundikiwa,* huvunjikiwa; *dawa,* utesi; *nazaa,* aibu na *nipete,* nimepata.

Wakati fulani watawala wa Mazrui walijiona mabingwa mpaka wakamuasi Sultani wa Zanzibari. Mtawala huyo wa Kimazrui alimwambia:

Hutaingia ngomeni
Na kuta zake hufiki
Pesi panga mkononi
Na midomo ya bunduki.
Knappert (1979:151).

Ubeti huo una mishororo minne ambayo inafanana kimpishano. Kila mshororo una mizani nane. Hauna vina vya kati.

Kabla ya Sultani wa Zanzibari kujibu madharau hayo Muyaka aliwaonya watu wa Mombasa. Anawaambia:

Ngome ni ngome ya mawe, na fusi za kufuiza
Ngome ni ya matumbawe na boriti kuikiza
Ngome wetwapo sikawe, enda hima na kufuza
Ngome imetuumiza, naswi tumumo ngomeni.
Abdulaziz (1979:18).

Ubeti huo una mishororo minne na kila mshororo una kina cha ndani na cha nje. Vina vyote vya ndani vinafanana kama vile vya nje katika mishororo mitatu ya kwanza; kila mshororo una mizani kumi na sita. Mpaka sasa tunaangazia mashairi ambayo yalitawala katika upwa wa Afrika ya Mashariki wakati huo.

Katika karne ya kumi na tisa aliishi Taylor ambaye alikuwa mmishonari. Alimudu fasihi ya Kiswahili kuliko mzungu yeyote aliyemtangulia. Huyo alikusanya methali za Kiswahili katika kitabu chake kiitwacho *African Aphorisms*. Anakutana na washairi maarufu kama Muhammad Sikujua na Muhammad Bin Ahmad Al-Mambassy. Mmoja wao anapomweleza juu ya Muyaka, Taylor akamwambia amtafutie fasihi yoyote kuhusu mashairi ya Muyaka. Kama si kazi ngumu ya Sikujua na Taylor kazi ya mtunzi huyo labda haingepatikana kabisa. Mmishonari huyo anajitosa kabisa na kufanya watunzi wengine wawe na msukumo katika fasihi ya Kiswahili. Baba wa rafiki yake anapofariki anaandika shairi hilo:

Ya Ilahi, umuweke, mpenzi wangu
Na mahaba yazidike, kwake na kwangu
Tuwe sawa, tupendeke, swi walimwengu.
Knappert (1979:234).

Shairi hilo la maombolezo ni aina ya ukawafi ambalo lina ukwapi, utao na mwandamizi. Lina mishororo mitatu na vina vipatanifu. Kila mshororo una mizani kumi na tatu. Ingawa utunzi wake haukuwa wa kisawa, Taylor hakurudi nyuma katika juhudi zake za kuendeleza fasihi ya Kiswahili. Si rahisi kuasisi kazi yake lakini aliwapa changamoto wasanii na wasomaji wa Kiswahili: Athari za tungo zake kwa waumini wa Kimisheni zimeenea Afrika Mashariki nzima. Tafsiri zake za kitabu cha Zaburi zinahitaji pongezi ingawa Kiswahili chake hakikuiingiliana vizuri. Kwa mfano:

Yuna heri aso njama, akenenda na wabaya
Kiumbe aso simama, kwa ndiya sio lekeya
Za wadhambi si za wema, wala hajajikaliya
Na wacheka mambo piya, kwa kikao cha wabishi.
Knappert (1979:236).

Ubeti huo una mishororo minne na kila mshororo una mizani kumi na sita na kuna upatanifu wa vina. Kitu muhimu ni kwamba ingawa si mzawa wa upwa wa Afrika Mashariki wala Afrika nzima, kiwango cha juhudi zake hakiwezi kudharauliwa.

Taylor anawachukua Waswahili kuwa watu wagumu kuridhisha. Kama hawatambui jitihada za tafsiri za wamishonari za Zaburi na nyimbo za sifa, basi hawafai kusaidiwa. Waswahili hao huwacheka hata Waswahili wenzao wanaoghani mashairi guni. Hata hivyo, uchunguzi wake unamwelekeza kuzamia ujuzi wa arudhi ya ushairi. Anaibuka na ujuzi huo na kuandika yafuatayo:

SIMI WANGU
Simi wangu mimi tena
Ni mali ya Muokozi
Nimekombozwa na Bwana
Na kumnyima siwezi.

Simi wangu siku zangu
uerevu wangu pia
nimempa Bwana wangu
na nitamtumikia

Simi wangu Mkombozi
amekwisha nikubali
mwisho atanipa ezi
kwa watu wake wa kweli.

Knappert (1979:237).

Vina vinapatana kwa mpishano. Kila mshororo una mizani nane. Ubeti wenyewe una mishororo minne. Beti zote ni tatu.

Tafsiri za Taylor za nyimbo za Kikristo ni dhana muhimu, kwamba nyimbo ni mashairi ambayo huimbwa, na hiyo ndiyo sababu anatafsiri nyimbo za sifa na Zaburi ingawa hazikufikia kiwango cha arudhi ya kimapokeo. Kimsingi msanii Taylor hakukata tamaa katika tafsiri zake maana ingawa tafsiri hizo zilipata upinzani, yeye alizidi kuendelea na shughuli hizo.

Haji na wenziwe (1981:51) wanasema: *Ushairi wa Taylor ulikuwa chanzo cha ushairi na shina lake, lakini hauwezi kuchukuliwa kuwa ni ushairi wa Kiswahili.* Wakimnukuu Taylor wanaandika wimbo huo:

Boriti ya Issa
Mti wa uzima
Umetupokonya mzigo
Kufa kwa imani
Tuliona vyema
Furaha kwetu daima.

Usijizuzuwe
U mtu mzima
Tela zindukana ujuwe
Ushike ibada
Ya Mola Karima
Sizuwe Tela sizuwe.

Yanatangatanga
Na vyuo kwapani
Atafuta mema haoni
Ibada ya Mola
Haiko somoni
Sizuwe Taylor sizuwe.

Wataalamu hao wanasema kuwa tungo zake hazikuwaridhisha washairi wenzake lakini walizikubali huku wakimcheza shere. Beti hizo tatu hazionyeshi kaida yoyote ya kiarudhi. Idadi ya mizani zinatofautiana. Vina vya mishororo hiyo haviingiliani. Lakini wataalamu hao wanamsifu Taylor kwa juhudi zake zisizoonyesha kuchoka, kufa moyo wala kutilia maanani stihizai za watunzi wenzake. Ingawa maudhui ni ya dini, wakati mwengine uteuzi wake wa msamiati hupotosha mada.

Wakati huo pia tunapata nyimbo nyingi ambazo hazifuati arudhi za kimapokeo. Zilikuwa zikiimbwa wakati wa sherehe za matambiko. Wakati wa kukoga mwaka watoto wa vyuoni wa zama hizo huimba:

Si zetu, si zetu ni za mwalimu
Upanga wa mbao na kalamu zetu
Hamuwezi kuima
Liushapo wimbi angama

Tulijilie kushika moo, jumbe
Ndwisi wana wa Mawali, pembe
Pambavu kikupumbaa, pumbe
Jitu lisilo nadhari ng'ombe

Haji na wenziwe (1981:61)

Kwenye beti hizo tunaona dalili ya vina vipatanifu lakini mizani zinatofautiana kiidadi. Lakini baadaye sheria zilianza. Haji na wenziwe (1981:51) wanasema:

Kiswahili sina budi, kukipa sana makamo,
Ni lugha yangu ya jadi, kwa uzawa nimo humo,
Yanipatia muradi, na kunikuzia kimo,
Nitokapo ni jadidi, pia hemani nimo.

Haji na wenzake wanakipigia debe Kiswahili. Hapo tunapata ubeti wenye mishororo minne yenye mizani kumi na sita kila mmoja. Kila mshororo una vina vya ndani na vya nje. Vina vya ndani vinafanana, na vya nje pia vinafanana.

Katika kipindi cha tatu cha ushairi wa Kiswahili tunapambana na watunzi wengine ambao ni pamoja na Ahmad Basheikh Husein wa Mombasa, Shaaban bin Robert wa Tanzania pwani, Mathias Mnyampala wa Tanzania bara, Amri Kaluta Abedi wa Tanzania visiwani na Ahmed Nassir wa Mombasa.

Baadhi ya mashairi ya Basheikh na hata tenzi zake hazikuandikwa. Zile zilizoandikwa zimepatikana na kunukuliwa na Ahmed bin Nassir, mpwawe. Hii ni barua aliyomwandikia dada yake:

KUNENA NAWE SIKOMI:

Kunena nawe sikomi
Daima nakuuswiya
Sitindi wangu ulimi
Kuwa jema hakwambia
Utakuja uma kieni
Usikipate kimoja.

Nalizivunda shughuli
Kwa kutaka tangamano
Kunionya adhilahi
Sio yetu maagano
Hakika ndimi hamali
Ela hilo zito mno.

Nilipotanabahi
Vituko na lako inda
Niliapa kwa Wallahi
Sitozisairi nyonda
Siwezi ikirahi
Ingawa moyo wapenda.

Knappert (1979:244)

Kwenye barua hiyo kila ubeti una mishororo sita, na kila mshororo una mizani nane. Vina vinafanana kwa mpishano. Beti hizo hazina vina vya ndani.Basheikh ni mjuzi wa misemo, jambo ambalo limetanda katika lugha ya Waswahili. Kwa mfano:

Mkosa bahati, hawi ni azizi
Huwa na kahati, na ufumanizi
*Kuliko na miti, hakuna wajenzi*

Kuna na mishowe, na vitendo piya
Moyo sihadawe, ukajinamiya
Ndio wakatiwe, kuona duniya.

Majuto adhima, najuta utovu
Konde nalolima, la miti mikavu
Nalipanda zema, navuna ziovu.

Knappert (1979:245).

Shairi hilo lina beti tatu, na kila ubeti una mishororo mitatu. Vina vya ndani na vya nje vinafanana. Kila mshororo una mizani kumi na mbili.

Basheikh pia alikulia Uswahilini ambako kuna makanyo ya kila aina. Katika shairi hili anawakanya wake kwa waume. Anasema:

Wake kwa waume, tutahadharini
Kumengiya shume, mwetu mitaani
Apiga vikeme, hujipa thamani.

Fumbo tulifumbe, swifa tuzitiye
Na mangi tuyambe, waja wasikiye
Asokucha ng'ombe, huwa ngombe yeye.

Anajishaua, na kujipa zingo
Ni nazi ya panza, haina kirengo
Ujapo mjaza, huna budi pengo.

Yuajitengeza, mangi kuyataka
Ni kugereng'eza, shida kuungika
Kwa kula mteza, kheri kumwepuka.
Knappert (1979:253).

Shairi hilo lina beti nne, na kila ubeti una mishororo mitatu ambayo ina vina vya ndani na vya nje vinavyofanana. Kila mshororo una mizani kumi na mbili.

Basheikh aliingia ushairini baada ya Muyaka. Kifo chake na cha Shabaan Robert vilipishana kwa mwaka mmoja, yaani 1961 kule Mombasa na 1962 kule Dar-es-salaam mtawalia. Basheikh aliishi wakati wa utamaduni wa dini ya Kiislamu na mageuzi halisi ya utamaduni wa Waswahili.

Mtunzi mwingine ni Shaaban Robert; mtu wa kupendeza na mwenye maadili mengi kwa jamii ya Waswahili. Kwa mfano: (1969:46) anasema:

TENDO

Tendo bora ni mwangaza, na ada jitahidini
Jitahidini kuweza, matendo yenye thamani
Mwili ukisha kuoza, na roho kuwa mbinguni
Jina liwe laangaza, kwa sifa makumbushoni.

Ubeti huo una mishororo minne na vina vya ndani na vya nje. Kila mshororo una mizani kumi na sita. Vina vya ndani vinafanana, na hata vina vya nje vinafanana pia.

Mtunzi huyo alishughulikia maudhui ya kila aina. Maingiliano yake na wazungu ambao alikuwa akifanya kazi chini yao ni mapana zaidi kuliko yale ya watunzi wengine wa wakati wa kipindi hicho cha tatu.

Jambo hilo linajitokeza kwenye utunzi wake. Kwa mfano; kwenye *Pambo la Lugha* anasema:

HITLER

Vita vimeamuka, baada ya miaka sita
Hitler ameanguka, enzi yake imetota
Nchi alizoteka, kama umeme kumeta
Kwisha hii miaka, wenyewe wamepata.

Norway na Poland, Hitler aliseta
Ufaransa na Holland, kuwatawala alipata
Akatimiza ushindi, kila alipopita
Walakini England, ilimtia matata.

Robert (1947:5)

Kila ubeti una mishoro minne, na kila mshororo una kina cha ndani na kina cha nje. Vina hivyo vinafanana. Kila mshororo una mizani kumi na sita.

Mtunzi huyo hakujikita kwenye mtindo wa tarbia peke yake. Anasema:

DUNIA WAZIMU

Iwapo dunia, nipendayo sana,
Na nuruze jua, mwezi na mchana,
Kwa ulua, nguvu na ujana?
Umeshapotea, uzuri wa jana,
Na nilivyokuwa, sitarudi tena,
Kitu cha ukiwa, dunia naona.

Ina furaha zinapita mbio
Pia majeraha tunakwenda nayo
Ina mashabaha kama wa kioo
Na ndani karaha isiyo upeo
Ina na mzaha wengi waishio
Mara wana jaha mara hawanayo

Inazo anasa, ladha na mapenzi
Pamoja na visa sawa na ushenzi
Inakupa hisa kisha hukuhizi
Tena huwafyosa watu wa ujuzi
Mtu akikosa kilicho azizi
Hupata mkasa na mengi majonzi

Kama ahukumu mambo ya dunia
Mtu wa elimu huwa mkichaa
Na mtaalamu huwa kapumbaa
Japo afahamu mema na mabaya
Dunia wazimu – wazimu dunia
Inaleta hamu na majuto pia!

Robert (1959:66).

Shairi hili lina beti nne. Kila ubeti una mishororo sita na kila mshororo una kina cha ndani na cha nje. Vina vya ndani vinafanana, navyo vina vya nje vinafanana pia. Kila mshororo una mizani kumi na mbili.

Mshairi mwingine ambaye tunamwangazia ni Mathias Mnyampala. Mtunzi huyo alijishughulisha na kazi za nathari na ushairi. Maudhui yake ni ya kidini. Knappert (1979:276) anamnukuu:

Mungu unipe wagio
Nitowe masimulio
Nitimize kusudio
La Enjili kusifia.

Nieleze Enjili
Kwa kisa na minajili
Kwa lugha ya Kiswahili
Kwa tenzi nasimulia

Katika beti hizi mbili, kila ubeti una mishororo minne. Kila mshororo una mizani nane. Vina vya mwisho katika mishororo mitatu ya mwanzo vinafanana. Vina vya bahari vinafanana katika shairi zima. Hapo tunapata muundo wa tarbia kwenye utungo huo.

Katika diwani yake ya *Waadhi wa Ushairi* (1965:96) Mnyampala anasema;

96. Ni raia ndio vyombo, vilivyoundiwa meli,
Na pia nchi ni chombo, kimeundika kamili,
Kiongozi ni kiwambo, nahodha mwenye akili,
Raia ni mihimili, ikamilishayo jengo.

97. Hawafuati wajibu, njia ya unyenyekeo,
Hawaheshimu mababu, wazazi hata wa vyeo,
Huwatokea kwa gubu, na kashifa na kemeo,
Cheo huwa ni kileo, kwa mtu wa kulimbuka.

98. Ushikapo madaraka, sione hapo ni basi,
Ukaanza kupuruka, na mbawazo na nukusi,
Anga litaharibika, kwa zingio na weusi,
Dhamana mwendo wa ngisi, unyonge hauna mwisho.

Hapo anatueleza mambo ya kisiasa. Kwenye beti hizo tatu, kila ubeti una mishororo minne, na kila mshororo una kina cha ndani na cha nje. Vina vya ndani vinafanana; navyo vina vya nje vinafanana pia. Mishororo hiyo ina mizani kumi na sita kila mmoja.

Akiendeleza maudhui ya siasa, anawaambia jamii.

81. Maonyo haya ya kweli, uache kusitasita
Epukana na kitali, cha nyuma kukufuata,
Kwa wakubwa ujidhili, sije ukaula mwata,
Dara ya kheri sirata, kiburi si muungwana.

Katika ubeti huo tunaona kwamba una mishororo minne. Kila mshororo una mizani kumi na sita. Ubeti huo una vina vya ndani na vya nje ambavyo vinafanana.

Akilalamika juu ya uvundifu wa wakoloni, anasema:

91. Ukoo huwa kabila, makabila ndo taifa,
Ni desturi na mila, na ndilo jambo la sifa,
Kila nchi wa mahala, kila pande na tarafa,
Huwezi unda mataifa, kama huna makabila.

Wakoloni wamevunjavunja makabila. Ubeti huo una mishororo minne. Kila mshororo una mizani kumi na sita. Mishororo hiyo ina vina vya ndani vinavyofanana; pia vina vya nje vinafanana. Kina cha kati cha mshororo wa nne kinafanana na vina vya mwisho vya ile mishororo mitatu ya awali.

Akitusawiria dhana ya majaaliwa, anatwambia:

> 87. Akinipa ufakiri, mwili kuwa dhaifu,
> Nipambane nayo shari, taabu na maumbufu,
> Ndipo Mungu kighairi, sitapata tahafifu,
> Ni kazi yake Latifu, maisha kunipimia

Ubeti huo una mishororo minne ambayo ina vina vya ndani na vya nje. Kwenye mishororo mitatu ya mwanzo, vina vya ndani vinafanana, na vina vya nje vinafanana. Kina cha ndani cha mshororo wa nne kinafanana na vina vya nje vya mistari iliyotangulia.

Mtunzi huyo anazingatia nyanja mbalimbali katika utunzi wake; na jambo hili linamwelimisha msomaji vilivyo na kumpa tahadhari katika mienendo yake maishani. Kwenye kazi hizo tulizonukuu anaheshimu arudhi ya wanamapakeo.

Mathias Mnyampala ndiye mtunzi wa kwanza katika kipindi hicho cha ushairi ambaye hakuzaliwa kwenye upwa wa Afrika Mashariki. Ufanisi wake katika utunzi ni kielelezo kizuri hasa kwa washairi chipukizi kutoka bara ambao wanataka kujipurukusha kutokana na mazingira yao hadi kwenye kiwango cha watunzi wa pwani.

Mtunzi mwengine ni Kaluta Amri Abedi. Yeye ni Mwislamu na utunzi wake unaangazia dhana ya Uislamu. Katika ufuataji wake wa dini anaonya jamii dhidi ya mavazi mafupi, hasa ya wanawake. Anasema:

NGUO ZITEREMSHENI

Sitara kubwa kuvaa, vazi refu miguuni
Msiige bila njia, mabibi kuniradhini
Vazi refu kulivaa, ni sitara mwilini
Nguo ziteremsheni, yapungue maasai

Kuvaa fupi si njia, na avae muumini
Baba ni baya tambua, ingawa la uzunguni
Hujahuja kwa hatua, bibi rudi kwa Mannani
Nguo ziteremsheni, yapungue maasai.

Abedi (1963:32)

Beti hizo zina mishororo minne kila mmoja. Mishororo hiyo ina vina vya ndani na vya nje. Vina vya ndani vinafanana kama vinavyofanana vina vya nje. Kila mshororo una mizani kumi na sita. Kina cha ndani cha bahari kinafanana na vina vya nje vya ile mishororo mitatu ya kwanza.

Mpaka sasa watunzi hao wa karne ya ishirini ambao tunawazungumzia sasa ni marehemu, lakini Ahmed Nassir mpaka sasa yuko nasi kule Malindi. Mashairi yake yana tarehe; kwa hivyo ni rahisi kufuata mabadiliko ya ushairi wake kulingana na wakati anaotunga na ukuaji wa hisia zake. Nyimbo zake nyingi hazijaandikwa. Akimnukuu, Knappert (1979:289) anasema:

Nyota ng'ara, mwezi ung'iye kizani
Siwe jura, uso kainama tini
Si khasara, kurarukiwa mshoni.

Katika ubeti huo, mishororo yote ni mitatu; na kila mshororo una kina cha ndani na kina cha nje. Vina vya ndani vinafanana. Vina vya nje navyo vinafanana. Kila mshororo una mizani kumi na mbili.

Mashairi hayo yaliandikwa mwaka 1954 ambapo mtazamo wake kuhusu wanawake ni hasi. Sasa hisia zake zinapata msisimko mpya. Knappert (1979:289) anamnukuu. Anasema:

Mpende mwenye busara, ajuaye kujitunga
Sipende alo jura, kumbe asiye changa
Mpende mwenye subira, mweza njaa na janga

Mpende mwenye hisani, alopata kufadhili
Sipende mtu khaini, kwa Mtume hana kweli
Mpende aso undani, mwenye kakabili.

Katika utungo huo tunapata beti mbili ambazo zina mishororo mitatu kila mmoja. Mishororo yote ina vina vya ndani vinavyofanana; pia vina vya nje vinafanana. Kila mshororo una mizani kumi na sita.

Mtunzi huyo huchanganya lugha kwenye utunzi wake. Hutunga nyimbo za Kiarabu, Kiurdu, na karibu za lahaja zote za Wabantu wa pwani. Hapo anatohoa msamiati wa Kiingereza na kuuchanganya na msamiati wa Kiswahili. Knappert (1979:296) anamnukuu. Anasema:

Wataka apu tu deti, mamwinyi utamaduni
Na kusema woti ziti, dhozi olidi fesheni
Kutakufa na laiti, kidole ki mdomoni.

Ubeti huo una mishororo mitatu yenye vina vya ndani vinavyofanana; na vina vya nje pia vinafanana. Kila mshororo una mizani kumi na sita.

Nyimbo zake zinaongea juu ya mada kadha. Katika mwaka wa 1966 alisifu lugha ya Kiswahili ambayo alisema Wazungu waliikashifu kwa kutoelewa muundo wa msamiati wake. Knappert (1979:307) anamnukuu. Anasema:

Risala enuka hima, ukae ukaatwili
Nina jambo takutuma, ubalegheshe suali
Nipate jawabu njema, yenye amani wa kweli
Nauliza Kiswahili, ni lugha ya watu gani?

Hapo tunapata ubeti wenye mishororo minne na kila mshororo una mizani kumi na sita. Vina vya ndani vya mishororo mitatu ya kwanza vinapatana, na vya nje pia vinapatana. Vina vya mishororo ya kibwagizo pia vinafanana.

Wakati anapotunga mashairi mtunzi huwa na hisia fulani ambazo humjia akilini mwake na hutaka kuziibua ili ziwanufaishe jamii. Alipokuwa gerezani Abdilalif Abdalla alipata shida za aina kadha. Anautuliza moyo wake kwa kuuambia:

1. Usilie moyo wangu, siliye moyo nyamaza
Usijitie matungu, siliye tajiumiza
Huno ndiwo ulimwengu, muna yasiyopendeza
Kwa hivyo moyo nyamaza, zidi kuwa na subira.

4. Usiwe kama mkiwa, moyo wangu tangamka
Kwani mnyonge ukiwa, na matama kujishika
Ng'ara mfano wa juwa, uwate kuhuzunika
Sijiuwe kwa mashaka, zidi kuwa na subira.

8. Moyo kwamba halikuwa, ulilolitarajiya
Lisikupe kuingiwa, na simanzi na kuliya
Hivyo ndivyo mambo huwa, ni kama lumbwi dunia
Shika n'nalokwambiya, zidi kuwa na subira.

12. Haya ni mafunzo kwako, funzika moyo funzika
Tabu na misukosuko, si mwishowe kukufika
Katika uhai wako, hutaweza kuy'epuka
Muda yakikudiriki, zidi kuwa na subira.

Abdalla (1973:48).

Kwenye shairi hili, tunapata beti nne, na kila ubeti una mishororo minne. Kila mshororo una kina cha ndani na cha nje. Vina vya ndani hubadilika katika kila ubeti. Vina vya nje pia hubadilika katika kila ubeti.

Dhana ya kukuza ushairi iliposhika kasi baadhi ya watunzi kama Mohamed (1984), Kineene wa Mutiso (1986), Kezilahabi (1988), Kithaka wa Mberia (2002) na wengineo wakaanza kususia muundo wa kanuni za vina na mizani. Tungo zao zinakiuka sheria hizo, na kwamba zinaufunga ushairi wa Kiswahili. Akiwa mstari wa mbele Mohamed (1984:v) anasema;

> Nimekuwa nikuufuata ushairi wa Kiswahili kwa miaka mingi na kuuhisi kwamba kiwango chake cha kisanaa na kimaudhui hakikui wala hakibadiliki. Kutokua kwake kunatokana na dhana ya kuchukulia tu kuwa sifa kuu za ushairi wa Kiswahili ni vina na mizani, mwala na urari, kibwagizo na beti; na hasa zile zenye mistari minne (yaani tarbia).

Anachokisema Mohamed ni kwamba, maana ya ushairi imo kwenye maudhui yake. Lakini wakati huo huo, huyo Mohamed akiwa na wenzake Haji, Hamad na Omar (1981:54) wanaandika hivi:

Nakuasa usikie, usemaji ni karamu
Maneno usitukie, sema mambo kwa kupima
Utamkapo ujue, neno halirudi nyuma
Ukosapo neno jema, kheri ulinyamazie.

Kheri ulinyamazie, ovu huleta khasama
Majuto yasikujie, laiti nisingelisema
Mtu baba azuaye, motowe utamchoma
Ukosapo neno jema, heri ujinyamaziye

Kwenye hizo beti mbili tunapata mishororo minne katika kila ubeti. Vina vya ndani vya mishororo mitatu ya mwanzo vinafanana; na vina vya nje vinafanana katika mistari yote mitatu ya mwanzo. Kina cha kati cha mshororo wa nne kinafanana na vina vya nje vya ile mishororo mitatu ya mwanzo. Pia kina cha nje cha bahari kinafanana na vina vya ndani vya mistari mitatu ya mwanzo.

Mshairi huwa na neno linalomsakama ndiposa hubidi aliseme. Mawazo yake hulenga mtu au jamii anayoasa. Hutumia maneno na mafumbo yanayokidhi haja yake. Shairi hilo la Mohammed na wenzake linafuata sheria za utunzi wa vina na mizani, huku likiangazia mada kwa kutumia maneno teule na kanuni za utunzi wa kimapokeo. Kanuni hizo ndizo zinazotofautisha lugha ya ushairi na lugha ya tanzu nyengine; kwa hivyo utamaduni wa lugha ya ushairi hufuata utaratibu na sheria zake.

Mpangilio ambao ulishikiliwa na wale watunzi waliofuata arudhi ya vina na mizani unafuata kanuni ya mizani kumi na sita katika kila mshororo. Shabaan Robert (1968:62) anasema:

WOGA

Nina asili ya woga, hadithi yasimulia,
Mwenye siwa atapiga, ilie katika hewa,
Masikio mkitega, mtasikia hekaya,
Woga ni maji naoga, ghadhabu ikinijia.

Nina asili ya woga, tumewachiwa wasia,
Wazee wametukaga, kago jema kutumia,
Hakuna tanga kwa mwoga, wasia umesaka,
Woga ni maji naoga, ghadhabu ikinijia.

Nina asili ya woga, woga kwangu mazoea,
Woga umekuwa shoga, mimi nao twatembea,
Woga sipendi kuaga, marafiki tumekuwa,
Woga ni maji naoga, ghadhabu ikinijia.

Katika hizo beti tatu Shabaan Robert anafuata kanuni za arudhi za vina na mizani. Kila ubeti una mishororo minne ambayo ina vina vya ndani na vya nje. Vina vyote vya ndani katika beti zote tatu vinafanana; navyo vina vyote vya nje pia vinafanana. Kila mshororo katika beti zote tatu una mizani kumi na sita. Vina vya mishororo ya kibwagizo vya beti zote tatu vinafanana.

Wanamapokeo huchukulia sheria za vina na mizani kama ndiyo uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili.

Mpaka sasa tumechunguza mashairi yenye mishororo ya mizani kumi na sita. Kila nusu mshororo una mizani nane. Lakini Mohamed pia anaandika nusu mishororo ya kwanza yenye mizani nne na ile nusu ya pili ina mizani nane kama kawaida. Kwa hivyo kila mshororo una mizani kumi na mbili. Kwa mfano:

Ndiwe wewe, mwenye kuhozi suduri
Wewe ndiwe, wa awali na akhari
Ndiwe wewe, ulokithiri uzuri
Mwenginewe, sijali sina habari.

Ndiwe wewe, mekupenda kwa hiari
Wewe ndiwe, mdhibiti zangu siri
Ndiwe wewe, mtoa zangu nusuri
Mwenginewe, havuki yako kadiri.

(2002:20)

Katika beti hizo mbili kuna vina vya ndani vinavyofanana na vya nje pia vinavyofanana. Kwenye kipande cha kwanza cha kila ubeti anatumia takriri kwa mpishano. Kila ubeti una mishororo minne. Amebuni mtindo mpya wa mizani nne badala ya nane kwenye nusu mishororo ya mwanzo ya beti zote mbili, na amekidhi kanuni ya vina na mizani.

Tukihitimisha sehemu hiyo ya *Maendeleo ya Ushairi,* tunaona kwamba kila kipindi cha ushairi kina muundo tofauti na ile miundo ya vipindi vyengine. Katika kipindi cha kwanza, ushairi wa Liyongo Fumo ambao unasawiri utawala wa Waswahili hauna athari kubwa wa msamiati wa lugha za kigeni. Msamiati wa ushairi huo unatuangazia matumizi mengi ya lugha za Kibantu.

Katika kipindi cha pili cha ushairi wa Kiswahili taathira za msamiati wa Kiingereza na Kiarabu unajitokeza. Hata miundo ya ushairi huo una taathira kubwa. Nao utawala wa Kiingereza ambao ulijaa siasa, maonevu na kejeli dhidi ya Waswahili na lugha yao uliwatia motisha wasanii wa ushairi kukabiliana na watawala hao.

Katika kipindi cha tatu tunapambana na washairi wapya ambao ni pamoja na Basheikh Husein, Shaban Robert, Kaluta Amri Abeid, Mathias Mnyampala, Ahmed Nassir Juma, na wengineo. Washairi hao wanapatana na enzi ya utamaduni wa dini ya Kiislamu na mvurugo wa athari za lugha za kigeni. Pia tunapambana na washairi kama Abdilatif Abdallah, Sheikh Nabhany na Hasani bin Ismail mtunzi wa *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali.* Tenzi za wakati huo zinapanuka kimaudhui. Zinaongea juu ya ugandamizwaji, maonevu, usaliti, na tamaduni za jamii. Kwa kiasi kikubwa watunzi hao wanafuata kanuni za arudhi lakini wengine wanatanabahi na kusema kuwa kanuni hizo zinaselelesha upanuzi wa ushairi wa Kiswahili. Mjadala huo unafaa kutiliwa maanani baina ya wanamapokeo na wanamapinduzi kwa sababu nia kubwa ya ushairi wa Kiswahili ni kuasisi maendeleo yake na ya watumiaji wake.

## 2.5 ATHARI ZA WAGENI

Athari za vina na mizani zinatokana na majilio ya Waajemi na Waarabu ambao wamehamia katika mwambao wa Afrika ya Mashariki, na vizazi vyao vikaswahilika kilugha na kitabia. Walipoandika mashairi walianza kutumia arudhi waliyokuja nayo mpaka ikapata mashiko katika fasihi ya Kiswahili. Pia msamiati wa dini ya Kiislamu unatumika sana katika ushairi. Abdulaziz (1979:88) anasema:

> Mbinu hii ya kutia maneno ya lugha nyengine kama Kiarabu ni mtindo unaotumiwa katika arudhi ya Kiajemi ambayo, kama Kiswahili, kimeathiriwa sana na maneno ya Kiarabu.

Ushairi wa tarbia ambao ndio mtindo ulioshika kasi katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa unatokana na athari za Kiarabu. Nyimbo asili za Waswahili ambazo huimbwa harusini hazikuwa na vina wala mizani, na zinaweza kulinganishwa na zile nyimbo zilizoimbwa na jamii za Wabantu ambazo pia hazikuwa na vina wala mizani. Kulingana na Abdulaziz, nyimbo ambazo zina vina zinaweza kuwa na taathira ya Kiarabu. Mtindo uliojulikana kutumiwa na wasanii wa ushairi wa Kiswahili ni takhmisa na tenzi. Takhmisa katika ushairi wa Kiswahili zilizotokana na Kiarabu zina mistari mitano na vina vinavyofanana. Anaendelea kusema kwamba ukopaji wa arudhi ya Kiarabu ulikomea tu kwenye vina. Wasanii wa ushairi wa Kiswahili walishindwa kukopa mtindo wa mizani kwa sababu ya tofauti zilizoko kwenye silabi za arudhi ya Kiarabu.

Katika tafsiri ya *Hamziyyah* iliyoandikwa na msanii Mohamed bin Said al-Busiri, Seyyid Aidarus Uthman wa Lamu hakutia vina vya kati kama ulivyokuwa ule wa Kiarabu. Tafsiri hiyo ina taathira kubwa ya lugha ya Kiarabu. Kwa mfano:

117. Kwa khuluku njema ya Mtume soyo Karima
Kakimisha yambo kwa sumuye soyo ajama.

Ubeti huo una mishororo miwili, na kila mshororo una mizani kumi na tano. Hauna vina vya kati kama ile *Hamziyyah* ya Kiarabu. Tunapata athari kubwa za msamiati wa Kiarabu kama vile *khuluku, Mtume, Karima,* n.k. Kimuundo pia ubeti huo una mishororo miwili na vina vipatanifu.

Maingiliano ya Waarabu na wenyeji wa upwa wa Afrika Mashariki yameathiri lugha ya Waswahili kwa kiasi kikubwa. Jina *Swahili* linafafanua dhana hiyo maana lina asili ya neno la Kiarabu *Swahil;* pwani.

Wakati wa kipindi cha tatu cha ushairi wa Kiswahili Ahmad Nassir anaonyesha athari kubwa ya msamiati wa Kiarabu. Kwa mfano:

Ali gharibu gharibu
Eshi galu abidi
metoka kwenu kwa tabu
Jiiti hadha biladi
asukuti ya kidhabu
jaurizo usizidi.
Knappert (1979:297).

Wimbo huo una maneno kumi na sita ya Kiarabu. Neno *galu* ni kitenzi, yaani walisema; *jiiti,* amekuja; *asukuti,* unyamaze, n.k.

Katika karne ya kumi na nane tunapata mchanganyiko wa ushairi wa Kiswahili wenye msamiati wa lugha ya Kiarabu. Kwa mfano:

Mola atatupa raha
bi idhini – ka Ilaha
Knappert (197:296).

Msanii amejaribu kujenga arudhi kwa kutumia mseto wa msamiati wa lugha ya Kiarabu na lugha ya Kiswahili. Mishororo hiyo miwili ina mizani nane katika kila mshororo. Vina vya mwisho ni patanifu.

Pia neno *mvinyo* la Kiswahili lina usuli wa msamiati wa lugha ya Kireno, *vinho.* Neno *malaya* la Kiswahili pia ni msamiati wa lugha ya Kireno, *malaia* yaani mtumishi wa nyumbani wa kike aliyetoka nchi ya *Malay.* Maneno yote ya michezo inayochezwa mezani kama *karata, drafu, puli,* n.k. yana usuli wa msamiati wa Kireno. Wareno hao walileta athari zao katika upwa huo uliosambaa Waislamu. Waswahili wa kutajika kule Mombasa walijua Kireno. Hata hivyo, Wareno hao, licha ya kuathiri msamiati wa Kiswahili, lugha yao pia ilitumika kutungia mashairi. Muyaka anasema:

Portugesi afala, faliki afala velo
Baziada spanyola, wa tarafai busolo
Si nyama za kuanila, defedhati dafedhalo
Vinyu ina kusumbula, xx ina butizalo.

Abdulaziz (1979:90)

Ubeti huo una mishororo minne, na kila mshororo una kina cha ndani na cha nje. Vina vya ndani vina upatanifu. Vina vya nje pia ni patanifu. Kila mshororo una mizani kumi na sita.

Lugha ya Kiswahili ina elementi za Kibantu, Kiarabu na Kizungu. Lugha hiyo ya ushairi wa Kiswahili imehifadhi mizizi ya msamiati wa Kibantu. Kila neno la Kiswahili ambalo limekopa msamiati wa neno la kigeni hupigwa msasa kisarufi ndipo likatumika. Kwa mfano neno *club* la Kiingereza limeswahilishwa na kuwa *kilabu* na wingi wake ni *vilabu,* ngeli nomino ya nane. Neno *book* la Kiingereza vile vile limekuwa neno la Kiswahili *kitabu* na wingi wake ni *vitabu.* Baadhi ya maneno yaliyoswahilishwa ni clutch, *kilachi;* bonnet, *boneti;* radiator, *redieta;* bumber, *bampa;* n.k.

Uswahilishwaji huo haukujikita kwenye nomino tu. Kitenzi *retire* cha Kiingereza kimekuwa *ritaya.* Neno hili linaweza kunyambuliwa na kuwa *ameritaya, wataritaya, ningeritaya,* n.k.

Hapo tunapata lugha ya Kiswahili ambayo imejitokeza tangu karne ya kumi na tisa na ishirini kutokana na msamiati wenye asili ya Kiingereza. Katika mwaka 2006, mwimbaji Prezzo anatuangazia athari ya nyimbo zake za Kiswahili kutokana na msamiati wa Kiingereza. Anasema:

> *Mafans* mi nawapenda wote
> *Mahaters* kama hamnipendi
> *Meza* wembe
> Nawa *live* kama Saida Karoli.
> Na wenye wivu wajinyonge.

Mbali na kuvunja arudhi za wanamapokeo Prezzo anachanganya lugha. Badala ya neno *fans* la Kiingereza ambalo ni wingi wa neno *fan* anatia idadi ya wingi maradufu kwa kutumia kiambishi *ma* cha wingi katika lugha ya Kiswahili. Pia anatumia neno *mahaters* kwa idadi ya wingi maradufu. Neno *haters* ni wingi wa nomino *hater* ya Kiingereza, na *ma* ni wingi wa adui mmoja katika lugha ya Kiswahili. Kitenzi *meza wembe* kingekuwa katika wingi, *mezeni nyembe.* Vile vile anatumia neno la Kiingereza *live.* Mizani ya mishororo hiyo imehitilafiana pakubwa. Mshororo wa kwanza una mizani kumi; wa pili, kumi na moja; wa tatu, nne; wa nne, kumi na mbili na wa tano, tisa. Ubeti huo una mishororo mitano. Vina vya mishororo hiyo havina upatanifu.

## 2.6 MASHAIRI HURU

Ushairi huru ulianza kujitokeza mwisho mwisho wa miaka ya sitini ya karne ya ishirini. Baadhi ya wataalamu wa fasihi ya Kiswahili husema ushairi huu umewaokoa wasomaji kutokana na pingu za vina na mizani. Kufunguliwa kwa pingu hizo kulianza katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Mazrui (1988) na Diyanni (1994) wanasema kuwa ushairi huu umewatoa wasomaji kwenye uchoshi wa vina na mizani unaokithiri.

Wafuasi wa wanamapokeo ambao ni pamoja na Lambert (1971), Kitsao (1975), Kazungu (1982) na Arege (1998) wanasema kuwa ushairi huru ni mkusanyiko wa tungo anuwai za ufundi pungufu, na kuwa ushairi huu huasi kimakusudi ushairi wa wanamapokeo. Senkoro (1982) anaunga mkono wazo hili kwa kusema kuwa fani imechongoza katika umilisi wa lugha kuliko maudhui maana mtunzi akiwa na ilhamu ya kuandika, wazo la kwanza kabisa hutegemea ufundi fulani ambao ni fani. Kama baadhi ya watunzi wa Kimagharibi, wanamapinduzi pia wanaamini kuwa mashairi si vina na mizani pekee bali ni muundo, wizani pamoja na ufundi wa kutumia lugha ya mkato. Miongoni mwa waathiriwa wa mawazo hayo ni Kahigi na Mulokozi (1973, 1976 na 1979), Kezilahabi (1974 na 1988) na Mberia (1997). Kazi za Kithaaka wa Mberia zimeendelea zaidi kwa vile amepiga hatua moja mbele kwa kuandika mashairi ya mchoro. Katika *Mchezo wa Karata* (1992) anatumia boga linalokatwa katikati kuashiria raslimali ya kitaifa ambayo yafaa igawanywe sawasawa baina ya tabaka la chini na la juu. Mtunzi huyu anaasi mpangilio wa wanamapokeo kiarudhi.

Baadhi ya wataalamu wa fasihi pia wanadai kuwa ushairi wa Kiswahili haukufuata arudhi. Swala hili na kupinga dhana ya arudhi ya wanamapokeo linafafanuliwa na Kezilahabi anaposema katika *Kichomi* (xiii):

> Mtu yeyote akiniuliza
> Kwa nini vina mizani
> Situmii namistari na
> Beti zisitoshelezi
> Nitamwambia: *Rafiki*
> *Kuna njia nyingi za kwenda*
> *Bustanini.*

Lakini kama mtu yule yule
Kunizoza akiendelea
Nitamwambia:
*Rafiki, twende nyumbani kwangu.*
*Tukifika jaribu kunifunza*
*Kutembea.*

Anachokisema Kezilahabi ni kwamba kuna njia nyingi za kufanyia jambo lile lile moja. Yeye anaamini juu ya uhuru wa kufanya atakayo kwa njia aipendayo, bora tu maudhui ya kazi hiyo yamwangazie msomaji. Katika karne ya ishirini na moja wanamapinduzi wameendelea zaidi katika kupuuza arudhi za vina na mizani.

## 2.7 LUGHA YA USHAIRI

Lugha ya Kiswahili ilianza kuandikwa kwa hati za Kiarabu katika karne ya kumi au hata kabla. Uandishi huo uliambatana na imani ya dini ya Kiislamu. Kwa hivyo haishangazi kupata maudhui ya tenzi nyingi za wakati huo yanayohusu dini ya Kiislamu. Hata hivyo tenzi hizo zina msamiati wenye elementi za Kibantu.

Tenzi za mwanzo ni zile zilizojitokeza katika karne ya kumi au hata kabla. Miongoni mwa wasanii wa wakati huo ni Fumo Liyongo na Seyyid Aidarusi Uthman. Fumo Liyongo anakumbukwa kama msanii wa kwanza wa kutunga nyimbo kwa lugha ya Kiswahili. Tenzi na nyimbo zake hazikuangazia sana maudhui ya dini ya Kiislamu; lugha yake ina asili ya msamiati wa Kibantu. Alijihusisha na maudhui ya uwindaji, mapenzi, harusi, wakati alipokuwa anaoga na akinywa pombe. Huyu ndiye aliyetunga wimbo wa kwanza kuhusu mvinyo. Kwa mfano:

We mteshi ulo mnazini
Nipe uchi ulio uchungu
Nitekee wa kikasini
Tesheweo na mgema wangu.

Nitekea na wa kichupani
Ulokuya na wale wazungu
Nitekea ulio nyunguni
Ulopikwa kwa kunyinywa nyungu.

Kisharabu nikema mezani
Nalitaka embe kungu langu
Embe kungu latupalo mani
Latupalo ndani tungutungu.

Embe kungu langikwa changoni
Pangikwapo siwa wa mavungu
Pangikwapo magoma ya ezi
Na mawano ya bangu.

Knappert (1979:68)

Hapo tunapata msamiati kama *mteshi,* mgema; *uchi,* mvinyo; *kikasini*, neno ambalo limetoholewa kutokana na neno *cask* la Kireno; *tesheweo,* lililogemwa; *kichupani*, chupa ndogo; *ulokuya na wale wazungu. Kuya* ni lahaja ya Kiamu. Pia dhana ya *wazungu* inatudhihirishia kuwa Wareno wanabadilisha mienendo ya Waswahili. Maingiliano yao na Wareno yaligeuza miji ya pwani kuwa mandhari ya starehe. Neno *nyunguni* linatupa hisia ya ukale. *Nikema,* glasi; *mani,* nguvu za kiume; *siwa,* pembe ya kunywea pombe; *magoma ya ezi,* magoma ya uganga na *mawano mawano ya bangu,* mikuki ya kivita. Lugha katika nyimbo hiyo ina mchanganyiko wa msamiati wa Kibantu na Kireno. Lahaja ya Kiamu pia inajitokeza. Kwa mfano maneno kama *ulo kuya, siwa, mteshi, uchi, bangu* na *mani* ni lahaja ya Kiamu.

*Hamziyyah* iliyotafsiriwa na Aidarusi ina msamiati wa lugha ya dini ya Kiislamu. Kwa mfano:

i) Naanza kwa jinale Bismillahi lenye adhama
Na ar – Rahamani Muwawazi na ar-Rahima.

ii) Swifa na matelo ya jamali na kuyuwiya
Zisitahikile Moli wangu Mola a'lama

iii) Salana salamu za dawama mada dahari
Zimteleleye Muhammadi mwenye makama.

iv) Na alize zote na sahaba na wandamizi
Na wandamizao kwa sira njema

v) Baada ya sayo nyi ndu zangu nataka dua
Mola ayasiri nitakayo kuyawandama.

vi) Lianna niliko nina nia taka kutenda
Kitenzi cha siyi *Hamziyyah* lake kalima.

vii) Azitungilewo Muhammadi mwane Saidi
Al-Busiri utoleo wenye nadhima.

Hapo tunapata maneno kama *Bismillahi,* kwa jina la Mwenyezi Mungu; *Na ar-Rahamani Muwawazi* na *ar – Rahima,* mwenye kuwarehemu, mwenye huruma na mwenye Rehema; *matelo jamali,* matendo mema; *kuyuwiya,* kujua; *Moli,* Mola; *alama,* mjuzi; *swahaba,* wafuasi; *sira,* mfano; *mada dahari,* siku zote; *makama,* mwenye utukufu; *dawama,* daima; *Lianna,* kwa sababu; *kalima,* neno; *nadhima,* mtungo n.k. Neno *adhama* au *adhwama,* utukufu. Pia tunapata msamiati wa Kiamu; *ndu,* ndugu; *jinale,* jina lake; *sayo,* hayo; *taka,* nataka; *mwane Saidi,* mtoto wa Saidi na *zimteleleye,* zimminikie.

Watunzi hao wawili wana maudhui tofauti, lakini swali ni kwamba, tungo zao hizo zina uhusiano gani? Imani na mikabala yao haiwezi kunasibishwa! Jibu ni kwamba tungo zote zinashangilia Kiswahili kama lugha ya ushairi kwa viwango na maudhui tofauti. Tungo hizo zimetungwa karibu wakati mmoja, na pengine kwenye mazingira mamoja.

Zinazingatia maslahi ya jamii ile ile moja. Vile vile baadhi ya mizani ya tungo zao zina idadi sawa. Kwa mfano:

Kijakazi Sada nakutuma hujatumika
Nenda kamwambia yangu mama kayalimuka
Afanye mkati mle ndani tupe kaweka
Karekeze pingu miguuni ikaniuka.

Knappert (1979:91)

Huo ni utungo wa Fumo Liyongo ambao pengine ulitungwa nusu karne mbele ya *Hamziyyah* ingawa lugha katika *Hamziyyah* ina ukale zaidi. Matumizi ya msamiati wa kale hutuangazia na kuakisi kipindi fulani kilichopita. Kwa muda mrefu lahaja ya Kiamu ndiyo iliyotumika kama lugha ya *ushairi mzuri*. Hii ni kwa sababu katika historia ya ushairi, malenga wa mwanzo mwanzo kama Fumo Liyongo na Aidarusi Uthman wanatumia lahaja hiyo kwa sababu Lamu ndicho kilikuwa kituo cha usomi.

Kijumwa (1913:24,41) naye anasema:

11. Wagala wakabaini
*Huyu Liongo ni nyani*
*Kwetu hayasilikani*
*Wala hatuyasikia.*

120. Wakamuona ndiyani
Wakampeka asikhini
Hata kwenyi Sulutwani
Mwane Liyongo akaja.

Katika ubeti wa 11, tunapata maneno ya lahaja ya Kiamu kama; *nyani*; nani, *hayasilikani*; hasikiki, *hatuyasikia*; hatujasikia. Katika ubeti wa 120 tunapata maneno ya lahaja ya Kiamu kama; *ndiyani*; njiani, *wakampeka*; wakampeleka, *askhini*; asikatae, *akaya*; akaja. Maneno mengine ya lahaja ya Kiamu katika utendi huu yanapatikana katika ubeti wa 12;

kwa mfano; *huwegema*; kuwakabili, 16. *wakipulika*; wakisikia, 18. *kampeka*; akampeleka, 27. *muini*; mjini, 30. *asimuhuli*; asichelewe, 31. *wakazengeya*; wakatafuta, 46. *katukuwa*; kachukua, 48. *wachenda*; wakaenda, 50. *kayepuwa*; akajiepusha, 54. *mwendani*; rafiki, 72. *kiteweo*; kitoweo, 93. *anipoke*; anipokonye n.k. Kwa hivyo utenzi wote umeandikwa kwa lugha ya Kiamu.

Pia tunapata maneno ya dini ya Kiislamu katika *Kasida ya Hamziyyah* iliyotafsiriwa kutoka lugha ya Kiarabu hadi lugha ya Kiswahili. Kasida hii ndio utunzi wa kale zaidi katika utamaduni wa dini ya Kiislamu. Uliandikwa kwa lugha ya Kiarabu na Al-Busiri na kutafsiriwa na Aidarusi katika mwaka 1652. Tafsiri hii pia ina maneno ya dini ya Kiislamu. Kwa mfano:

Mish-Katil mashabih
Sirat ibl Hisham
Muhadharatil Tarikh al – umamil Islammiyyah

Kwa hivyo kulingana na nukuu hili lugha ya Kiarabu inatumika katika *Kasida ya Hamziyyah*. Vile vile tunapata nukuu hili:

1. Hali wakwelaye kukwelako mitume yonte
Uwingu usiwo kulotewa ni moya sama?

Neno *yonte* yaani yote ni neno lenye asili ya Kingozi. *Usiwo kulotewa* yaani usio kuchelewa ni maneno yenye asili ya Kingozi. Neno *moya* ni lahaja ya Kiamu yaani moja; na *sama* ni uwingu katika lugha ya Kiarabu. Kwa hivyo katika ubeti huu tunapata mseto wa lugha.

Katika ubeti ufuatao tunaambiwa:

58. Wachu nyweshezeo na kufuru mitima yao
Ndwele yao ya dhala ikosheze tabibu kwima.

Neno *wachu* ni Kitukuu yaani watu; *nyweshezeo kufuru* yaani wamejaa ukafiri. Neno *kufuru* lina asili ya neno la Kiarabu. *Ndwele* ni maradhi; *dhala* ni kupotoka. Lina asili ya neno la Kiarabu. *Kwima* ni kusimama. *Mitima* ni nyoyo. *Twabibu* ni mganga au tabibu. Kwa hivyo nukuu hizi mbili kutoka kwa *Kasida ya Hamziyyah* zinatuonyesha jinsi lugha mbalimbali zinavyotumiwa katika ushairi wa Kiswahili.

Kwa hivyo tunapata mchanganyiko wa lugha na lahaja mbalimbali kwenye tungo hizo mbili za wasanii hao, yaani Fumo Liyongo na Aidarusi. Fumo Liyongo alitumia msamiati wa Kireno, Kingozi, Kimijikenda, Kipokomo, Kiswahili n.k. Aidarusi alitumia lahaja mbalimbali kama Kiamu, Kitikuu na msamiati wenye asili ya Kiarabu.

Wakati huo, tungo nyingi za Pate na kwengineko ziliandikwa. Tunapata tenzi za *Kumsifu Yanga, Hamziyyah, Siri li – Asirali, Mwana Lemba, Tambuka,* n.k. Kutokana na utunzi huo, Seyyid Abdallah bin Ali alizuka na *Al-Inskishafi* kueleza maporomoko ya Pate. Msamiati wa utenzi huo wa *Al-Inkishafi* haukuwa na maneno mengi ya kigeni. Kwa mfano:

33. Watoto wangapi uwaweneo
Ukawa yakini kupona
Sasa nyumba zati ziwateteo
Katika luhudi iwafundiye

34. Uwene wangapi watu wakwasi
Walo wakiwaa kama sham'si
Wa muluku zana za adharusi
Dhahabu na fedha wakhiniziye

35. Malimwengu yote yawatiile
Na dunia yao iwalokele
Wachenenda zitwa zao zilele
Mato mafumbuzi wayafumbiye

36. Wakimia mbinu na zao shingo
Na nyuma na mbele ili miyongo
Wakaapo pote ili zitengo
Askari jama watandiye.

Hapo tunaona kuwa lugha ya ushairi ya mtunzi huyo haina msamiati mwingi wa kigeni kwa sababu kisa hicho kinatokana na mazingara ya hapa hapa Afrika ya Mashariki. Tungo nyengine zinaeleza mambo ya Arabuni na mazingira ya huko. Katika *Al-Inkishafi* msamiati ni wa huko Pate. Tunapata maneno kama *uwaweneo,* uliowashuhudia; *ukawayakini,* ukawahakikishia; *nyumba zati,* makaburi; *ziwateteo,* zimewakabili; *luhudi,* kaburi lililo na mwanandani; *iwafundie,* imewafunika; *uwene,* umeona; *wakwasi,* matajiri; *walo wakiwaa,* waliokuwa waking'ara; *wakhiniziye,* walizungukwa na mali; *yawatiile;* yaliwatii, *iliwaokele,* iliwanyokea; *zitwa,* vichwa; *zilele,* vimelalia nyuma kwa kiburi; *wakimia mbinu,* wakitupa mikono kwa mikogo; *miyongo,* makundi, *zitengo,* sehemu iliyotengwa; *jama,* askari wengi; *wawatandie,* wamewazunguka; *mbake,* zinazowaka; *zikinawiri,* ziking'ara n.k.

Hapo tunapata maneno haba yenye asili ya Kiarabu. Kwenye beti hizo kuna neno *muluku,* milki, *sham'si,* jua na *adharusi,* vita yenye usuli wa msamiati wa Kiarabu lakini maneno mengi ni ya lahaja ya Kiamu.

Hapa tena Sayyid Abdallah katika *Al-Inkishafi* anazidi kutuangazia matumizi zaidi ya msamiati wa Kiislamu: Anasema;

1. Bismillahi naikadimu
hali ya kutunga hino nudhumu
Na ar- Rahmani kiirasimu
basi ar-Rahimi nyuma ikaye.

Wakati anapomwomba Mungu atimize uwezo wake, Abdallah anamwomba pia aichochee ilhamu yake ya kutunga. *Bismillahi naikadimu*; jina la Mungu natanguliza; *hali ya kutunga hino nudhumu.* Neno hili nudhumu ni neno lenye asili ya Kiarabu. Pia anataja kwa Kiarabu majina ya Mungu; *ar-Rahmani* na *ar- Rahimi*.

Kwa hivyo hapa tumetaja kwa kifupi lugha ya ushairi tangu kuzuka kwa Liyongo, Aidarusi hadi Sayyid Abdallah.

Sayyid Abdallah bin Ali ni mkazi wa Pate, na hapo anatueleza mambo aliyoshuhudia kabla ya uvamizi huo. Baada ya uvamizi, anatuambia:

49. Nyumba zao mbake ziwele tame
Makinda ya popo iyu wengeme
Husikii hisi wala ukeme
Zitanda matandu walitandiye

50. Madaka ya nyumba ya zisahani
Sasa walaliye wana wa nyuni
Bumu hukoroma kati nyumbani
Zisiji na koti waikaliye.

51. Wana wa zipungu wapende zango
Na wana wa ndiwa humia shingo
Na kupija mbawa matongotongo
Siku za zitati waliwashiye

53. Ziwanda za nyumba ziwele mwitu
Ungi wa matuka na kutukutu
Milango ya ndia yatisha mtu
Kwa kete za kiza kilifundiye

Kwenye beti hizo tunapata maneno kama *mbake,* zinazowaka ; *ziwele* zimekuwa; *tame,* magofu; *wengeme,* wamening'inia; *ukeme,* kelele; *matandu,* buibui; *walitandiye,* wamelizungushia utandu wa buibui; *zipungu* aina ya mwewe wakubwa; *wapende* wamepanda; *zango,* vyango vya kutundika nguo; *ndiwa,* njiwa; *humia shingo,* kuchezesha shingo; *kupija,* kupiga; *matongotongo,* kwa mfulutizo; *zitati,* ndege; *waliwashiye,* wamelowea; *ziwanda,* viwanja; *ziwele,* zimekuwa; *ungi,* wingi; *matuka,* vichaka; *kutukutu,* magugu; *ndia,* njia; *kete,* kimya; *kilifundiye,* kimelifunika, n.k.

Lugha hiyo inatuangazia kwamba wakati huo wa kutunga utungo huo hakukuwa na wageni wengi kule Pate.

Hata wale waandamizi wa ushairi wa Fumo Liyongo na Aidarusi, Mabwana Mwengo, Abu Bakari na baadaye mwandishi wa *Utenzi wa Fatuma* uliosomwa Lamu mwaka wa 1937, na *Al-Inkishafi* ulioandikwa na Sayyid Abdalla A. Nassir walichanganya lugha nyingi katika utunzi wao. Bwana Mwengo aliishi Pate na akaandika *Utenzi wa Herikali* kwa hati zake mwenyewe. Baadhi ya matumizi ya lugha ya ushairi yanapatikana kwenye ubeti ufuatao:

447. Amiri kajilabisi
kapanda wakwe farasi
mukundufu si mweusi
na zita kuvumilia.

*Kajilabisi* ni neno kutoka Kiarabu, yaani kuvaa. *Kapanda wakwe farasi* badala ya *kapanda farasi wake*. Neno *wakwe* yaani wake ni lahaja ya Kingozi. Anapangua maneno kwenye mshororo huu kukidhi upatanifu wa vina. Pia anasema; *mkundufu si mweusi* yaani farasi huyo ni mwekundu, si mweusi. Neno *mkundufu* lina asili ya lahaja ya Kiamu. Tuangalie lugha katika ubeti ufuatao:

466. Sahaba za muongofu
wakalinganya sufufu
myoyo isina haufu
wayakinike kitaa.

*Sahaba za muongofu*, yaani wafuasi wa Mtume; *wakalinganya sufufu* wakakusanyika wengi, Hii ni lahaja ya Kiamu; *myoyo isina haufu*, myoyo isiyo na hofu; *wayakimile kitaa,* wanahakika watashinda vitani. Maneno haya yote hayapatikani kwenye lugha ya ushairi wa leo. Msamiati wa Bwana Mwengo ni wa Kiamu, na unatabiri nguvu, uwezo, ushindi na fahari ya jeshi la Mtume. Kwa hivyo matumizi ya maneno yake katika ushairi yanatuelekeza katika ufahari wa dini ya Kiislamu.

Naye mtoto wa Bwana Mwengo, Abu Bakari anatumia sana lugha ya baba yake. Katika ubeti ufuatao anasema:

350. Akatongoa Musammi
*Halidi nipulikani*
*twaa banu mahazuni*
*simba-ke wenye manyaa.*

*Simba-ke*; simba wanawake. Hii ni picha ya Kiafrika. Simba mwanamke huwinda na kumpatia simba mume. Abu Bakari anatumia msamiati wenye ufahari au kuonyesha ushindi. *Akatongoa Musammi*; akasema mwenye mamlaka, mwenye uwezo, mwenye ushindi. *Halidi nipulikani*; Halidi nisikizeni, chukua mashujaa wanaume na wanawake wenye kucha kali; *simba-ke wenye manyaa*. Lahaja ya Kiamu inajitokeza sana kwenye msamiati wake. Pia Abu Bakari anatumia tashibihi na chuku. Anasema:

Waliwene kuu tapo
*Likivuma kama pepo*
*Livuyishalo matari.*

Fasili yake ni kwamba waliona jeshi kubwa; *waliwene kuu tapo*; *likivuma kama pepo;* tashibihi; *livuyishalo matari*, yaani ukubwa wa jeshi hilo huangusha mvua; chuku. Kwa hivyo Abu Bakari anatumia msamiati wa Kiamu kubashiri ushindi unaofuata kwa kutumia tashibihi na chuku. Kwa hivyo lugha ya ushairi hutupa dhamira ya mtunzi na matarajio yake pia.

Nao *Utenzi wa Fatuma* uliandikwa katikati ya karne ya kumi na nane. Kwenye ubeti huu Fatuma anasema:

8. Mungu ndiye mwenye quwa
aumbao kiumbuwa
mwenye kuieta mvua
kwa quduraye Jaliya.

Katika ubeti huu mtunzi anatumia msamiati wa lahaja ya Kiamu; *aumbao kiumbuwa;* aumbaye na kubomoa; *kuieta;* kuileta; maneno *kwa quduraye Jaliya;* yametokana na Kiarabu; kwa amri na uwezo wake Maulana.

Pia Fatuma, badala ya kumtaka Mungu ampe mali anamwambia:

306. Hiyo ndangu maharia
Mola atanitendea
naye atanishiria
Kulla yambu humwelea.

Anatumia lahaja ya Kiamu, *hiyo ndangu maharia*; hayo ndiyo mahari yangu; *naye Mola atanishiria*, Mungu atanifanyia, na anaelewa kila kitu. Huu ni msamiati wa lahaja ya Kiamu na wa Kiislamu.

Lugha hii ya kishairi imehifadhi elementi za Kibantu. Kila msamiati unaotoholewa umefuata kanuni za Kibantu. Utohozi huu hauhusu tu msamiati wa Kiarabu, bali hata msamiati wa Kiingereza na lugha nyengine. Bila shaka msomaji anaweza kuelewa maana ya maneno ya Kiingereza yaliyojitokeza katika lugha ya ushairi katika karne ya kumi na tisa. Sheikh Swadi bin Ali wa Lamu anasema:

Haifai, kutoyuwa yangu hali
nili hai, kwako siweki badali
*gudi bai, yanisiki mai dali.*

Knappert (1979:34).

Fasili yake ni kwamba: Inatakikana uelewe hali yangu, kwani bado nili hai. Sina mwingine isipokuwa wewe tu. Kwa heri, mimi ni mgonjwa mpenzi. Anatohoa maneno *gudi bai*; kwaheri, *yaniski;* mimi ni mgonjwa na *mai dali*; mpenzi wangu. Vile vile Sheikh Swadi bin Ali analalamika kuwa siku hizi watu hawanywi ule mvinyo wa kawaida. Anasema:

Wawapi wanywao *biya*
*wiski* na *champeni*
*sipiriti* inangiya
kwa rahisi madukani
*sitimu* ni mara moya
mara hamtambuwani.

Knappert (1979:34).

Anasema kuwa siku hizi kunauzwa *sipiriti* madukani, yaani pombe isiyopimwa kitaalamu. Watu hunywa *biya, wiski, na champeni* na mara kidogo wamelewa. Hawasikizani. Ulevini siku hizi hakuna sitara. Anasema, *sitimu ni mara moya.* Kwa hivyo, licha ya utohozi wa maneno ya Kiingereza, anatumia pia lahaja ya Kiamu. Pia anatumia maneno ya Kiarabu. Kwa mfano:

*Li ziyara jiituka*
*e sababu ghadhabuka*
*liyaumu kuamuka*
*iwe nzuri sabahuka*
*sema kaifa haluka*
*kalubi ni abaduka.*

*Knappert (1979:45)*

*Ziyara* ni neno lenye usuli wa Kiarabu; safari. Kwa hiyo msichana anamwambia; nimekuja kukutembelea, kwa nini umekasirika? *Ghadhabuka*? *leo* kama unaamka, *liyaumu sabahuka;* asubuhi yako iwe nzuri. *Hebu sema, wambaje*? Moyo wangu ni

mtumwa wako; *kalubi* ni *abaduka*; Kwa hivyo mshairi anachanganya msamiati wa Kiarabu na wa Kiswahili.

Ahmad Nassir Juma pia anatumia sitiari ambayo inazua hisia nyingi. Anasema:

> Mkononi, ndiwa meuka ghafula
> Nambiani, msinitumiye hila
> yu angani, au metenga mahala?
> Knappert (1979:42).

Anamfananisha mpenzi wake na *njiwa*. Anasema njiwa huyu ameruka ghafla. Niambieni msinifanyie hila. *Yu angani au metenga mahala*; bado yuko juu juu au amepata mshikaji?

Vile vile mshairi huwa na uhuru wa kurefusha maneno au kudondoa maneno ili akidhi mizani. Katika *Sauti ya Dhiki* Abdulatif Abdalla (1973:6) anasema:

> *Tuza moyo*
> Akhi tuliza mtima, uwate kusononeka
> Hakuna lisilokoma, siku '*kifika 'tatoka*
> Kusubiri ni lazima, na kumuomba Rabuka
> Wasiya wako *'meshika.*

Amefupisha maneno kama '*tatoka;* utatoka, '*kifika;* ikifika, *'meshika*; nimeshika. Kama angeandika maneno hayo kwa mjazo hangekuwa na upatanifu wa mizani. Kwa hivyo mifano hiyo inatuonyesha kuwa mtunzi huwa na uwezo wa kudondoa herufi au silabi bila kupoteza maana na kukidhi upatanifu wa mizani.

Vile vile mtunzi anaweza kurefusha maneno au kugeuza mpangilio wa maneno. Katika K*asida ya Hamziyyah* tunapata maneno kama *amulowele*; amuoe, *mashaahidi;* mashahid*i*, n.k. Huku ni kurefusha maneno. Katika kubadilisha maneno tunapata *Adama;* Adamu, *suma;* sumu, *dama;* damu, n.k. Kwa mfano:

5. Dhalil ulumi zalawazo kwa alalimu
Al-ghaibu ndako na masimu ya *Adama*

41. Pakuhiwa kwake moyo wake kachi kifua
Kuliviwa nayama kuyoshani nyelusi *dama*

115. Kanuka Yahudi litizile mbuzi kitana
Kwa ngapi shakiya tashilepo kumpa *sama?*

Kwa hivyo lugha ya ushairi ni zingativu na maelezo yake ni ya mkato.

Matumizi ya lugha katika ushairi hutofautiana na matumizi ya lugha ya tanzu nyengine kwa sababu msanii katika ushairi hufanya uteuzi maalumu wa msamiati wake au maneno ambayo huyaunda na kuyaendeleza kwa njia tofauti ili kukidhi dhamira yake. Msanii hutumia maneno yaliyo na sifa fulani ambayo huyatumia kwa njia isiyo ya kawaida. Wakati mwingine mshairi hurudiarudia mshororo fulani, motifu au mbinu nyengine kama mbinu rejeshi, ishara au jazanda ili kuibua na kusisitiza jambo analodhamiria. Mara nyengine dhana ya mshairi huibuka kwenye anwani ingawa si kila mara tunaposoma anwani ya shairi tunapata dhamira.

Mshairi pia ana uhuru wa kupindua miundo ya kisintaksia ili kuhimiza wazo fulani. Miundo hii hujitokeza katika *pindu*. Kwa mfano katika *Diwani ya Akilimali* mtunzi anasema:

1. Ua langu la moyoni, ua nituze nipowe
Ua langu sinihini, na nipoze nituwe
Ua nikae shingoni, ua usiniambuwe
Ua la moyoni ua, *ua lichanuwe kwangu*

2. *Ua lichanuwe kwangu,* kama koja lichanuwe
Ua sinitoke kwangu, ukawa na mwinginewe
Ua ewe uwe wangu, milele mimi na wewe
Ua la moyoni ua, ua lichanuwe kwangu
Akilimali (1973: 63).

Hapo, kipande cha pili cha mshororo wa kibwagizo kinaanza mshororo wa kwanza wa ubeti wa pili. Aina hii ya utungo inahusishwa na utanzu wa nyimbo pia, lakini kama tunavyoona unaweza kupatikana kwenye tungo za kishairi.

Katika diwani ya *Karibu Ndani* mtunzi anatwambia:

DHAMIRI YANGU.
Dhamira imenifunga shingoni
Nami kama mbuzi nimefungwa
Kwenye mti wa utu. Kamba ni fupi
Na nimekwishachora duara.
Majani niwezayo kufikia yote nimekula
Ninaona majani mengi mbele yangu
Lakini siwezi kuyafikia: *kamba, kamba*

*Kamba* isiyoonekana haikatiki
Nami sasa sitaki ikatike, maana,
Mbuzi wa kamba alipofunguliwa, mashamba
Aliharibu na mbwa aliuma watu.
Ninamshukuru aliyenifunga hapa
Lakini lazima nitamke kwa nguvu
*Hapa nilipo sina uhuru.*
Kezilahabi (1988: 36)

Utungo huo una beti mbili. Katika ubeti wa kwanza, neno *kamba* linajitokeza mara mbili mwisho wa ubeti. Pia neno *kamba* linajitokeza mara moja mwanzo wa ubeti wa pili. Neno *kamba* linatumika kama mkufu wa kuunganisha mawazo ya ubeti wa kwanza na yale ya ubeti wa pili. Huu ni ukufu wa aina fulani ambao husaidia mtiririko wa mawazo katika beti hizi mbili. Hili ni shairi la pindu. Kwenye diwani ya *Jicho la Ndani* msimulizi anatwambia:

Watoto wanaopendwa
mimba zao kibashiri
Mama huenda jisafisha…
Na kuchukua hadhari
Vyakula kujipangia
mimba kuiengaenga
na machuchu kusugua
na titi kuzitakasa
zibakie safi daima!
Yabakie na wororo
Yachukue mviringo
Yafufurike *maziwa*

*Maziwa* ya mama
Huwangoja
Na kisha ya mkebe,
Akiba hununuliwa
Darizeni kwa darizeni
Au pengine muuza maziwa
Ya ng'ombe ataagiziwa!
Alete chupa mzo mzo
Ikiwa mama kifuani
Maziwa yatamkaukia!

Mohamed (2002:57)

Neno *maziwa* linajitokeza mwisho wa ubeti wa kwanza na mwanzo wa ubeti wa pili. Neno hili linasaidia mtiririko wa mawazo kutoka ubeti wa kwanza hadi ubeti wa pili. Hili ni shairi la pindu.

Miundo hii inaweza kusababishwa na lengo la kupata upatanifu wa vina na mizani au sababu ya kibalagha. Mageuzo haya humlazimu msomaji azingatie msisitizo anaodhamiria msanii kama uko mwanzoni au baadaye. Anapofanya hivyo msanii huwa anakuza wazo analodhamiria.

Baadhi ya washairi hutumia msamiati unaozungumzia nyumba ilhali wanaelezea jambo tofauti. Kwa mfano, Kithaaka wa Mberia (1997:25) anasema:

SI MASKANI MAPYA!
Haya si maskani mapya
Maskani mapya gani, ambamo
Tunanyonywa damu dawamu
Na kunguni vitandani
Na chawa nyweleni
Na mbungo njiani?

Msanii anaongea juu ya hali ya umaskini wa jamii. Hiyo ni sitiari. Jamii wamepata uhuru, lakini hali yao inazidi kuwa mbaya. Umaskini unazidi kuwalemea. Ndipo akasema, *Haya si maskani mapya,* yaani jamii hawajaanza kufurahia matunda ya uhuru. Kuna unyonyaji unaoendelea. Anaongea juu ya mazingira dhaifu ya jamii.

Pia Shaaban Robert (1947:1) anasema:

PANYA
Panya alitoka, uwanjani kujigamba
Kuwa ana mamlaka, na nguvu kama simba
Simba alicheka, akasema *Ewe Pumba*
*Hulingani na paka wataradhia usimba!*

Hapo simba anaiambia jamii kuwa mnyonge siku zote hubaki mnyonge. Kulingana na fasihi simulizi, simba ni mfalme wa wanyama kwa sababu ya hekima, nguvu na ujasiri wake. Kwa hivyo sitiari hiyo inatukumbusha tuheshimu viongozi wetu.

Mwisho, Abdilatif Abdallah (1973:27) anasema:

MWEREVU HAJINYOWI
Mwenye nacho wajishasha, wajiona kama ndovu
Kitu kimekulewesha, huutambui uovu
Ngoma yako itakesha, au ni nguvu za povu?
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Hapo mtunzi anatumia tashibihi, *kama ndovu,* na sitiari *nguvu za povu.*_Ndovu ni mnyama mwenye nguvu. Kwa hivyo msimulizi anamwonya mhusika wake asijifananishe na ndovu kwa nguvu alizonazo maana hizo zake ni *nguvu za povu.* Povu, hata kama ni kubwa kama ndovu huyeyuka linapopulizwa. Anatuambia kuwa mtu akipata kitu, ale polepole. Ayafahamu mazingara yake. Asijishashe maana huenda kitu hicho kikaisha. Iwapo hataheshimu wenzake wakati anapokuwa na pato, likiisha, hatapata msaada wowote kwa sababu hakusaidia yeyote wakati huo na pato. Hiyo ndiyo maana mtunzi akasema *mwerevu hajinyowi.* Anakanya jamii wawe na tahadhari wakati wa ufanisi wao.

Pia huongea juu ya mazingira, ndege, wanyama na safari ambayo inaoana na dhamira ya ushairi huo. Hapa mtunzi huzingatia maelezo yake kupitia kwa sitiari kuangazia wazo alilonalo.

Katika lugha ya ushairi, mbinu hizi ni pamoja na takriri, ritifaa, tashibihi, sitiari, chuku, uhuishi, taswira, taashira, semi, balagha, kejeli, tabaini, n.k ambazo tutazifafanua zaidi katika sura ya tatu.

## 2.8 HITIMISHO

Katika sehemu hii tumeshughulikia dhana ya fasihi simulizi, maana ya ushairi, chimbuko la ushairi, maendeleo ya ushairi, athari za wageni, mashairi huru na lugha ya ushairi. Tutafafanua vipengele hivi zaidi katika sura ya tatu kama vinavyojitokeza katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali.*

# SURA YA TATU

## 3.0 UTANGULIZI

Ndani ya sura hii tunachanganua fani katika Utenzi wa Swifa ya Nguvumali. Kabla ya uchanganuzi huo tunaeleza kwa muhtasari yaliyomo. Utenzi huu unasimulia juu ya kundi la wachawi ambao wanamwua Salima kwa kumtoa sadaka ili kijiji chao kiepukane na madhara fulani. Kisa hiki kinatokea kwenye kijiji cha Mteniyapa katika sehemu iitwayo Panenenene katika upwa wa Afrika Mashariki. Kifo cha Salima kinakanganya wanakijiji mpaka wanamwalika mganga Nguvumali aje awategulie kitendawili hicho. Mganga huyo anathibitisha kuwa Salima ameuawa kwa uchawi. Anawatambua wachawi hao na kuwakabidhi serikali ambayo inawafunga jela kwa muda fulani. Kisa hiki kinatokea wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani, jambo ambalo linapingana na maadili ya dini ya Kiislamu.

Katika tasnifu hii tunafanya uchanganuzi wa fani ambayo mshairi anaitumia kuwasilisha ujumbe wake. Wazo kuu hapa ni mgogoro unaojitokeza baina ya wachawi na Nguvumali ambaye anawatambulisha. Migogoro mingine ni dhana ya waovu inayowakilishwa na wachawi na dhana ya wema inayowakilishwa na Nguvumali, serikali na wanakijiji.

Mtunzi ametumia vipengele vya fani kama mtindo, muundo, toni, msuko, wahusika, mandhari, wakati na tamathali za usemi. Nia yetu ni kuvichunguza vipengele hivyo kwa uangalifu ili tujue kama amefaulu kuibua dhamira anayokusudia.

### 3.1.0 MTINDO

Dhana ya mtindo inaweza kufafanuliwa kwa namna mbili. Mtunzi hutumia mtindo ili ajenge kazi yake ya kifasihi ambayo sura ya kazi hiyo hutofautiana na sura ya kazi iliyoandikwa na mtunzi mwingine. Wakati mwingine pia mtunzi hupendelea kuangalia na kuelezea aina fulani ya maudhui. Pengine anapendelea kuandika mambo ya kisiasa,

utamaduni wa jamii fulani, maelezo ya kisayansi n.k. Msomaji anapoona kazi hiyo anaweza kuitambua kuwa aliyeiandika ni mtunzi fulani. Kwa hivyo mtindo ni upangaji maalumu wa fani na maudhui ambao una upekee. Hata kama watunzi tofauti wanaandika juu ya mada inayofanana mitindo yao huwa tofauti na hili jambo ndilo linalomtambulisha mtunzi mmoja na mwingine. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa mtindo ni mtu binafsi. Mtindo pia ni namna ya kutumia lugha ili msomaji aweze kupata ujumbe kupitia kwa matumizi ya fani na vipengele vyake. Mtunzi anapoanza kuandika kitu, kinachomjia akilini kwanza ni mada kisha anafikiria nyenzo za lugha na uchaguzi wa maneno. Hapa matumizi ya dhana ya fani na vipengele vyake hujitokeza. Tunaweza kusema kuwa mtindo ni dhana ya ufundi ambayo hujitokeza kutokana na wazo kuu. Hii ni dhana inayoshughulikia kimsingi ufafanuzi wa lugha, muundo, wahusika, mandhari, wakati na msuko. Mtunzi katika utenzi huu ametumia lahaja, Kiswahili sanifu, Kiarabu na Kiingereza.

### 3.1.1 LAHAJA

Dhana hii inabainishwa kama kitarafa cha lugha ambacho hujitokeza kijamii au kimaeneo. Hii ni dhana ambayo huchipuka kutokana na jamii moja kwa sababu ya athari za kimazingira kama vile kugawanywa na mito, misitu, majangwa, bahari n.k. Jamii hii ikitengana haiwezi kuwasiliana kwa urahisi. Kwa hivyo, utengano huo hukuza upekee katika usemaji wao. Utabaka pia huzua lahaja mpaka mawasiliano baina ya tabaka moja na lingine yakatatizika. Mabadiliko haya huweza yakawa katika kiwango cha sauti, maumbo ya maneno, mpangilio, maana, msamiati n.k. Tofauti hizi hazionekani katika maongezi tu bali katika maandishi pia. Lahaja ni mfumo ambao unaweza kujisimamia katika mawasiliano ya jamii fulani.

Mtunzi ametumia maneno ya kilahaja yanayotumika sehemu ya Kilwa. Matumizi ya lahaja hii huangazia dhamira ya mtunzi mara kadha wa kadha. Msamiati anaoutumia una sifa za kusisitiza wazo fulani kulingana na hali ya wachawi hao. Kwa mfano:

14. Nne Binti Ramadhani
Asiye siri moyoni
*Hatta (h)umo makundini*
Shakka wakimfanyia.

20. Yatakimbia majeshi
(H)upati tena bireshi
Ila kwa kitu ni keshi
Mfano wa kununua

Anapotumia hii 'h' katika mabano kwenye neno ni kuwa tu anataka kutuonyesha kuwa katika Kiswahili sanifu linatamkwa hivyo. Kwa mfano neno *(h)umo* (14) linasisitiza utengano au usaliti wa Binti Ramadhani unaotarajiwa; na neno *(H)upati* (20), Binti Jizi anamsisitizia Binti Hanifu kuwa siyo nia ya kundi hili kuendelea kumpa tena hifadhi iwapo hatamtoa dada yake mhanga. Wazo hili linathibitishwa na mkubwa wao Shambi anaposema: *(H)apo atoe nduguye, Ao yeye afidie* linamletea Binti Hanifu mtanzuko wa kihisia hasa kama linatoka kwa Shambi, mkubwa wao. Mifano mingine inajitokeza kwenye beti za 53, 63, 64, 76, 90, 101, 113, 121, 148, 180, 194 na 213.

Matokeo mengine ya lahaja hujitokeza katika matumizi ya [r] na [l]; sababu ni kwamba kulingana na lahaja ya Kilwa tofauti ya vitamkwa hivi si kubwa kisauti. Matumizi ya herufi hizi huingiliana au hupishana. Kwa mfano, pale panapostahili [r] hutiwa [l] na pia pale panapostahili [l] hutiwa [r]. Kwa mfano, maneno kama: 7. *Kijeri*, 22. *Kakalili* na *Ukweri*, 65. *Uzuli* na *Nguvumari*. Katika lugha sanifu yangekuwa *Kijeli, Kakariri, Ukweli, Uzuri* na *Nguvumali*. Anatumia *silikali* badala ya *serikali* (303,350), na *Nguvumali* (308) inajitokeza kama *Nguvumari*. Anachukulia kuwa matumizi ya [r] na [l] ni mamoja au hayana athari kubwa. Lahaja pia inajitokeza pale msanii anapodondoa herufi [y] katika maneno kama; n*divyo*, u*livyoniambia*, n*inavyokupima*, a*livyodhani* na *tunavyofikiri* na kujitokeza kama; *ndivo* (76*), ulivoniambia* (65), *ninavokupima* (154), *alivodhani* (231) na *tunavofikiri* (238).

Vile vile kuna matumizi ya lahaja ya Kiamu ambapo sauti [y] inatumiwa badala ya [j]. Maneno kama *wanajua* na *pamoja* yanajitokeza kama *wanayua* (39, 68) na *pamoya* (154, 214, 246). Pia neno *machungu* linakuwa *matungu* (50, 81, 103).

### 3.1.2 MSAMIATI WA KIARABU

Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* mtunzi ameathiriwa na msamiati wa dini ya Kiislamu. Tukiangalia majina ya Mwenyezi Mungu kama *Mola* (1), *Rabbana* (2, 180, 205), *Rabbi* (3, 176), *Ilahi* (77), *Jalia* (180) na *Rabbuka* (93) yote ni majina ya kidini. Majina yote haya yanasawiri sifa za Mwenyezi Mungu.

Pia mtunzi anasema (66):

> 5. Zilitokea *khabari*
> Sasa nakupa ajiri
> Awali ya Nguvumali
> Hapa Siwa kuingia.

Neno *khabari* lina asili ya msamiati wa Kiarabu. Maneno mengine yenye asili ya Kiarabu hupatikana kwenye ubeti wa 6. *Nawaitu* na *Kukhadithi*, 13. *khofu*, 17. *khatima*, 22. *kakalili* na *mkabili*, 24. *msabiki*, 25. *amani*, 30. *kalatwili*, 42. *akaqimu*, 45. *hadhimu*, 102. *alihuruhi*, 109. *kuradidi*, n.k.

### 3.1.3 MSAMIATI WA KIINGEREZA

Pia mtunzi anatumia maneno ambayo yametoholewa kutokana na lugha ya Kiingereza. Neno *baiskeli* limetoholewa kutokana na neno *bicycle* la Kiingereza. Pia neno *motukari* lina asili ya neno *motorcar* la Kiingereza. Tunapata msamiati wa aina hii katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* ambao Hasani bin Ismail anautumia kwa sababu fulani. Mtunzi analenga hadhira ya kisasa kwa kutumia maneno yanayotoholewa kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili. Baadhi ya maneno haya ni kama: *Keshi* (20),

*Chemba* (41), *saini* (204), *Lipoti* (260), *jajiment* (277) n.k. Msamiati huu wa Kiingereza unaashiria hadhira ambayo imeelimika na kwamba unateka nyara hisia zao. Kwa mfano:

312. Zilijaa *baiskeli*
Hazikuja *motukari*
Sababu shamba akhiri
Kama unavotambua.

Mbinu hii husababishwa na mtunzi ili apate upatanifu wa vina, mizani na wizani.

3.2.0 IDHINI YA MSHAIRI

Katika matumizi ya lugha ya ushairi mtunzi ana uhuru mkubwa sana katika uteuzi wa msamiati, umbuji wake, na matumizi ya maneno katika njia ambayo si ya kawaida. Mtunzi huweza kutumia maneno kwa kupindua miundo ya sentensi. Anapofanya hivyo huwa ana nia ya kupata upatanifu wa vina na mizani au kinachopewa umuhimu na ambacho msomaji lazima akizingatie. Idhini hii humwezesha mshairi akageuza miundo ya lugha ya kawaida katika viwango vya tahajia, miundo ya maneno, vipande vya sentensi au hata sentensi yenyewe. Pia anaweza kutumia maneno ambayo si ya kawaida. Tunachosema ni kwamba mshairi anaweza kudondosha, kurefusha au kubadilisha herufi fulani. Vile vile mtunzi anaweza kutumia maneno kwa maana zinazotofautiana na zile zinazotarajiwa. Maana hizi hujitokeza kwenye muktadha au hata nje ya muktadha. Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* mbinu hizi zinatumika sana. Katika kutumia mbinu hizi mtunzi husisitiza hali zilizoko katika jamii husika. Mbinu hizi ni pamoja na mazida au kurefusha maneno, inkisari yaani kufupisha maneno na tabdila ambayo hujitokeza wakati ambapo mtunzi hubadilisha tahajia. Kwa mfano badala ya kusema: *Tutaingia zaani* anasema: 63. *Zaani tutaingia*. Katika kugeuza muundo wa kawaida mtunzi anasisitiza *zaani* ili kuonyesha hatima yao iwapo hawakutimiza matarajio ya mkubwa wao Shambi. Pia mtunzi anatusawiria ukatili wa Shambi kwa kutumia mbinu hiyo. Anaposisitiza umuhimu wa zinguo mtunzi anasema:

58. Asubuhi na mapema

Bwana Shambi bin Dima

Anakuja himahima

*Kembani anatokea.*

Badala ya *anatokea kembani* anasema *kembani anatokea* yaani anasisitiza neno *kembani* ili umuhimu wa harakati hizo unawiri. *Kemba* ni mahali ambapo uchawi hufanywa. Pia anaposisitiza uhusiano wa karibu wa Binti Hanifu na Salima mtunzi anasema:

79. Kumwona dada yake

Mzawa na baba yake

Jumla na mama yake

*Pamoja wamezaliwa.*

Mbinu hii inampa matumaini Salima kuwa iwapo wale wachawi watatu wengine wana nia ya kumfanyia ubaya, dada yake hangeweza maana wamezaliwa baba kwa mama. Hapo anasisitiza wazo hilo kwa kubadilisha muundo kutoka *wamezaliwa pamoja* na kuwa *pamoja wamezaliwa.* Msisitizo uko kwenye neno *pamoja* ili kuonyesha uhusiano wao. Pia kule kembani matumaini ya Salima yanageuka na kukatishwa tamaa. Anashangazwa na ile haraka ya dada yake. Mtunzi anasema:

82. Bwana Shambi atamke

Basi apo mweke

Alimwona dada yake

*Upesi kumnyanyua.*

Mshangao wa Salima unadhihirika maana mtunzi anatwambia; Alimwona dada yake, *Upesi kumnyanyua* badala ya *kumnyanyua upesi.* Dhana ya *upesi* ndiyo inayotiliwa msisitizo. Dada yake anamweka mahali maalumu na hapo wanampaka madawa harakaharaka ili wamzonge. Mtunzi anatuangazia ukatili wa Binti Hanifu na hamasa zake. Kwa hivyo, tunachosema ni kwamba tunapogeuza muundo wa sentensi wa kawaida

huwa tunasisitiza kile kilichopewa umuhimu. Wachawi hawa wanachelewa katika harakati zao za kuzingua mji ndipo sasa mtunzi anatumia muundo wa *zaani tutaingia* ili kutuonyesha haraka yao katika kutimiza wajibu wao; *pamoja wamezaliwa* ili kututhibitishia unasaba wa Salima na Binti Hanifu kuwa ingawa anamtoa mhanga, yeye ni dada yake; na *upesi kumnyanyua* ili atusawirie ukatili wa Binti Hanifu kuwa anahamasika kutimiza yale anayoahidi wachawi wenzake kwa haraka hata ingawa Salima ni dada yake wa baba kwa mama.

### 3.2.1 MAZIDA

Katika mbinu hii msanii huwa na tabia ya kurefusha maneno au kuzidisha silabi kwa mujibu wa kupata upatanifu wa mizani. Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* kama angetumia muundo wa kawaida hangepata upatanifu wa vina na mizani. Kwa mfano:

38. Binti Jizi nenda mbio
Kawaambie wenzio
Ni maneno kama hayo
Na *menginewe* sikia.

Mtunzi anatumia neno, *menginewe* badala ya *mengine*. Kwa kutumia neno *menginewe* mtunzi amekidhi mbinu ya mizani. Mbinu hii inajitokeza tena kama ifuatavyo; ubeti wa 17. *tunadharawiya* badala ya *tunadharau*, 185. *ninahitajia* badala ya *ninahitaji*, 278. *kucheleweya* badala ya *kuchelewa*, 372. *kukubalia* badala ya *kukubali* n.k. Maneno haya anayoyarefusha mtunzi mara nyingi yanakidhi mbinu ya mizani. Kama angetumia muundo wa kawaida mtunzi hangepata upatanifu wa mizani. Kwa hivyo yeye hutumia mbinu hii ili apate upatanifu huo. Akifanya hivyo shairi huweza kuimbika na wizani kupatikana. Mbinu hii hutumiwa kwa kurefusha maneno kwa madhumuni ya kupata upatanifu wa mizani.

### 3.2.2 INKISARI

Kama katika mazida ambapo mtunzi hurefusha maneno ili apate upatanifu wa mizani mbinu hii ya inkisari hutumiwa kwa lengo hilo hilo pia. Mtunzi hufupisha maneno kwa kudondoa silabi. Katika ubeti ufuatao mtunzi anasema:

16. Sikizeni *nisemayo*
    Tena mukae kituo
    Tufanye mji zinguo
    Miaka imetimia.

Kwa kawaida neno *nisemayo* huandikwa *ninayosema*. Msanii amedondoa silabi *na*. Hapo anaendeleza maneno kwa jinsi tofauti. Kama tunavyosema idhini hiyo inajitokeza katika viwango mbalimbali vya lugha; kitahajia, kisauti, kimaana, kirejista n.k. Kwa mfano:

28. Munifikie kwa upesi
    Leo ni Jumamosi
    Moyo una wasiwasi
    Na ruhu *ijaturia.*

Anatumia *ijaturia* badala ya *haijaturia*. Kwa kudondosha silabi *ha* ambayo huonyesha ukanushi mtunzi ana dhana ile ile ya ukanushi badala ya kauli yakinishi. Anachowaeleza wenziwe ni kwamba moyo wake una wasiwasi; haujatulia. Maana hii inapatikana kwenye muktadha wa kisa chenyewe. Siku zinaenda na bado hawajaamua la kutenda, na ndipo hapo wanapokutana wakisema:

57. Jumatano imejili
    Tusikawilie mno
    Wanasikiza amri
    Bwana *atayotwambia.*

Badala ya *atakayotwambia* mtunzi anadondoa silabi *ka*. Kama angetumia neno katika ukamilifu wake mtunzi hangepata usawa wa mizani maana kila mshororo una mizani nane. Mbinu hii pia inatumika kwenye ubeti wa (16) *Nisemayo* badala ya *ninayosema,* (37) *wa* badala ya *wana*, (40) *nduguye* badala ya *ndugu yake*, (42) *kazichukua* badala ya *akazichukua*, (114) *mkwewe* badala ya *mkwe wake*, (250) *kenda* badala ya *akaenda*, (333) *alivo* badala ya *alivyokuwa* (336) *wachama* badala ya *wanachama* n.k. Kwa hivyo mtunzi hapa anatumia mbinu hii ya inkisari kuleta upatanifu wa mizani katika kila mshororo. Hufanya hivyo kwa kudondoa baadhi ya tahajia au silabi.

### 3.2.3 TABDILA

Mbinu hii inatumiwa hasa katika ushairi kuirejelea tabia ya kugeuza tahajia katika maneno fulani. Dhana hii inajitokeza pale ambapo mshairi anataka kupata upatanifu wa mizani. Hubadilisha sauti pia kwa ajili ya wizani. Kimsingi mbinu hii hutokana na sababu ya kiarudhi. Kwa mfano:

1. Bismillahi naanza
   Jina la Mola wa *enza*
   Muhammadi mpendeza
   Kwa Mola wetu Jalia.

Neno *enza* katika mshororo wa pili lingekuwa *enzi* lakini kwa kutaka kupata upatanisho amebadilisha *zi* kuwa *za* ili kukidhi vina. Pia katika ubeti ufuatao:

2. Nakuomba ya Rabbana
   Unijalie kijana
   Nitungapo *shairina*
   Pasiwe tena hudhia.

Badala ya kutumia neno *shairini* katika mshororo wa tatu anatumia neno *shairina* ili akidhi upatanifu wa vina. Vile vile katika ubeti huu ufuatao:

120. Nikumbukapo kizazi
Wakikalibu mchozi
Ndipo hujiwa *moyonzi*
Na fikira za dunia.

Msanii anatumia neno *moyonzi* badala ya neno *moyoni* ili alete upatanisho wa vina vya *zi*. Katika ubeti ufuatao:

210. Kaona nyoka wawili
Wanamfata *kiviri*
Dalili ya Nguvumali
Ya kuweza kumjia.

Badala ya kutumia neno *kivuli* anatumia neno *kiviri*. Anabadilisha tahajia *u* kwa *i*. Angetumia neno *kivuli* angesawiri lugha sanifu ya Kiswahili. Mifano mingine ni 272. *ufajiri* na *hapapa* badala ya *alfajiri* na *hapakuwa* ili kuwe na upatanifu wa mizani.

## 3.3.0 TAMATHALI ZA USEMI

Kuvuna na wengine (1992), Mbatiah (2001) na Wamitila (2003) wanakubaliana juu ya maelezo ya tamathali za usemi kuwa hutumiwa kufananisha dhana moja na nyengine tofauti. Maana asilia inaweza kugeuzwa na kuleta maana tofauti. Mtunzi hutueleza mambo mengi kwa kutumia maneno machache.

Hizi ni mbinu ambazo hutumika katika kazi za kifasihi kwa nia ya kuongeza maana katika ushairi. Maana hizi huweza kutokea ndani ya matini au hata nje ya matini hiyo. Mbinu hizi pia hutumia lugha katika viwango vya maana au kwenye mpangilio wa maneno ili kuzua maana mpya au kusisitiza. Tunachunguza jinsi mpangilio wa maneno unavyosababisha matokeo ya tamathali za usemi kama vile taswira, tashibihi, sitiari, tashihisi, metonimia, n.k.

### 3.3.1 TASHIBIHI

Mbinu hii hufananisha vitu viwili moja kwa moja. Msomaji huiona picha ya msanii anayosawiri bila ya matatizo mengi. Maneno kama *kama, mithili ya, mfano wa* na *ja* hutumika. Kimsingi, mbinu hii hufafanua wazi maana, dhana,.picha au hali fulani kwa ulinganisho ambao ni lazima uwe na mantiki ya kimuktadha na ni lazima ukubalike katika jamii tumizi.

Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* msanii anatuambia;

> 68. Binti Hanifu mdogo
> Alikwenda *kama gogo*
> Yamemfika marogo
> Bila mwenyewe kujua.

Tunaelewa sifa ya gogo kuwa halina uhai na huweza likafanywa vyovyote bila kujitetea. Kwa sababu ya yale madawa ya wachawi, Salima anapatwa na ubumbuwazi; hana hisia na wala hana fahamu tena. Kwa hivyo ingawa anatembea hajijui. Anajipeleka kule porini kwa wachawi bila makusudio yake. Msanii pia anatusawiria nguvu za madawa ya wachawi hao ambazo zinampumbaza Salima kiwango cha kutojua afanyayo. Vile vile mtunzi anatuambia;

> 96. Binti Hanifu mdogo
> Alibaki zigozigo
> *Kafungwa kama muhogo*
> Sakti ameturia.

Kule kumfananisha Salima na muhogo ni kutuonyesha picha ya kutoweza kujitetea kabisa maana wachawi hao wamemtatia kweli kweli. Salima anatulia kabisa maana anajua hakuwa na la kufanya tena ili ajiokoe. Mtunzi hapa anatusawiria kiwango cha ukatili na maovu yanayojitokeza katika jamii hiyo.

Katika kutuonyesha jinsi Shambi anavyoathiriwa na nguvu za Nguvumali mtunzi anatupa tashibihi nyengine. Kwa mfano:

223. Kaota anasema naye
Na koja kampa yeye
*Mfano kama nduguye*
Na vingi kumtolea.

Nguvumali bado hajafika lakini nguvu zake zinamwathiri Shambi ambaye anaonyeshwa kama mtu anayetaka kujisalimisha pamoja na vifaa vyake vya uchawi. Katika hali ya kawaida ndugu wawili hupendana na kupana zawadi lakini Shambi ni mchawi na anaonyesha kushindwa mbele ya mganga Nguvumali. Tashibihi hii inatuchorea picha ya wema dhidi ya uovu na pia inatusawiria maporomoko ya Binti Hanifu kwa kumtoa dada yake mhanga. Maovu yanayotendwa na wachawi dhidi ya jamii yanafichuliwa na waovu wenyewe. Katika mkondo ule ule wa kutusawiria uovu utakavyoshindwa na wema mtunzi anatuambia:

276. Polisi (h)ao wawili
*Kama ni kumi na mbili*
Walipanda baiskeli
*Wanaluka kama njiwa.*

Picha anayotuchorea mtunzi ni ile nguvu serikali waliyonayo. Polisi *wawili* wana nguvu za polisi *kumi na mbili*. Mtunzi anatuonyesha hamasa na uwajibikaji wa serikali dhidi ya waovu. Pia anatuonyesha haraka waliyonayo katika kufuatiliza mambo dhidi ya waovu anaposema *wanaluka kama njiwa.* Pia mtunzi anaposema:

334. Akautoa ulimi
*Unawaka kama lami*
'Mtu nimeua mimi'
Jamii wakasikia.

Ushahidi anaotoa Shambi kuwa yeye ndiye aliyemwua Salima unatudhihirishia kuwa Nguvumali na serikali wana uwezo wa kuwafanya waovu waungame kwa kutumia asasi tofauti tofauti.

### 3.3.2 TAKRIRI

Dhana hii hujitokeza pale ambapo msanii hurudiarudia kitu fulani kwa sababu ya kuzua hisia kwa msomaji. Inaweza pia kufasiliwa kama umbo linalorudiwa katika kuandikwa ili kupata umbo moja katika kiwango cha mshororo wote kwenye ubeti na hata kibwagizo. Mtunzi anaweza kuitikia kwa takriri bila kufikiria kwa sababu ya hasira, furaha au huzuni. Mbinu hii huleta taathira kwa sababu ya ule mtiririko wa maneno hayo hasa ikitumiwa vizuri hutekeleza jukumu muhimu sana kimaana na kisanaa. Pia takriri hubeba kazi muhimu ya kimaana yaani kazi ya msisitizo. Wakati mwingine mshairi hutumia visawe vya maneno ili kuleta msisitizo ule ule kiujumbe. Kwa hivyo tungependa kutalii ili tujue aina tofautitofauti za takriri na uamilifu wake katika utenzi husika. Kuna aina nyingi za takriri ambazo hujitokeza katika kiwango cha irabu, konsonanti, neno, mistari, muundo wa sentensi, vina, mizani, wizani, mawazo na kibwagizo.

#### 3.3.2.1 TAKRIRI MANENO

Katika Kiswahili mara nyingi tunapata mfuatano wa silabi na maneno. Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* tunapata takriri ya maneno. Kwa mfano:

12. Wa pili ni Binti Jizi  
*Ndiye* mtunga vikozi  
*Ndiye* yeye kiungozi  
Na njia za kuteua.

Umuhimu wa Binti Jizi katika kikundi hiki cha wachawi unasawiriwa na takriri ya neno *ndiye*. Yeye ni *kiongozi* na *ndiye* anayeongoza *kikosi* hicho. Takriri nyengine inajitokeza wakati mtunzi anapoonyesha hisia zake. Anasema:

74. Anapotea porini

Upande wa pwani

*Maskini maskini*

Salima anapotea.

Salima amezongwa na madawa ya wachawi hao na hali ile ya ubumbuwazi sasa imemkolea. Anakwenda kukutana na hatima yake bila kudhamiria. Takriri ya maneno pia inajitokeza katika ubeti wa 78: *kulekule maporini*. Anapoondoka nyumbani nia yake ni kwenda kukata kuni lakini kumbe anafuata hatima yake mahali ambapo wachawi hao wanamsubiri. Pia unasaba wa Binti Hanifu na Salima unasawiriwa na takriri ya neno *yake*. Kwa mfano:

79. Kamwona dada *yake*

Mzawa na baba *yake*

Jumla na mama *yake*

Pamoja wamezaliwa.

Takriri hii, mbali na kutuonyesha ukaribu wa unasaba baina ya dada hao, inatukariria kimawazo kwamba kikawaida hatari hiyo haingemkumba Salima maana wamezaliwa baba na mama na Binti Hanifu. Mtunzi anatuonyesha na kututhibitishia ukatili na dhamira ya wachawi hao. Mtunzi anatupa takriri ya wizani kwenye ubeti huo huo kwa kutumia neno *yake*. Wizani pia unajitokeza wakati Bwana Mwenye anapomkemea Binti Ramadhani. Anasema:

142. Yale anayoyasema

Na bwana yuko wima

*Ewe mama! ewe mama!*

Yako sitayasikia.

Bwana Mwenye anagundua hila ya Binti Ramadhani ambaye hataki Bwana Mwenye aende kupiga ripoti serikalini. Anataka kumchelewesha ili yeye na wachawi wenziwe waende wakamtoe Salima kule porini na kumpeleka kule bandani ili watu waone kuwa ameuawa na banda lililomwangukia. Hiyo ni takriri ya mawazo na ya maneno yanayotoa

msisitizo wa hamasa aliyonayo Bwana Mwenye. Nia yake ya kwenda kupiga ripoti ni kujinusuru yeye na wanakijiji iwapo Salima hangeonekana. Katika ubeti 232 tunapata takriri zifuatazo: *waje tena wale wale* na *ndugu yangu yule yule*. Hapa Binti Hanifu anawaita wote wanaomtafuta Salima waje washuhudie kwamba anayemwona bandani si mwingine bali Salima wanayemtafuta.

### 3.3.2.2 TAKRIRI PINDU

Mbinu hii hujitokeza mahali ambapo mshororo wa mwisho wa ubeti hurudiwa katika mshororo wa kwanza wa ubeti unaofuata ingawa maneno hupinduliwa. Dhana inayojitokeza ni ile ile ya msisitizo. Kwa mfano:

58. Asubuhi na mapema
Bwana Shambi bin Dima
Anakuja hima hima
*Kembani anatokea.*

59. *Anatokea kembani*
Upande huo wa pwani
Walikutana njiani
Aliona kuchelewa.

Hisia za Shambi zinabainika kwenye takriri hii ya pindu. Badala ya kuwangojea wachawi wenzake yeye anarauka peke yake. Mtunzi anatuonyesha hamasa za Bwana Shambi na jinsi anavyoona umuhimu wa zinguo. Hapa mtunzi anatubainishia harara alizonazo mchawi huyu. Katika ubeti wa 273 na 274 tunaona takriri pindu nyengine isemayo: *Dalili ilitokea* na *ilitokea dalili* ambapo mtunzi anatuthibitishia kuwa ule wasia aliotoa mwathiriwa unatimia maana usiku kunanyesha mvua kubwa mpaka wanakijiji hawana mahali pa kujificha. Asubuhi yake polisi wawili wanakuja na dhoruba *kama polisi kumi na mbili*. Wanawapiga wanakijiji mpaka baadhi yao wanazirai. Mambo haya yote yanatabiriwa na mwathiriwa. Vile vile katika beti za 352 na 353 tunasoma: *Vibao*

*vimeenea* na *vimeenea vibao*. Hizi ni hamasa za polisi kuwapiga wanakijiji ili waseme ni nani mwuaji wa Salima. Huu ni ule ule utabiri wa mwathiriwa ambao msanii anatuthibitishia juu ya dhana ya wema dhidi ya uovu.

### 3.3.2.3 TAKRIRI WAZO

Mbinu hii inatuonyesha kuwa serikali haishindwi wakati uovu unapojikita. Uovu wa watu wachache hauwezi kukosa njia ya kumalizwa. Mtunzi anasema:

> 338. Jumla ya wale watu
> *Wachawi sana watatu*
> *Wa nne tena si mtu*
> Amekwisha kujifia.
>
> 339. Anayekabidhi sirikali
> *Wachawi watatu kamili*
> *Wa nne amesafiri*
> Akhera ameingia.

Mbeleni walikuwa wachawi wanne lakini sasa wamebakia watatu. Binti Ramadhani hayupo tena. Anachotuashiria mtunzi ni mtiririko wa mawazo ya Salima kwamba unazidi kuwaathiri wachawi hao. Salima anamkanya dada yake dhidi ya kumfanyia ubaya. Sasa mateso yanawakabili mpaka Binti Ramadhani anafariki. Serikali haishindwi na hao waliobakia.

### 3.3.3 SITIARI

Kulingana na Mbatiah (2001) na Wamitila (2003) wanakubaliana kuwa mbinu hii hufananisha vitu viwili kwa kukipa sifa kitu kimoja na kusema ni kitu kingine. Ulinganisho huu hauko wazi kama ule wa tashibihi. Maana ya sifa ya kitu cha kwanza hufichika kwenye sifa ya kitu cha pili. Wakati mwingine sifa ya kitu hujitokeza kupitia

kwa jina la kitu hicho. Sitiari pia hutumika pale msanii anapotoa hadithi akilenga hali fulani katika jamii.

Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* mbinu hii inajitokeza sana. Wachawi hawa watatu wanakubaliana kuhusu zinguo lakini mmoja wao anaanza kuonyesha dalili ya kujiuzulu, na ndipo mkubwa wao Shambi akasema:

36. Akalia Binti Jizi
Shambi akasema wazi
*Mimi kunifanya ngozi*
Sitaweza kuridhia.

37. *Mimi kunifanya ngoma*
Sitakubali wa chama
Bora mutoe gharama
Na miye nikatumia.

Maana halisi ya ngoma ni ala ya muziki inayotengenezwa kwa kuwamba ngozi kwenye mzinga; mchezo wa kufuata mdundo wa ala hiyo; kufanya jambo lisilo la faida. Maana ya ngozi nayo ni sehemu ya juu inayofunika nyama katika mwili wa kiumbe. Anachosema Shambi ni kwamba wanachama wenzake wasimlazimishe kufanya jambo ambalo halina manufaa. Vile vile ngoma haiwi ngoma mpaka kiumbe kife ndipo ngozi yake itumike kwa kuwamba ngoma. Kwa hivyo, anachosisitiza Shambi ni kwamba iwapo mchezo huu utachezwa, lazima kiumbe kipatikane ili kiuawe ili ngoma iwambwe. Hakuna njia nyengine ya kuwamba ngoma bila ngozi. Katika uhalisia wa uwambaji *ngoma* kila mtu huvutia kwake ili ile *ngozi* iwe ngumu ili ilie vizuri. Hapa msanii anatuashiria kuwa Shambi anapandwa na hamaki kwa sababu ya ugoigoi wa baadhi ya wanachama. Yeye analitilia maanani wazo hili la zinguo ndipo anapowaambia wasimfanye *ngozi* wala *ngoma*. Wachawi hawa wanaanza kuwa na mtafaruku. Msomaji lazima aainishe sifa za *ngozi* na *ngoma* ndipo ahamishe sifa zake kwa Shambi. Pia mtunzi

anatupa hisia za dhiki ambazo wachawi hawa wanapata kupitia kwa hawa polisi wawili. Anasema:

354. Mnyamwezi na Jaluo
Walifurahi siku hiyo
*Wamepata ngozi zao*
Bomani wanarejea.

Sifa hii inajitokeza sababu ya kipigo walichopata wachawi na wanakijiji kutoka kwa polisi hao ambao wamefurahi sana. Pia Binti Jizi anamwambia Binti Hanifu:

20. *Yatakimbia majeshi*
(H)upati tena bireshi
Ila kwa kitu ni keshi
*Mfano wa kununua.*

Hapa majeshi ni hili kundi la wachawi. Ufananisho huu unatusawiria nguvu na mamlaka waliyonayo wachawi hawa. Mtunzi anatumia mbinu hii kutudhihirishia hamasa za wachawi hawa na jinsi wanavyozozana; pili, furaha waliyonayo polisi kwa kupata *ngozi* zao. Pia anapomwambia *Ila kwa kitu ni keshi* ni kwamba hakuna kitu cha bure. Lazima atoe huyo dada yake mhanga kama anavyolipa pesa dukani maana kila mmoja wao ashatoa mtu wake. Mbinu hii hukipa sifa kitu kimoja na kumaanisha kitu kingine. Vitu hivi havina ushabihiano kiumbo kwa hivyo inafaa msomaji azingatie sifa za kitu cha pili ndipo aelewe sifa za kitu cha kwanza. Sitiari nyengine zinajitokeza kwenye ubeti wa 262. *Njooni leo mle ngozi*, 343. *Kipimo cha aibu zake, zinapata kilo mia*, 345. *Uzito wa aibu zake, zitapata hamsumia.*

### 3.3.4 TASHIHISI

Mbinu hii pia inajulikana kama 'uhuishi'. Hutumiwa na wasanii kuvipa uhai vitu ambavyo havina uhai au kuwapa wanyama tabia au sifa za kibinadamu. Tukizingatia

mbinu hii katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* mtunzi anahuisha dhana ambazo hazina uhai. Kwa mfano anasema:

34. Ukitupita wakati
*Hatumpati mauti*
Kwa hivo ni tafauti
Jumatano kupitia.

Hapa mtunzi anahuisha *mauti.* Wachawi hao wanafanya mashauri ya kwamba Jumatano ikipita hawawezi tena kupata maiti ya kufanyia kafara hiyo. Pia katika hamaki zao wanasema;

42. Binti Jizi akaqimu
Azichukua salamu
*Naye moyo una hamu*
Kama unavotambua.

Baada ya kikao chake na Shambi, Biti Jizi anapandwa na jadhba ya kutaka kutimiza shughuli za zinguo. Katika kuonyesha hamasa hizo msanii anatumia mbinu hii ya tashihisi kwa kusema; *naye moyo una hamu* ili atuonyeshe hamasa ya wachawi hawa. Katika kutuonyesha hatima ya wachawi hao msanii anasema:

377. *Jajiment ikahukumu*
Wafungwe wote maalum
Kuwawacha ni haramu
Sharia imeziwia.

Kwa kawaida mtu ndiye anayehukumu lakini hapa msanii anaihuisha hiyo hukumu anaposema: *Jajiment ikahukumu* ili asisitize kuwa uovu hushindwa mbele ya wema. Katika utenzi huu mtunzi anasema:

270. Basi wamelala pale
*Kumngoja mauti yule*
(H)apakuwa na kilele
Wala mtu kusongea.

Katika ubeti huo wa 270 umati wanalala nyumba ya maiti anaposema *Kumngoja mauti yule.*

### 3.3.5 BALAGHA

Mbinu hii hujitokeza pale msemaji anapouliza swali bila ya kutarajia majibu kutoka kwa msikilizaji. Kwa mfano:

103. Tafadhali ndugu yangu
*Mbona wanipa matungu?*
Haswa nipe kosa langu
*Nini nimekosea?*

Salima anateswa lakini hakutarajia dada yake achangie mateso haya. Maswali haya hayapati majibu maana hata Salima anajua kuwa dada yake Binti Hanifu hangemjibu. Msanii anavuta hisia za hadhira ili wamwonee huruma Salima na pia anatuangazia ukatili wa Binti Hanifu anapotangamana na wachawi wenziwe. Uovu huu unafanyika kifamilia. Maswali haya ya ubeti wa 103- *mbona wanipa matungu? Nini nimekukosea?* Haya ni aina ya maswali ya balagha.

Swali la balagha kutoka kwa Shambi linajitokeza kwenye ubeti ufuatao:

127. Akisharudi nyumbani
*Utafanya dawa gani?*
Wote wanamjuani
Waweza kusimuria.

Umoja wa wachawi hawa umeanza kuvurugika. Msomaji anapatwa na taharuki ya kutaka kujua ni tukio gani ambalo linakuja maana mmoja wao anajiuzulu na bila shaka pengo hilo linasababisha wale wengine kuingiwa na woga kuwa wanaweza kusalitiwa na Binti Ramadhani. Pengo hili lina tashwishi kwa wale wachawi wengine isipokuwa Shambi ambaye anaonyesha uthabiti kupitia kwa ubeti wa 127 ambao tumeunukuu hapo juu.

### 3.3.6 TABAINI

Dhana hii huonyesha kukinzana lakini maana ya msingi haibadiliki. Mzungumzaji hutumia kauli chanya kwa kutumia kikanushi *si*. Kuna msisitizo kwenye kauli hii lakini haujitokezi waziwazi. Kwa mfano: kafara ya kumtoa Salima mhanga *si ndogo* tuna maana kafara hiyo ni kubwa. Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* mbinu hii inajitokeza kwa wingi. Kwa mfano:

7. Niyasemayo ni kweli
   Niliona kwa dalili
   *Sio haja* ya kijeri
   Shairi langu pokea.

Mtunzi ameshatamka kwamba *Niyasemayo ni kweli* na anaposema tena *sio haja ya kijeri* anasisitiza ile kauli ya mwanzo ya ukweli. Kikanushi *si* kinatilia mkazo ukweli huu lakini si kwa uwazi vile. Katika kutia msisitizo Binti Ramadhani haoni haja ya kuendelea na harakati ya kumtesa Salima. Anasema:

115. Asemavyo mkwe wangu
     Umenipata uchungu
     Hayo kweli *si urongo*
     Najua yatatokea.

Salima ni mke wa Ramadhani Mponda ambaye ni mtoto wa Binti Ramadhani. Hapa anatumia mbinu hii ya tabaini Hayo kweli *si urongo* ili hadhira ijue kuwa Binti Ramadhani hana msimamo dhidi ya harakati za wachawi wenziwe ya kuzingua kijiji

chao. Vile vile Liwali anaiashiria hadhira kuwa hali ya Binti Ramadhani si nzuri yaani yu taabani. Anasema:

> 302. Tena yuko ospitari
> Hali yake *si nzuri*
> Inaonesha dalili
> Umauti kumjia.

Badala ya kusema hali yake *ni mbaya* Liwali anatumia kinyume *si nzuri*. Kwa hivyo mbinu hii hutumiwa kuonyesha msisitizo usio waziwazi. Mbinu hii hupoza ukali wa hali iliyopo.

### 3.3.7 USAMBAMBA

Mbinu hii huonyesha sehemu mbili zinazokinzana. Tunaweza kuitumia katika kiwango cha sentensi, vipande vya sentensi, mpangilio wa kimuundo au usambamba wa kidhamira. Wakati Binti Jizi anapomwambia Binti Hanifu atoe mtu wake kama sadaka Binti Hanifu anajibu hivi:

> 21. Binti Hanifu katamka
> *Ni kweli hiyo hakika*
> *Lakini iko mashaka*
> Mwenewe kuyatambua.

Mbinu hii hutumiwa na mtunzi ili aweke wazi mawazo mazito kwenye shairi. Binti Hanifu anaelewa jukumu lake la kumtoa dada yake mhanga lakini Salima mwenyewe anaweza kutambua. Huo ni usambamba wa kimaana. Pia wachawi hawa wanapokutana Shambi anasisitiza kuwa yale makubaliano yao lazima yatekelezwe. Binti Hanifu lazima amtoe dada yake sadaka. Anasema:

> 36. Akalia Binti Jizi
> Shambi akasema wazi
> *Mimi kunifanya ngozi*
> *Sitaweza kuridhia.*

*37. Mimi kunifanya ngoma*

*Sitakubali wa chama*

Bora mtoe gharama

Na miye nikitumia.

Kama mkubwa wa wachawi hao Shambi anatoa usambamba kuwaonyesha kuwa ahadi ni deni na hatakubali kuvunjwa kauli. Usambamba mwingine unaojitokeza kwenye utenzi huu ni kama ufuatavyo:

160. Jamaa wote wafike

*Wanaume na wanawake*

Na mgeni asibaki

Kama alipofika.

Usambamba huu unaonyesha utangamano wa jamii hii ambayo inashikana katika hali ya kutatanisha kama hii. Liwali anaposema *wanaume* na *wanawake* anajumuisha karibu kila mtu maana mwanamke na mwanamume kimsingi ni watu wanaojumuika kuleta umoja. Usambamba mwingine unatokea pale msanii anaposema:

222. Kaona watu wa mbali

*Waarabu* na *Waswahili*

Naye uyo Nguvumari

Njozini alimjia.

Mtunzi anaelezea taharuki ambayo inatanda katika hadhira ya kutaka kujua matokeo baada ya kuwasili Nguvumali ili awatambulishe wachawi hawa. Kuwasili kwake kunatangamanisha umati wa desturi tofautitofauti yaani *Waarabu* na *Waswahili*; hata kama wana tajiriba zisizofanana lakini kuja kwa Nguvumali kunawaleta pamoja. Pia neno matwana lina maana ya watumwa wanaume na neno majakazi ni watumwa wanawake. Liwali anasema:

262. Jaluo na Mnyamwezi
Njooni leo mle ngozi
*Matwana na Majakazi*
Leo nimewaziwia.

Hapa licha ya kutuonyesha uwezo ambao Liwali yuko nao, mtunzi anatusawiria wingi wa watu ambao Liwali amewakusanya ili wale askari Jaluo na Mnyamwezi waje tayari kutia watu adhabu. Liwali hakukusanya waungwana peke yake bali hata *Matwana* na *Majakazi*. Usambamba huu una sifa ya wingi wa watu ambao Liwali amekusanya. Uko usambamba wa aina nyingi lakini huo tulionukuu unatuonyesha kuwa jukumu la kumtafuta Salima linaunganisha kila mume na mke. Ulinganisho huo unakinzana kimaana lakini unaonyesha msisitizo wa mkusanyiko na wingi wa wahusika. Umoja wao pia unasisitizwa na kuwa harakati hizi zina umuhimu kwao.

### 3.3.8 TAHARUKI

Mbinu hii huonyesha hamu kubwa anayokuwa nayo msomaji kutokana na matarajio yake. Hajui jinsi mambo yatakavyotokea. Mtunzi huficha habari muhimu kuhusu wahusika au matukio fulani ili msomaji apatwe na hamu ya kuendelea kusoma zaidi. Pale Binti Hanifu anapopatwa na ugonjwa wa ghafla wa tumbo msomaji anapatwa na taharuki. Maswali kadhaa hujitokeza: Je, wachawi wenzake watafanya nini wakijua hali ya Binti Hanifu? Mkubwa wao Shambi atasema nini? Je, watakuja lini kumjulia hali? Shambi anakuja kumjulia hali. Je atamwambia nini Binti Hanifu? Tunaambiwa:

62. Alipofika nyumbani
Kamkuta kitandani
Anajishuku taabani
*Tumbo limeniziwia.*

63. Kasema: *Wacha mchezo*

*Utakupata mzozo*

*Uvunjapo ma(h)imizo*

*Zaani utaingia.*

Baada ya tisho hilo kutoka kwa Shambi, Binti Hanifu anaungana na wenziwe na kutimiza mahimizo.

Ujumbe huu wa Shambi unaleta taharuki. Msomaji anataka kusoma ili aone kama atamtoa dadake au atajitoa yeye mwenyewe. Mbinu hii ya taharuki huzidi kumhamasisha msomaji azidi kusoma ili aone mwisho wa kitendawili hicho.

Pia Salima anapopotea wachawi hao wanajitia kimbelembele. Wanaungana na wanakijiji wengine katika harakati za kumtafuta Salima ili wazuzue wanakijiji. Mshairi anasema:

134. Wale wachawi yaqini

*Wakisha rudi nyumbani*

*Kujitia makundini*

*Shauli kusaidia.*

Msomaji anaingiwa na hamu ya kutaka kujua ni mbinu gani wachawi hawa watatumia ili wasitambulikane. Binti Ramadhani naye anajitia ushekhe maana tunaambiwa:

168. Mama Binti Ramadhani

Maneno alibaini

*Nitie kwanza ubani*

*Ndipo tutaendelea.*

Msomaji anapatwa na taharuki ya kutaka kujua kama Binti Ramadhani atakubaliwa kutia ubani. Baada ya wachawi hao kumwacha Salima msituni, tunajiuliza kama Binti Hanifu atakuja usiku kumwokoa Salima au vipi? Binti Ramadhani je, atamhurumia mwanawe

kwa kumrudisha Salima kwake? Je, wanakijiji watampata kabla hajauawa? Maswali haya humpa hamu msomaji kutaka kuyajibu. Pia pale Shambi anapopendekeza Nguvumali aitwe msanii anatwambia;

> 184. Bwana Shambi kalatwili
> Na kujitia fahari
> *Hapa aje Nguvumali*
> *Ndiyo haswa welekea.*

Tuna hamu ya kutaka kujua sifa za Nguvumali ni za kweli? Nguvumali anapowasili msomaji huwa na hamu ya kujua matokeo. Mbinu hii hutumiwa na mtunzi ili akuze sifa za wahusika na kumpa msomaji hamu ya kutaka kusoma zaidi.

### 3.3.9 MBINU REJESHI

Mbinu hii hurejelea matukio ya wakati uliopita ili iimarishe hisia za msomaji kuhusu wahusika hao. Mbinu hii humwangazia msomaji matukio ya awali. Mtunzi huimarisha historia ya mhusika kwa kutumia mbinu hii, na pia mbinu hii humfanya msomaji asichoke. Humpumzisha msomaji asiendelee kusoma mtindo ule ule na hivyo kumwongezea taharuki ingawaje mtindo huu huathiri mtiririko wa matukio. Salima anasema kwamba:

> 104. Mimi nalitumai
> Tukae wote nyumbani
> Mwenzangu una undani
> *Kumbe ukinifanyia.*

Hapa tunaelezwa juu ya uhusiano waliokuwa nao dada hawa tangu zamani. Kulingana na Salima hakukuwa na ubaya wowote kati yao. Kumbe Binti Hanifu alikuwa na njama za kumwangamiza.

Anapomaliza kutunga mtunzi anatupa asili ya utunzi wake. Anasema:

385. Babu yangu wa kikeni
*Akitunga (h)apo zamani*
Kitabu akaweka ndani
Na mama akamwusia.

386. *Nikifa miye mwanangu*
Ndani muna kitabu changu
Mpe mjukuu wangu
Na radhi nitakuwea.

Mtunzi anatubainishia kuwa umalenga wake ni wa kurithi. Babu yake ambaye alikuwa akitunga *pale zamani* alimpa binti yake utungo ili amkabidhi yeye pindi anapofariki. Mama yake hakuwa na haraka. Alimsubiri mpaka alipomaliza kusoma, maana mtunzi anatuambia:

387. Baada ya kutoka chuoni
Mama akanita ndani
*Kitabu (h)iki zamani*
*Baba alikuwekea.*

Baada ya kukipokea kitabu hiki mtunzi anatuambia:

388. *Nikaona mwanzo wake*
*Mpaka na mwisho wake*
Yote maneno yake
*Moyoni yakaningia.*

Anatueleza kuwa baada ya kukisoma tangu mwanzo hadi mwisho alikipenda kwa sababu kila neno lilipenya moyo wake na kumpa mwamko katika dhana hii ya utunzi. Kwa hivyo anapoandika mtunzi hutumia mbinu rejeshi kuyaelezea matukio yaliyotokea wakati wa nyuma ya wakati wa hadithi yenyewe.

### 3.3.10 MBINU ELEKEZI

Mtunzi huonyesha hadhira mwisho wa kisa, jambo ambalo humtia taharuki msomaji azidi kujiuliza jinsi tukio hilo linavyofikia hapo, ingawaje mbinu hii haimfungi msomaji kutaka kujua mwisho wa kisa. Mbinu hii pia hutabiri matukio ya baadaye. Salima anamwambia dada yake:

110. Dada yangu waniua
Bila kisa kujua
*Lakini utatambua*
*Zahani utaingia.*

111. *Utaingia zahani*
(H)una raha duniani
Ujue hasa yaqini
*Ajiri kwa kuzaliwa.*

Salima sasa anapewa dawa ya kumlegeza viungo vya mwili na kumlemaza hisia zake. Lakini anamwonya dada yake kuwa yatampata mazito. Binti Ramadhani mkwewe pia anaingiwa na kiwewe mpaka anaachana na kundi hilo. Anasema:

115. Asemavyo mkwe wangu
Umenipata uchungu
Hayo kweli si urongo
*Najua yatatokea.*

Salima ni mkewe Ramadhani Mponda mtoto wa Binti Ramadhani. Binti Ramadhani anajuta kwa kumfanyia maovu mkwewe. Liwali anapowasili Panenenene anaungana na wenyeji kufuturu na baadaye anasema:

159. Kwisha kula katamka
Usiku umishafika
*Tulalapo kuamka*
*Hewani nahitajia.*

*160. Jamaa wote wafike*
Waume na wanawake
*Na mgeni asibaki*
*Kama alipofikia.*

Liwali anaongea sasa juu ya mambo yatakavyofanyika keshoye. Hamu ya kutaka kujua matukio ya *kesho yanamfanya msomaji asome zaidi ili ajue yatakayojiri. Pia mtunzi* humpumzisha msomaji kwa kuvunja mtiririko wa matukio aliyozoea.

3.3.11 CHUKU

Mbinu hii hujitokeza pale msanii anapokuza jambo au kulifanya liwe dogo sana kupita kiasi. Mbinu hii hudhamiria kusisitiza sifa hiyo ya ukubwa au udogo na huchangia katika kuhimiza masuala fulani katika kazi husika. Kwenye utenzi huu mshairi anasema:

276. Polisi (h)ao wawili
*Kama ni kumi na mbili*
Walipanda baiskeli
Wanaluka kama njiwa.

Hapa mshairi anachimza swala la nguvu iliyonayo serikali. Mjaluo na Mnyamwezi wanavuruga kijiji kizima kama kwamba ni askari *kumi na mbili.*

Moyo wa Binti Jizi unapewa hisia ya kuwa na hamu ya kutaka kuwaarifu wenziwe yale aliyoambiwa na Shambi kwa haraka. Mbinu hii inatuonyesha nia ya wachawi hawa

kutimiza waliyoyapanga himahima, na kwa kuwa wanamwogopa Shambi wanayakubali maana Binti Ramadhani anasema:

54. Akipata Bwana Shambi
*Sisi tuko mvivumbi*
*Tutakuwa lambilambi*
Hatuna pa kusemea.

Vumbi ni kitu kama unga kitokanacho na msagiko wa mchanga, udongo, mawe au mbao. Binti Ramadhani anatoa sifa za Shambi kwa kusema: *Sisi tuko mvivumbi*, *tutakuwa lambilambi* anamsifu Shambi kupindukia kuwa ana uwezo wa kuwasaga wakabakia vumbi. Kusisitiza uwezo wa Shambi, Binti Ramadhani anatumia neno *rambirambi*, yaani anaweza kuwaua.

### 3.3.12 NJOZI

Mbinu hii hueleza maono anayopata mtu usingizini. Mara nyengine mambo hutokea kama vile mtu anavyoota. Katika njozi mtu huoteshwa ufahari, uchochole, adhabu n.k. Katika utenzi huu Binti Ramadhani anasema:

121. Kulala ni kibuhuti
(H)ujiona sakarati
*(H)ujiotea mauti*
*Watu wananichukua.*

Binti Ramadhani hulala akiweweseka na kushtukashtuka, huwa na huzuni, majonzi na majuto. Pia huota amekufa. Njozi hizi huwa kama onyo kwa mhusika anayezipata. Mshairi humpa msomaji matarajio kuhusu njozi hizi kuwa jambo hili laweza kutokea. Kwa ajili ya ndoto hizi, Binti Ramadhani anaepukana na wachawi wenziwe katika kumfanyia uchawi mkwewe Salima. Binti Ramadhani haoni usalama wake mwenyewe ukiimarika.

Baada ya Shambi kutarajia na kuahidi kumgharamia Nguvumali, njiani anaporudi nyumbani anaona vioja. Nyoka wawili wanafuata kivuli chake. Anapofika nyumbani anataka kuthibitisha kama Nguvumali ni mganga kweli au la. Lakini kabla ya usiku, pembe zake za uchawi zinapasukapasuka. Koja lake linakatikakatika vipande, ndumba zake zinakuwa pesepese (216) na hali nyengine zinazoonyesha kuvurugika. Hapo mtunzi anasema hivi kumhusu Shambi:

220. *Kaota anaanguka*
*Na makamasi kutoka*
*Na machela yamefika*
*Yakuja kumchukua.*

222. *Kaota watu wa mbali*
*Waarabu na Waswahili*
*Naye uyo Nguvumari*
*Njozini alimjia.*

223. *Kaota anasema naye*
*Na koja kampa yeye*
*Mfano kama nduguye*
*Na vingi kumtolea.*

Njozi hizi zinamtia Shambi uoga. Anaota kutokwa na makamasi baada ya kuanguka na machela yanambeba. Kuja kwa Nguvumali kunavutia watu wengi- Waarabu na Waswahili wanakuja kumwona Nguvumali. Kisha anachukua koja lake na kumpa. Mambo haya yanamtokea Shambi, Nguvumali anapowasili. Kwa hivyo mtunzi anatumia mbinu hii kutuonyesha vile Shambi anauona mwisho wake. Pili Nguvumali ana uwezo wa kuwatambua wachawi hawa; tatu kuja kwa Nguvumali kunavutia watu wengi.

### 3.3.13 KEJELI

Mbinu hii hutumiwa wakati ambapo msemaji hutamka maneno ambayo maana yake ni kinyume. Mtunzi katika utenzi huu anasema:

> 134. Wale wachawi yaqini
> Wakisha rudi nyumbani
> *Kujitia makundini*
> Shauli kusaidia.

Mtunzi anaposema *kujitia makundini* anatupa hadithi ndefu sana. Kwa ufupi wachawi hawa wanataka kuwazuzua wanakijiji ili uovu wao usitambulikane. Katika ubeti wa 168, Binti Ramadhani anataka kuwa wa kwanza kuchoma ubani kabla ya kuanza shughuli za kumtafuta Salima. Wanataka kuomba dua ili shughuli hiyo ifanikiwe lakini moyoni Binti Ramadhani anajua kuwa haitafanikiwa maana yeye na wachawi wenziwe wameshatekeleza yao. Kitendo chake cha kutia ubani kinapotosha.

Bwana Shambi kama kiongozi wa wachawi naye anapendekeza Nguvumali aitwe aje amtambue mwuuaji wa Salima. Anasema:

> 184. Bwana Shambi kalatwili
> Na kujitia ufahari
> *Hapa aje Nguvumali*
> *Ndio haswa welekea.*
>
> 185. *Nguvumali afike*
> *Afanye uganga wake*
> *Na kiumbe aoneke*
> *Mimi ninahitajia.*

Anaweka dhamana ya kulipa gharama ya Nguvumali. Anaitia saini barua ya kumwalika (197). Katika ubeti wa 233 Binti Hanifu anatoa ushuhuda wa kumwona dada yake Salima aliyekwenda kukata kuni na kibanda kikamwangukia, akafa. Kwa hivyo mbinu hii ya kejeli inanawirisha hisia na sifa za wahusika hawa.

### 3.3.14 NAHAU

Hii ni mbinu ya kutumia lugha ili ijenge picha fulani kwa msomaji. Msanii hutumia maneno yenye maana maalumu yasiyotokana na maana ya kawaida ya maneno hayo. Shambi anapendekeza kuwa Nguvumali aitwe. Msanii anasema:

184. Yale anayoeleza
Anafanya ninatengeza
*Kumbe khadithi ya pweza*
*Makaa kujiparia.*

Maana ya maneno haya *kumbe khadithi ya pweza, makaa kujiparia* ni kwamba pweza anapowekwa makaani akiwa hai hutumia mikono yake kujipalia makaa. Hii ndiyo maana ya kawaida, lakini maana maalumu ni kwamba Shambi ni mkuu wa wale wachawi wanne na anapohitajia kuwa Nguvumali aitwe, ni yeye atakayeingia taabuni kama yule pweza anayejipalia makaa. Jambo hili la Shambi kupendekeza Nguvumali aitwe linampa msomaji hamu ya kusoma utenzi huu ili aweze kujua kuwa Nguvumali atakapokuja hali itakuwa vipi maana Shambi anajitia mashakani. Pia pale Liwali anapowaita askari Mjaluo na Mnyamwezi mtunzi anaandika hivi:

262. Jaluo na Mnyamwezi
*Njooni leo mule ngozi*
Matwana na majakazi
Leo nimewaziwia.

Maana ya kawaida ya maneno haya: *Njooni leo mle ngozi* ni kwamba hao askari waje ili wapewe ngozi waile. Lakini maana maalumu ni kwamba wapige watu ili waseme ni nani aliyemwua Salima. Mbinu hii hueleza udhati wa hali kwa lugha ambayo maana yake ni fiche. Mbinu hii inatumika kwingi kwenye utenzi huu. Kwa mfano ubeti wa 280 mtunzi anasema *viliingia vibao* yaani watu wanapigwa sana. Pia *vibao vimeenea* (352) ina maana kwamba watu walipigwa sana ili waseme mwuuaji ni nani. Katika ubeti wa 154 mtunzi anasema kuwa askari *wamepata ngozi zao* yaani walisheherekea hali hii ya kupiga watu vilivyo ili wawatambulishe wauaji. Shambi anapotambuliwa kuwa yeye ni mmoja wa wauaji anasema: *kuja kunipaka vumbi* (373) yaani Nguvumali amekuja kumharibia sifa na jina lake. Hii ndiyo maana maalumu. Mshairi anatumia nahau ambayo inamfanya msomaji aingiwe na msisimko na hamu ya kusoma utenzi huu kwa dhati.

### 3.3.15 LITIFATI

Mbinu hii hujitokeza pale mtunzi anapomwacha mhusika awasiliane na msomaji kwa njia ya moja kwa moja. Hapa mtunzi huepukana na jukumu la kutoa sifa ya mhusika au matukio. Msomaji huona sifa ya mhusika kutokana na maneno ya mhusika mwenyewe. Binti Jizi anaongea na Binti Hanifu kwa kumwambia:

*22. Awe mtoto wako*
*Ao ni ndugu yako*
*Asiwe jelani yako*
*Siye anayetakiwa.*

Kwa hivyo wahusika huwasiliana wao kwa wao.

Pia kwa ajili ya msimamo dhaifu wa baadhi ya wachawi wenzake Shambi anawaarifu:

*36. Mimi kunifanya ngoma*
*Sitakubali wa chama*
*Bora mutoe gharama*
*Na miye nikitumia.*

Hapa Shambi anateta, na msomaji anashuhudia utesi huo moja kwa moja kuwa hao wenzake wasimfanye mpuuzi au wasimdharau. Mbinu hii pia inajitokeza pale Salima anapoongea na dada yake katika beti za 85, 103, 104, 105 n.k. Shambi naye anamwambia Binti Hanifu amweke Salima mahali panapostahili ili apewe madawa. Anamwambia *basi apo mweke (82).*

Binti Ramadhani anageuza nia ya kuendelea kumtesa Salima maana malalamiko ya Salima yanayeyusha ukatili wake. Anasema:

127. Mwana Binti Ramadhani
Akijitoa kundini
*Toka leo abadan*
*Siwezi kushuhudia.*

Kwa hivyo msanii humnukuu msemaji moja kwa moja. Mara nyengine unukuzi unaweza kuwa na wasemaji wawili au zaidi.

### 3.3.16 TASWIRA

Mbinu hii hujitokeza wakati mtu anapoona mambo au vitu vikimjia akilini mwake. Picha hii huundwa na neno, kirai au maelezo fulani. Ishara pia huweza kuleta taswira akilini mwa mtu. Ishara hizi huwa na maana inayofichika. Katika utenzi huu mshairi anatueleza kuwa Shambi anaonyesha ufahari hata akahimiza kuitwa kwa Nguvumali aje awatambue wachawi hao. Pia anaahidi kumlipa gharama zake. Lakini vijana hawa Yasini Kinina na Hamadi Ramadhani wanapoenda kumwita Nguvumali, Shambi anaanza kuona ishara mbaya. Mtunzi anatuambia:

*210. Kaona nyoka wawili*
*Wanamfata kiviri*
Dalili ya Nguvumali
Ya kuweza kumjia.

Hii ni ishara ya kuwa Nguvumali anapowasili Shambi anaweza kutambulikana kama mchawi. Taswira kama hii huzua hofu.

Katika kutueleza juu ya hizo shamrashamra mtunzi anasema

310. Watu walijumuika
*Mji ulitikisika*
Palikuwa patashika
Zagao limeingia.

Taswira hii inatuonyesha hali ilivyo mjini baada ya kuja kwa Nguvumali. Binti Ramadhani anakufa: Binti Hanifu anakuwa majinuni; yaani akili yake inachanganyika, Shambi anaungama kuwa yeye ndiye mchawi; anasema katika ubeti wa 334. *Mtu nimeua mimi.* Kwa hivyo, Hasani bin Ismail anatuonyesha hisia changamani za wanakijiji. Kule mji *kutikisika* ni taswira ya taabu ambazo wanakijiji wanazipata wakati Nguvumali anapofanya uganga wake. Mtunzi anatusawiria hali halisi ya kijiji hicho.

## 3. 4.0 MUUNDO

Kulingana na Mbatiah (2001), Wamitila (2003), Grill (1985), Msokile (1993) na Mohammed (2002) wanakubaliana kuwa kuna miundo ya aina nyingi katika sanaa tofauti, na hata katika maumbo ya sanaa ya aina moja. Wanasema maana pia husababisha tofauti hizo. Katika ushairi kuna maudhui ya utamaduni, mapenzi, siasa n.k. Katika kuelezea mada hizo kunaweza kuwa na vipengele vya fani vinavyotofautisha maudhui hayo. Katika mashairi ya kimapokeo vipengele vya wizani, vina, mizani na beti hujitokeza. Muundo huhusisha mtiririko wa matukio katika shairi ili kueleza kisa.

Tunapofanya uhakiki tunajaribu kuchunguza jinsi msanii anavyounda na kuunganisha matukio, vitendo na mawazo. Baadhi ya kazi za kifasihi zina miundo ya moja kwa moja ilhali miundo mingine ni changamano. Wakati tunapohakiki muundo tunachunguza elementi katika mpangilio thabiti wa kazi hizo na jinsi zinavyounganishwa. Kutokana na mpangilio huo tunapata umbo, ruwaza na sura maalumu. Mbinu hii hurejelea uhusiano unaokuwako kati ya vipengele mbalimbali vinavyounda kazi kamili ya kijumla. Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* Hasani Ismail huenda mbele na nyuma ili kuthibitisha matukio fulani katika visa hivyo. Mtiririko wa hadithi yake si wa moja kwa moja.

### 3.4.1 BETI

Hii ni mbinu ambayo mtunzi hugawanya kazi yake kwenye vifungu mbalimbali vilivyo na idadi sawa ya mistari. Kwa kawaida tenzi huwa na mistari minne katika kila ubeti. Katika beti tatu za kwanza mshairi anaomba dua ili Mungu ampe nguvu, fahamu na hekima. Anasema:

3. *Rabbi nipe fahamu*
*Unijalie elimu*
*Nataka kuyahukumu*
*Shairini kuyatia.*

Kutoka ubeti wa nne msanii anaanza kuchonga kalamu na kuanza kutueleza kisa chenyewe mpaka ubeti wa mia tatu themanini na tatu. Kutoka ubeti wa mia tatu themanini na nne anamaliza hadithi yake na kuingilia usuli wa utunzi wake. Kimsingi utenzi huu unagawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni dua, sehemu ya pili ni kisa chenyewe na sehemu ya tatu ni usuli wa utunzi wake. Utenzi huu una beti mia tatu tisini na tatu.

### 3.4.2 MIZANI

Mbinu hii hurejelea idadi ya silabi au mizani katika kila mshororo. Katika ubeti unaofuata mtunzi anatuambia hivi:

161. *Basi wamelala pale*
*Nyumba ya mauti yule*
*Mfano utafikiri*
*Kama kenda kutembea.*

Ubeti huu una mishororo minne na kila mstari una mizani au silabi nane. Katika mazingira fulani [m] hujiainisha kama kitamkwa. Kwenye ubeti huu mshororo wa tatu *Mfano Utafikiri*, herufi 'm' inajiainisha kama kitamkwa kwa hivyo mshororo huu una mizani nane. Vokali pia zina sifa za kitamkwa. Kwa mfano:

156. *Alitoka peke yake*
Kwa hapo nyumbani kwake
*Aliwapata wenzake*
Baada ya kuendelea.

Katika ubeti huu mshororo wa kwanza unaanza na herufi *'a', Alitoka peke yake* ambapo inajiainisha kama kitamkwa. Hata katika mshororo wa tatu katika ubeti huu huu yaani *Aliwapata Wenzake*; herufi '*a'* pia ina sifa ya kitamkwa, hivyo basi mishororo hii ina mizani nane nane. Kwa mfano:

23. Awe mtoto wako
*Ao ni ndugu yako*
Isiwe jelani yako
Siye anayetakiwa.

83. *Kabla ya kumweka chini*
Dadaye alibaini
Hiyo deni nampani
Sina nnalodaiwa.

130. Basi leo abadan
Tena narudi nyumbani
*Agheru shetani*
Najuta na kuzaliwa.

Ubeti wa 23 mshororo wa kwanza na mshororo wa pili ina mizani saba, ubeti wa 83 mshororo wa kwanza una mizani tisa, ubeti wa 130 una mizani sita. Mifano mingine ya mtunzi kushindwa kudhibiti mizani nane katika kila mstari inajitokeza katika beti za 9, 27, 40, 82, 110, 136, 152, 153, 155, n.k.

### 3.4.3 VINA

Hizi ni sauti au silabi zinazopatikana mwisho wa mshororo katika utenzi ambao hauna vina vya kati. Kina ni kitamkwa cha mwisho cha mshororo ambacho huwa na upatanisho na vina vingine. Zingatia kuwa kina cha mstari wa mwisho katika kila ubeti wa utenzi huitwa bahari. Katika utenzi huu mtunzi anajitahidi kuleta upatanisho wa vina. Vile vile katika ushairi vokali *a*, silabi *wa* na silabi *ya* hazitofautishwi sana maana herufi *w* na *y* ni nusu vokali kwa hivyo matumizi yao huweza kupishana kama katika beti za 23, 83, 130 n.k hasa katika ukariri wa mashairi. Katika ubeti ufuatao mtunzi anasema:

1. Bismilahi naa*nza*
Jina la Mola wa e*nza*
Muhammadi mpende*za*
Kwa Mola wetu Jalia.

Katika mshororo wa pili kina kingekuwa *zi* lakini ametumia *za*. Nia yake ya kufanya hivyo ni kupata mfanano wa vina. Kwa hivyo mshairi amefaulu katika jukumu hilo ndiposa tunaona kuwa mishororo ya tatu ya mwanzo ina vina *za*. Upatanisho huo pia unajitokeza kwenye ubeti wa 10 n.k. Tunapata upatanifu katika beti za 118, 127, 144, 170, 200, 358, 307, 341 n.k. Katika ubeti ufuatao msanii anaonekana kama ameshindwa kuleta upatanisho wa vina. Kwa mfano:

5. Zilitokea khabari
Sasa nakupa ajiri
Awali ya Nguvuma*li*
Hapa Siwa kuingia.

Katika mshororo wa kwanza na wa pili kina ni *ri* na mshororo wa tatu kina ni *li*. Hii ni kwa sababu katika lahaja ya Kilwa matumizi ya /*r*/na /*l*/ huweza kubadilishana.

## 3.5 TONI

Kulingana na Wamitila (2003), Grill (1985) na Roberts na mwenzake (1972) dhana hii huhusishwa na hisia zinazomjia msomaji. Hisia hizi hutokea pale mshairi anapoongea, hali yake, sauti yake, mikogo yake, maringo yake, miondoko yake, mwelekeo wake, matarajio yake na jinsi anavyozuia mihemko yake. Mwelekeo wa mshairi na wa msomaji huwa vipi? Msomaji anaibuka na hisia gani? Yote haya hujitokeza katika toni ya mshairi. Mambo kama chuku, stihizai, sitiari, tashibihi, uteuzi wa msamiati hujitokeza na hujenga hisia za msomaji kupitia kwa toni. Nia kubwa ya mshairi ni kumsisimua, kumburudisha na kumwelimisha msomaji. Kuzua mihemko kwa msanii ni jambo muhimu kwa sababu msomaji hujenga hisia zake kutokana na hali hiyo ya msanii. Kwa hivyo toni huelezea mkabala wa msanii kuhusu wahusika alionao kwenye shairi. Tunachokisema ni kwamba mseto wa toni zinategemea aina ya mawazo na jinsi yanavyowasilishwa na mtunzi.

Toni hizi huzua hisia za msomaji wakati msanii anapoimba shairi lake. Zinaweza kuwa hofu, sikitiko, huruma, huzuni n.k. Katika utenzi huu mtunzi anatumia toni ya unyenyekevu mbele ya Mwenyezi Mungu anapoanza utunzi wake. Tunapousoma utenzi wenyewe tunaona kuwa zile beti tatu za kwanza ni toni ya dua. Kwa mfano:

1. *Bismillahi naanza*
*Jina la Mola wa enza*
*Muhammadi mpendeza*
*Kwa Mola wetu Jalia n k.*

Mshairi anamwomba Mungu amwondolee udhia wa aina yoyote, ampe fahamu, amjaalie elimu na uwezo maridhawa ili aweze kutoa hukumu inayostahili.

Aina nyingine ya toni inayojitokeza kwenye utenzi huu ni ile ya kutisha. Shambi anamtisha Binti Hanifu, na pia ana toni ya kuamrisha na yenye matusi. Katika ubeti ufuatao Shambi anamtisha Binti Hanifu kwa kumwambia:

63. Kasema: *Wacha mchezo*
*Utakupata mzozo*
*Uvunjapo ma(h)imizo*
*Zaani utaingia.*

Binti Hanifu anatishwa hali ya kwamba anakiri kufuata amri na matakwa ya wachawi wenziwe maana anasema:

65.*Basi Bwana nimekiri*
Sasa nafanya safari
Najivuta kwa dhamiri
Kama ulivonambia.

Baada ya kutishwa na Shambi, Binti Hanifu anaondoka haraka kwa kuogopa matokeo ya vitisho hivyo. Hapa tunashuhudia toni ya kukiri na kunyenyekea.

Wakati wachawi hao wanapomzonga kwa kutumia madawa Salima anamwambia dada yake;

104. Mimi nalitumai
Tukae wote nyumbani
*Mwenzangu una undani*
*Kumbe ukinifanyia.*

110. Dada yangu waniua
Bila kisa kujua
*Lakini utatambua*
*Zahani utaingia.*

Hapa Salima anatumia toni ya unyenyekevu, kusihi na wosia. Anamtabiria dada yake adhabu atakayopata hapa duniani na akhera.

Baada ya malalamiko ya Salima, Binti Ramadhani anasema:

115. Asemayo mkwe wangu
Umenipata uchungu
*Hayo kweli si urongo*
*Najua yatatokea.*

Binti Ramadhani anaonyesha majuto maana hatimaye anawashauri wachawi wenziwe wamrudishe Salima nyumbani lakini mkubwa wao Shambi anakataa. Anasema:

127. *Akisharudi nyumbani*
*Utafanya dawa gani*
*Wote wanamjuani*
*Waweza kusimuria.*

Toni ya Shambi ni ya kutaka kujua kwamba wakimrudisha Salima nyumbani kutatokea nini? Hii ni toni ya kuuliza kwa hivyo athari ya maneno ya msimulizi kupitia kwa mhusika ndiyo inayoipa ufanifu toni na kujenga hisia kwa msomaji.

## 3.6 MSUKO

Hii ni mbinu ambayo msanii hutumia katika kazi ya kifasihi kutuonyesha mpangilio wa matukio yakifuatana. Tunashuhudia tukio moja likitokea baada ya lingine. Wakati mwingine matukio hayafuatani kimpangilio.

Katika kazi ya kisanaa, msuko ni dhana muhimu sana maana *huhimidi maudhui na* dhamira ya msanii. Wakati mwingine mtunzi husheheneza msuko vitushi vingi kiasi ya kumshangaza msomaji. Kwenye utenzi huu tunamwona mtunzi akiomba dua katika beti tatu za mwanzo ili Mungu ampe hekima ya kuweza kutunga bila ya matatizo yoyote. Kutoka ubeti wa nne hadi wa tisa mtunzi anatanguliza hadithi na kutueleza dhamira yake ya kutunga. Kisa chenyewe kinajitokeza katika sehemu ya pili ambapo wachawi wanne wanakutana na kupendekeza kuwa mmoja wao atoe aali yake mhanga ili wakifanyie kijiji hicho zinguo. Binti Jizi, mmoja wa wanawake hao wachawi anamwambia Binti Hanifu hivi:

19. *Sasa hivi duru kwako*
*Utoe na wewe wako*
*Kutumai kwa wenzako*
*Wengi watakukimbia.*

Anapoambiwa hayo Binti Hanifu anaonyesha kusitasita kwa sababu haoni vile anavyoweza kutekeleza jukumu hilo. Tunaambiwa:

21. Binti Hanifu katamka
*Ni kweli hiyo hakika*
*Lakini iko mashakka*
*Mwenewe kuyatambua.*

Jawabu thabiti kutoka kwa Binti Jizi linatokea. Anamwambia Binti Hanifu:

22. Binti Jizi kakalili
*Mimi nakupa ukweri*
*Huyo huyo mkabili*
*Ndiye anayetakiwa.*

23. *Awe mtoto wako*
*Ao ni ndugu yako*
*Isiwe jelani yako*
*Siye anayetakiwa.*

Baada ya mazungumzo hayo wanaagana kukutana siku ya pili ambapo Binti Hanifu hakuhudhuria sababu ya uzito wa swala hilo la kumtoa dada yake Salima kafara. Shambi anamtuma Binti Jizi kwamba:

40. *Binti Hanifu mwambie*
*(H)apo atoe nduguye*
*Ao yeye afidie*
*Sisi tutampokea.*

Jawabu hili linamtatanisha Binti Hanifu mpaka anakuwa mgonjwa wa tumbo. Shambi anakasirika na kwenda mwenyewe kwa Binti Hanifu na kumwambia:

63. Kasema: *Wacha mchezo*
*Utakupata mzozo*
*Uvunjapo ma(h)imizo*
*Zaani utaingia.*

Shambi ni kiongozi katili. Binti Hanifu anatanzika maana kama hangemtoa dada yake mhanga basi yeye angekuwa badili yake. Anamwambia Shambi:

65. *Basi Bwana, nimekiri*
*Sasa nafanya safari*
*Najivuta kwa dhamiri*
*Kama ulivonambia.*

Hapa sasa dhamira ya Binti Hanifu ishapata mwelekeo maana baada ya kukubaliana na wachawi hao anatekeleza azima hiyo. Hili ni tukio la kwanza. Tukio la pili ni lile ambalo

Salima anapatwa na madawa ya wachawi hawa na sasa amerukwa na akili. Anaenda kule kuliko na wachawi hao. Kulingana na yeye anaenda kukata kuni peke yake lakini msanii anatwambia:

74. *Anapotea porini*
*Upande ule wa pwani*
*Maskini maskini*
*Salima anapotea.*

Tukio hili linampeleka Salima huko porini bila ya yeye kudhamiria. Huko anauawa na wachawi hao licha ya kuwanyenyekea, lakini kabla ya kuuawa Salima anamsihi dada yake amwachilie arudi nyumbani. Salima anaingiwa na matumaini kuwa angepona maana anasema:

81. *Kumwona dada yangu*
*Sipati tena matungu*
*Iwe amri ya Mungu*
*Siwezi kukataria.*

Salima anadhania kuwa dada yake angemwonea huruma na kumwachilia. Kama ni amri ya Mungu siwezi kupingana nayo. Lakini uthabiti wa dada yake unamshangaza Salima na kumtia hofu maana msanii anatwambia:

83. Kabla ya kumweka chini
Dadaye alibaini
*Hiyo deni nampani*
*Sina nnalodaiwa.*

Binti Hanifu anawakabidhi wachawi hao deni lao. Inaonekana wazi kwamba amekata shauri kutimiza wajibu wake. Salima anapotea.

Tukio hili la kupotea kwa Salima linatupeleka kijijini ambako watu wanamtafuta bila ya mafanikio. Hapo wanaamua kupeleka ripoti serikalini. Haya yakitokea watu wanatumana

Nguvumali aje awatambulishe wachawi hawa. Hata Shambi naye anaunga mkono jambo hili maana mtunzi anasema:

184. Bwana Shambi kalatwili
Na kujitia fahari
*Hapa aje Nguvumari*
*Ndio haswa welekea.*

Bwana Shambi anaunga mkono wazo la kumleta mganga huyu. Anazuzua wanakijiji wasitambue kuhusika kwake. Vijana wawili wanatumwa na barua kwa wakili. Shambi anajitolea kulipa gharama ya Nguvumali.

Mtunzi anatueleza mambo yanayompata Shambi wakati akirudi kwake kuwa anaanza kuingiwa na hofu. Anaona *nyoka wawili wanafuata kivuli chake;* dalili ya Nguvumali. Baadhi ya vitu vyake vinapotea na vingine vinapasuka. Usiku njozi zinazomjia ni kwamba Nguvumali amewasili na watu wengi wanafika kumwona, na yeye Shambi anachukua koja lake akamtunukia Nguvumali. Baadaye anaamka akiwa na hofu.

Shambi anamtuma Binti Hanifu aende porini akidai anaenda kukata kuni. Hiyo ni baada ya kumbeba Salima hadi kibandani akiwa maiti. Msanii anatuambia hivi kuhusu Binti Hanifu:

232. Alipiga ukelele:
*Waje tena wale wale*
*Ndugu yangu yule yule*
*Nimekwisha mgundua.*

Watu wanapofika wanaiona kweli maiti ya Salima lakini ina kasoro. Pia wanashangaa kwa sababu hapo inapoonekana maiti hiyo wamepapekuapekua sana. Lakini wanashukuru na kumzika baada ya Liwali kuwasili. Polisi pia wanakuja na kufanya msako. Watu wanapigwa, Binti Ramadhani anatiwa nguvuni na anawataja wenziwe nao wakashikwa.

Tukio lingine ni kuwasili kwa Nguvumali ambaye anawatambua wachawi hao. Msanii anatuambia:

293. Sasa tunayakabili
*Turudi kwa Nguvumali*
Watoto wale wawili
Wamekwisha kurejea.

Watoto hawa wawili wanakuja na Nguvumali ambaye anawatambulisha wachawi hao. Binti Ramadhani anakufia hospitalini na wenzake wanafungwa. Sehemu hii ya pili ina beti 375 ambapo msanii anatupa dhana ya zinguo wanalofanya wachawi hao. Dhana hii inampa Binti Hanifu kilinge maana kama hatamtoa dada yake basi yeye angefidia. Kwenda mbele huku na kurudi nyuma kwa msanii huimarisha tabia thabiti ya baadhi ya wahusika kama Shambi, husawiri ugoigoi wa wahusika kama Binti Ramadhani na Binti Hanifu na kunawirisha matukio yanayofuatana.

Tukiangazia sehemu ya tatu ambayo ndiyo ya mwisho mtunzi anatueleza kuhusu chanzo cha utunzi wake. Anasema:

385. Babu yangu wa kukeni
Akitunga (h) apo zamani
Kitabu akaweka ndani
Na mama akamwusia.

386. *Nikifa miye mwanangu*
*Ndani muna kitabu changu*
*Mpe mjukuu wangu*
*Na radhi nitakuwea.*

Mtunzi anatueleza asili ya kipawa cha utunzi wake ambacho anakirithi kutoka kwa babu yake. Katika ubeti wa 389 anataja jina lake kama Hasani bin Ismail. Anasoma tena dua na kuwaambia watu wamwombee Mungu ili njia zake ziendelee kuwa nyoofu.

Kwa hivyo tunaona kwamba msuko wa utenzi huu huenda mbele na kurudi nyuma. Matukio hayafuatani kimpangilio. Muundo huu unatumiwa sana katika utenzi huu. Hapa tunapata tukio kuu ambalo ni mgogoro baina ya Nguvumali na wachawi hawa wanne. Lakini ndani ya mgogoro huu kuna matukio kadhaa ambayo yanajitokeza katika sehemu ya pili. Wachawi wanne wanakutana ili wakifanyie zinguo kijiji chao. Tukio hilo linazua mzozo baina ya wachawi wenyewe maana Binti Hanifu anakanganyika. Huyu ndiye anayetakikana kumtoa dada yake Salima mhanga. Baada ya vitisho anakubali. Tukio la pili, Salima anarogwa na wachawi hawa na kupotea, na hatimaye anakufa. Tukio la tatu ni zagao. Wanakijiji wanamtafuta na kumwona siku ya tatu ambapo mwili wake una kasoro. Tukio la nne ni pale wanakijiji wanapotumana aitwe Nguvumali aje awatambulishe wachawi hao.

Tunaporudishwa nyuma tunamwona Shambi ambaye ni mkuu wa wachawi hawa akipata taabu kutokana na nguvu za mganga Nguvumali hata kabla hajawasili. Tunarudishwa nyuma tena kwa wale watoto wanaotumwa kumleta Nguvumali. Anapowasili anawatambulisha wachawi hao ambao wanafungwa jela, na mmoja wao, Binti Ramadhani, anakufia hospitalini.

## 3.7 WAHUSIKA

Hivi ni viumbe vinavyoumbwa na msanii. Kwenye kazi ya kifasihi matendo ya viumbe hawa hufanana na matendo ya binadamu. Viumbe hawa wanaweza kuwa binadamu, wanyama, ndege, wadudu, misitu n.k. Baadhi ya wahusika hawa hupewa nafasi na mtunzi kutenda, kusema, kujiwasilisha na kujitambulisha kwa hadhira. Wanapofanya hivyo hadhira hupata fursa ya kuwajua na kuwahukumu. Kusawirika kwao pia hutegemea malengo ya msanii. Watunzi wengine huchagua viumbe visivyo binadamu ili waifumbe hadhira. Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* mtunzi Hasani bin Ismail anachagua wahusika binadamu ambao anawagawanya katika makundi mawili makuu; waovu na wema. Ndani ya kundi la waovu tunapata Shambi bin Dima; mkuu wa wachawi hawa, Binti Jizi, Binti Hanifu na Binti Ramadhani. Wachawi hawa wanasawiriwa kama waovu na makatili. Msanii anatuambia kuhusu wachawi hawa kwamba:

10. Wachawi wanne yaqini
Walikutana jioni
*Shauli gani jamani*
*La kuweza kutumia?*

Wachawi hawa wanakaa faragha ili wajue vile watafanya juu ya kuzingua kijiji chao. Mkubwa wao ambaye ni Shambi anamwagiza Binti Jizi kwamba:

40. *Binti Hanifu mwambie*
*(H) apo atoe nduguye*
*Ao yeye afidie*
*Sisi tutampokea.*

Msanii ananawirisha ukatili wa Shambi kutokana na maneno yake. Hadhira inashuhudia pia ukatili wake moja kwa moja. Ukatili wake unajitokeza zaidi anaposema:

334. Akautoa ulimi
Unawaka kama lami
*Mtu nimeua mimi*
Jamii wakasikia.

Anaposema *mtu nimeua mimi,* Shambi anatuthibitishia kuwa yeye ni mchawi na anahusika na kifo cha Salima.Baada ya kumwua Salima, Shambi anakata ulimi wake ili afanyie uchawi zaidi.

Tukimrejelea Binti Jizi, mtunzi anamsawiri kama mwanamke katili maana anamwambia Binti Hanifu:

23. *Awe mtoto wako*
*Ao ni ndugu yako*
*Isiwe jelani yako*
*Siye anayetakiwa.*

Mtindo huu wa kutoa kafara unaonekana hauanzi leo. Inaonekana kila mchawi ameshatoa mtu wake mhanga na mtu huyo ana sifa maalumu. Kwa mujibu wa wachawi hao jirani si mtu muhimu katika harakati zao. Anapokubali kumtoa dada yake kafara haangalii tena nyuma. Anasema:

83. Kabla ya kumweka chini
Dadaye alibaini
*Hiyo deni nampani*
*Sina nnalodaiwa.*

Hapo awali tumesema kwamba inaonekana wachawi wengine wameshatoa madeni yao isipokuwa Binti Hanifu. Baada ya kumwua Salima, wachawi hao wanajitia kundini katika kumtafuta Salima. Binti Ramadhani anasema:

168. Mama Binti Ramadhani
Maneno alibaini
*Nitie kwanza ubani*
*Ndipo tutaendelea.*

Msanii hapa anamsawiri Binti Ramadhani kama mtu mwovu ambaye baada ya kuua anajifanya mtu wa dini. Anaanza yeye kutia ubani. Mwanamke huyu anafumba watu macho ili wasimtilie shaka.

Wahusika wema ni kinyume cha wahusika waovu. Katika kuonyesha uovu wa wachawi hao mhusika mwema ambaye ni Salima anachaguliwa na msanii atolewe kafara. Baadhi ya wahusika wema ni Bwana Mwenye ambaye anakwenda kupiga ripoti serikalini juu ya kupotea kwa Salima. Anasema:

138. *Bassi sasa naondoka*
*Lipoti naipeleka*
*Isituwee mashakka*
*Halafu tukasangaa.*

Bwana Mwenye ana dhamira za aina mbili. Ya kwanza ni kumpata Salima kwa kutaka msaada serikalini, na ya pili ni kujikinga yeye na wanakijiji. Vile vile msanii anawasawiri Liwali Selemani Nufusi na jumbe wake Hamisi kama watu wema; maana anatuambia:

152. Liwali Selemani Nufusi
Na jumbe wake Hamisi
*Wana huruma za kasi*
*Walitamani kulia.*

Maneno haya yanatusawiria wema wa watu hawa wawili. Tunaonyeshwa utu wao maana tunajulishwa juu ya hisia zao.

Wale vijana wawili wanaotumwa kwenda kumleta Nguvumali pia ni watu wema maana msanii anatuambia:

200. Wa kwanza Yasini Kimina
*Kijana wetu (h) azina*
*Hapendi mambo ya laana*
*Tena yeye mzaliwa.*

Msanii anampa kijana huyu sifa za aina tatu: Kijana huyu anapendwa sana yaani *hazina,* pia hapendi kufanya mambo yenye *kuleta laana* na yeye ni *kijana wa kijijini.*

Kuhusu kijana wa pili, msanii anatwambia:

201. Wa pili Hamadi Ramadhani
*Kijana mwenye imani*
*Ngawa aswi chuoni*
*Lakini kaelekea.*

Kuwa yeye hakusoma sana si jambo lenye ubaya maana ni mtu mwenye *imani na anapendeza.*

Selemani na Bwana Hamisi ni watumishi wa serikali ambao wanapokea ujumbe wa kupotea kwa Salima (141). Komera na Bwana Kagendu pia ni watu wema (165, 203). Wanawahamasisha wanakijiji katika harakati za kumtafuta Salima. Nguvumali naye anasawiriwa kuwa na sifa ya kupambana na wachawi jambo ambalo ni kinga kwa wanyonge. Mtunzi anatueleza haya kumhusu:

294. Wamerudi na Nguvumali
Mganga wa kiasili
*Hata chini ya jabali*
*Uchawi anautoa.*

Kufanya hivyo yaani kutoa uchawi ni jambo la busara. Nguvumali anatambulikana na kukubalika serikalini (303). Wahusika wengine ni Jaluo na Mnyamwezi ambao wanafanya uchunguzi wa kuwapata wahalifu. Pia wale wanaokuja na Nguvumali ni wahusika wema. Pengine hatuwataji wahusika wote lakini kimsingi wahusika wema hujitambulisha kwa hadhira kupitia kwa matendo na maneno yao kama wafanyavyo wahusika waovu ambao ukatili wao unakithiri. Mshairi anawaumba ili dhamira na maudhui anayokusudia yajitokeze. Katika kuendeleza msuko wa hadithi kuu wahusika hawa wanachangia sana matukio kadha ambayo yameunda kisa chenyewe.

Pia katika kutuonyesha hamasa zinazowapata wanakijiji mtunzi anatwambia:

163. Hatima wakaamka
Na jamaa wakafika
*Wale aliyewataka*
*Na wengine kuzidia.*

164. Walikuja makusudi
Waliyetoka baidi
Kuifatia *jihadi*
Msangao kuingia.

165. Anakuja Banadira
Na Mwenye Bwana Komera
*Wazee wenye fikira*
(H)apo walihudhuria.

166. Vijana wa mtaani
*Hakubakia jelani*
Waliyekuwa mashambani
*Wote walihudhuria.*

167. Wakubwa wa vijijini
*Wengi sita wa a(r)baini*
*Akina Shambi amini*
*Na wao walijitia.*

Mtunzi anaposema; *Na wengine kuzidia*, anatuonyesha kuwa si wale wa Liwali na mjumbe wa vijijini waliotaka tu, bali zaidi. Maana liwali alitaka wale waume na wanawake waliolala pale kijijini na wageni ambao walikuwako alipokuwa akisema maneno haya. Pia anatuambia *kuifatia jihadi*. Jihadi ni vita vya kidini katika dini ya Kiislamu. Pia anatwambia *waliyetoka baidi.* Baidi ni sehemu za mbali. Kwa hivyo, licha ya wale waliolala pale kijijini, wengine walikuja kutoka mbali kumtafuta Salima. Kwa hivyo wanakijiji, wageni waliolala pale, Banadira, Mwenye Bwana Komera, vijana wa mitaani, jirani kutoka mashambani, wakubwa wa vijijini, liwali na jumbe Hasani wote ni watu wema maana wanakuja kupambana na uovu unaoletwa na wachawi hawa.

## 3.8 MANDHARI

Kila msomaji anaelewa kuwa matukio hukumbukwa zaidi katika utenzi. Wakati mwingine tunamwona mhusika akitembea msituni au kwenye miji ambayo ina magorofa makubwa makubwa na magari mengi. Sehemu kama hizi ndizo mandhari. Sehemu hizi

zina umuhimu sana katika kazi ya kifasihi. Watunzi wengi huyapa mandhari sifa kubwa katika utunzi wao.

Mandhari ni sehemu ambazo hujitokeza, jamii wanamoishi yaani familia, marafiki na utamaduni wao, mahali pa matukio na athari zinazoletwa na elementi hizo. Mandhari hukumbukwa kwa sababu pengine yanatisha, yanavutia au kusisimua. Baadhi ya mandhari husaidia kuonyesha hisia za wahusika na tabia zao. Watunzi wengine huchagua mandhari fulani ili waangazie msimamo wao. Msomaji huweza kuona msimamo wa msanii kupitia kwa mandhari na jinsi msanii huyo anavyosawiri mandhari hayo. Mandhari mengine huwa na mvuto mpaka yakaumba ulimwengu wao. Kwa hivyo mandhari huzua hisia za msomaji kwa sababu wakati mwingine msanii hulazimisha iwe hivyo. Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* mtunzi anatupa aina mbalimbali za mandhari ili maudhui na dhamira yake ijitokeze. Anasema:

58. Asubuhi na mapema
    Bwana Shambi bin Dima
    Anakuja himahima
    *Kembani anatokea.*

Mandhari haya yanaonyesha mahali ambapo wachawi hukutana na ni mahali ambapo ushirikina na usihiri hufanywa maana neno *Kemba* ni mahali ambapo huhusiana na mambo ya kimazingara. Kule kembani pia kuna mahali maalumu ambapo mhusika anayetolewa mhanga huwekwa maana Shambi anasema:

82. Bwana Shambi atamke:
    *Basi apo mweke*
    Alimwona dada yake
    Upesi kamnyanyua.

Wazo hili linaonyesha ukatili wa wachawi hawa katika utaratibu wao wa kutimiza mambo haya. Pia katika kutekeleza amri ya Shambi, Salima anapatwa na mshangao kwa

sababu mtunzi anatwambia: *Alimwona dada yake, upesi kamnyanyua.* Kitendo hiki kinamzulia Salima hofu na kukata tamaa.

Pia hali ya mshikamano wa jamii unajitokeza kwenye mazingira ya dironi. Dironi ni mahali ambapo watu hukusanyika na kufuturu pamoja. Mtunzi anatuambia

158. Waliowasili jioni
Panenenene mashambani
Walifikia dironi
Wanafuturu pamoya.

Pia wanalala pamoja ndani ya nyumba ya maiti. Mshairi anasema:

162. Kwa hali ya namna zake
*Jinsi ya nyumba yake*
*Jumla ya vyombo vyake*
Huruma zitakujia.

Pengine kama wangelala mahali tofauti hisia za huruma na sikitiko hazingewapata lakini msanii anawapangia walale kwenye mandhari haya ili kuzua hisia hizi za huruma kwa sababu vyombo vya marehemu labda vilivyo vingi au kupangika kwa utaratibu vinazua hisia za huruma. Vyombo hivi vinaleta kumbukumbu ya marehemu, maana mtunzi anaendelea kutuambia:

161. Basi wamelala pale
Nyumba ya mauti yule
Mfano utafikiri
*Kama kenda kutembea.*

Kwa hivyo katika kazi hii ya kifasihi mandhari haya yameiga mandhari halisi ambayo yanaathiri hadhira na msomaji kwa huruma na sikitiko juu ya Salima.

Mtunzi anatwambia kuwa baada ya Yasini Kimina na Hamadi Ramadhani kutumwa kwenda kumleta Nguvumali, Bwana Shambi anarudi nyumbani kwake. Vituko anavyoona njiani na hata nyumbani kwake vinamtia hofu. Mshairi anatwambia:

210. *Kaonа nyoka wawili*
*Wanamfata kiviri*
Dalili ya Nguvumali
Ya kuweza kumjia.

Shambi ndiye anayehimiza kuitwa kwa Nguvumali aje atambulishe wachawi. Vile vile anakuwa mdhamini wa Nguvumali. Mshairi anachagua mandhari ya njiani hata kabla ya kufika nyumbani kwake azue hofu katika maisha ya Shambi na kumhakikishia kuwa Nguvumali ana sifa za kikweli. Hofu hii inaongezeka kule nyumbani maana anapofika hakuona *zindiko* lake. Zindiko ni mahali ambapo vifaa vya kiuchawi hufichwa. Mtunzi tena anatuambia hivi kuhusu Shambi:

212. Kachukua koja lake
Kavaa shingoni mwake
Hali yuko peke yake
*Porini akaingia.*

Mtunzi anatuzushia mandhari ya porini ambako Shambi anakusanya vyombo vyote vya uchawi lakini mapembe yanapasuka, koja linakatika na mahali pale panatapakaa vitu vyake vyote vya uchawi. Hofu hii inazuka kwa sababu ya mandhari anayochagua mtunzi. Katika kutaka kuzuzua jamii msanii anasema:

227. Walimtia bandani
Waseme (h)ao hewani
Alikuja vunja kuni
*Banda linamwangukia.*

Nia ya wachawi hawa ni kuwazuzua wanakijiji ili wasadiki kuwa Salima ameangukiwa na banda. Jambo hili la kuiona maiti ya Salima bandani linaongeza changamoto ya wanakijiji ya kumtafuta Nguvumali maana wanasema:

238. Wakamjibu suali
Hebu tupe dalili
Sisi tunavofikiri
*Kwa (h) apa tulipitia.*

Mandhari haya yanazua hamu zaidi ya wanakijiji kutaka kuelewa zaidi juu ya hali iliyomkumba Salima.

## 3. 9 WAKATI

Dhana hii hutumiwa na msanii kuonyesha kipindi au vipindi ambapo matukio yanayosimuliwa hutokea. Dhana hii inaweza kutumika pia kuonyesha kipindi cha kimapisi. Mapisi haya ni muhimu sana katika kazi ya kifasihi. Katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* msanii anawakutanisha wachawi hawa jioni. Anasema:

10. Wachawi wanne yaqini
*Walikutana jioni*
Shauli gani jamani
La kuweza kutumia?

Wachawi hawa wanakutana jioni ili jamii isiwatilie shaka maana shughuli za uchawi hufanywa usiku. Kwa hiyo mtunzi anachagua jioni ili shughuli hizi zisigunduliwe. Baada ya kikao hiki mkuu wa wachawi anaingia hamasa maana mtunzi anatwambia:

58. *Asubuhi na mapema*
Bwana Shambi bin Dima
Anakuja himahima
Kembani anatokea.

Shambi anarauka *asubuhi na mapema.* Mtunzi anatuonyesha hamasa za Shambi kukutana na wachawi wenzake ili watekeleze jukumu lao la kuzingua mji. Mbinu hii ya wakati huzua hisia za kuficha na kuharakisha mambo ili yasigunduliwe na yafanyike upesi.

Pia Salima anapotea mchana kabla hajafuturu. Anaenda msituni kukata kuni. Kama wachawi hao wangemwita msituni usiku shaka ingetanda haraka au kama angeenda usiku kutafuta kuni halingekuwa jambo la kawaida.

Vile vile mshairi anachagua usiku kumletea njozi Shambi maana halingekuwa jambo la kawaida kumwotesha mchana. Mshairi anatwambia:

219. *Alipolala jioni*
Njozi zikaja kichwani
Kizunguzungu usoni
Kilevi kilimjia.

220. *Kaota ananguka*
Na makamasi kumtoka
Na machela yalifika
Ya kuja kumchukua.

Mshairi anamwotesha Shambi kumthibitishia juu ya uwezo wa Nguvumali. Kwa hivyo wakati huzua hisia za hofu, huzuni, sikitiko n.k. Katika ndoto zake usiku Shambi anaona watu wengi: Liwali, Waarabu na Waafrika wanakuja kumwona Nguvumali. Katika ndoto hizo, Shambi anampa koja lake Nguvumali kama kwamba ni nduguye.

Katika kumficha Salima asionekane tunaambiwa:

225. Babu Shambi kafikiri
*Usiku fi-' l- leyli*
Ikamjia akili
Naye (h)aikumfaria.

Hapa mtunzi anachagua usiku kwa wachawi hawa kumchukua Salima hadi bandani, na dada yake anaenda porini mchana akidai anaenda kukata kuni. Katika harakati hizi Binti Hanifu anadai kuwa amemwona dada yake akiwa maiti. Kwa hivyo wakati hujenga matukio na wahusika ili kukamilisha matukio yao kama tunavyoona. Hivyo dhana hii ya wakati hutumiwa kuelezea kipindi au vipindi ambapo hali na matukio yanayosimuliwa hutokea. Mbinu hii ya wakati imefana sana katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali.*

## 3.10 HITIMISHO

Katika sura hii tumechunguza jinsi fani inavyotumiwa kwa mapana yake kuendeleza dhamira ya mtunzi na maudhui. Fani katika utenzi huu imeteuliwa kwa ufanifu mkubwa ili kutimiza malengo ya mtunzi.

Tumebainisha kuwa Hasani bin Ismail ameathiriwa na lahaja ya Kilwa. Pia majilio ya Waarabu na Wazungu yamempa mchango mkubwa katika kukuza lugha yake katika utenzi huu. Utenzi huu umefuata fomula ya tenzi nyengine zote yaani umeanza na dua, hadithi yenyewe, asili na ilhamu ya mtunzi inavyoanza, dua tena na kuwasihi jamii wamweke mbele ya Mwenyezi Mungu ili watu wazidi kumpenda. Anasema ingawa amezaliwa Kilwa mjini lakini makao yake sasa ni mashambani.

## SURA YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

Baada ya utafiti wetu sasa tunaangazia somo kwa muhtasari. Tumehakiki fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* na jinsi vipengele vyake vinavyosaidia kusukuma mbele maudhui ya kazi hiyo. Pia tumejaribu kubainisha jinsi Hasani bin Ismail alivyotumia lahaja ya Kilwa katika utunzi wake. Tumejadili mapendekezo yetu kama yanavyojitokeza katika nadharia tete.

### 4.1 UTANGULIZI

Katika sura ya kwanza, tumeonyesha na kufafanua vigezo tulivyotumia ambavyo ni pamoja na somo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu ya kuchagua somo, yaliyoandikwa kuhusu somo, upeo na mipaka, msingi wa nadharia, nadharia tete na vilevile tumejadili njia tulizotumia za kukusanyia data.

Kwenye sura ya pili tumefafanua swala la fasihi simulizi, maana ya ushairi, lugha ya ushairi, maendeleo ya ushairi, athari za wageni na ushairi huru. Kuhusu fasihi simulizi, tumegundua kwamba ni aina ya simulizi ambayo hupitisha ujumbe kwa msikilizaji kwa njia ya mdomo. Msimulizi hutumia fani katika fasihi kupitishia ujumbe kwa msikilizaji. Katika mawasiliano hayo binadamu hujifunza maadili, wosia, hekima, mawaidha, n.k.

Pia tumeeleza maana ya ushairi na jinsi matumizi ya lugha ya ushairi yanavyotofautiana na matumizi ya lugha ya tanzu nyengine za fasihi. Ushairi huzua hisia tofauti tofauti katika akili ya msomaji. Kwa kutumia fani, maneno hutumiwa na mtunzi kwa njia isiyo ya kawaida ili akidhi dhamira yake.

Pia tumechunguza chimbuko la ushairi na maendeleo yake. Tumegundua kwamba mwanzo wa ushairi ni nyimbo zilizoimbwa pale zamani. Nyimbo hizo ziliimbwa katika vipindi mbalimbali. Maingiliano ya wageni na wenyeji wa upwa wa Afrika Mashariki yalizua utamaduni mpya ambao uliendeleza ushairi andishi. Kutokana na athari hizi

miundo ya ushairi ilianza kugeuka. Msamiati wa Kiarabu na Kiingereza ulianza kujipenyeza katika lugha ya ushairi, na kuendeleza ushairi mbele.
Katika sura ya tatu tumejadili vipengele vya fani kama vinavyojitokeza katika utenzi huu. Tumejadili mtindo aliotumia mtunzi, lugha ya ushairi, muundo, wahusika, toni, msuko, mandhari na wakati wa matukio hayo. Kuhusu mtindo, mtunzi ametumia sana lahaja ya Kilwa, utohozi wa maneno ya Kiarabu na Kiingereza ili afanishe maudhui katika kazi hii. Pia ametumia tamathali nyingi za usemi.

Amegawanya utenzi huu kwenye beti zenye mistari minne kila ubeti. Beti hizi zina mistari yenye mizani zilizolingana. Vina vya mistari mitatu ya mwanzo vina upatanifu. Kina cha bahari, yaani mstari wa nne, hakina upatanifu na vina vya mistari iliyotangulia. Utenzi huu una beti mia tatu tisini na tatu.

Mtunzi amechagua wahusika wema na waovu. Wahusika wema wanatatizwa na wahusika waovu mpaka maisha katika kijiji yanakuwa magumu. Serikali inaunga mkono wahusika wema dhidi ya wale waovu. Mganga Nguvumali naye anajitolea na kuunga mkono hawa wahusika wema. Anawatambulisha hawa wahusika waovu ambao wanafungwa gerezani. Mmoja wao anafariki akiwa hospitalini kwa ajili ya kipigo kutokana na polisi. Kwa hivyo, uteuzi wa wahusika unatusawiria vizuri uovu unaoendelea kwenye kijiji cha Mteniyapa.

Msuko wa hadithi hii ni wa moja kwa moja, ingawa una vitushi vingi. Msuko wenyewe ni sahili na umegawanywa kwenye matendo kadha. Wachawi wanakutana na kuamua kutekeleza dhana yao ya kufanyia zinguo kijiji hicho. Mwathiriwa anapotea na kuuawa. Wanakijiji wanaipasha serikali habari, huku wakimwalika mganga Nguvumali kuja kuwategulia kitendawili cha kupotea, na hatimaye kufa kwa Salima.

Toni inayotuonyesha hisia za msanii inajitokeza, na kwamba wahusika wanatumia toni mseto. Baadhi ya toni hizi ni pamoja na toni ya kuamrisha inayotolewa na mkuu wa wachawi hawa, toni ya kukiri, unyenyekevu inayotolewa na mwathiriwa, matusi, kejeli, n.k.

Kuhusu mandhari na wakati, mtunzi anatumia mbinu hizi sawasawa. Tunaona wahusika wakisawiri mandhari na wakati tofautitofauti kulingana na dhamira ya mtunzi. Wachawi hawa wanakutana jioni na mahali ambapo wanakijiji hawawaoni. Mandhari na wakati hutegemea wahusika wenyewe na dhamira zao. Mtunzi amefaulu katika kuchagua mandhari na wakati unaofaa.

Kwa hivyo mtunzi amefanisha kazi yake kwa kutumia vipengele vya fani. Wahusika wanasawiri ukatili wao kwa kutumia lugha, mandhari na wakati maalumu. Msuko, mtindo na muundo wa utenzi huu umechukuana na dhamira ya mtunzi na jinsi fani inavyotekeleza kazi yake na kuendeleza maudhui ya kazi yake.

## 4.2 MASUALA MUHIMU

Katika tasnifu hii tumeshughulikia fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali.* Tumedhamiria kuthibitisha nadharia tete tano.

Nadharia tete ya kwanza ni kwamba mtunzi ametumia msamiati akilenga hadhira ya kisasa. Tumethibitisha kwamba nadharia hii ina ukweli kwa sababu vipengele vya fani kama vile utohozi wa msamiati wa lugha ya Kiarabu na Kiingereza umefana sana. Pia ametumia tamathali nyingi za usemi kwa kina. Vile vile ametumia nahau na methali za Kiswahili kutuangazia hali halisi ya jamii anamoishi.

Nadharia tete ya pili ni kwamba baadhi ya wahusika hugeuza lugha kulingana na hadhira kwa sababu ya malengo fulani. Mkuu wa wachawi anapoongea na wachawi wenzake hutumia lugha ya vitisho na msamiati funge. Msamiati wanaouelewa wao wenyewe. Hutumia lugha ya vitisho, matusi na kejeli. Anajua kwamba wachawi hawa wanamheshimu na kumwogopa. Lakini akiwa na wanakijiji hutumia msamiati wa unyenyekevu. Kwa hivyo nadharia hii ina mashiko sana maana hataki wanakijiji watambue kuwa anahusika na kifo cha Salima. Anajitolea hata kugharamia mambo fulani ya Nguvumali.

Nadharia tete ya tatu inasema kwamba matumizi ya lugha ya mtunzi yanabeba dhamira anayokusudia. Ni kweli kabisa kwa sababu lugha ya mkuu wa wachawi imejaa vitisho, kejeli na kuamrisha. Nia ya mtunzi ni kutusawiria hisia za ukatili anazokuwa nazo mchawi hasa kiongozi wao. Siyo huyu tu bali hata wachawi wengine wanaofikia uamuzi wa kuwatoa watu wa familia yao kafara.

Hata pale Binti Ramadhani anapojitolea kutia ubani kwanza; mtunzi anataka tuone kwamba katika jamii, wako watu wa aina hiyo ya kujionyesha kuwa ni watu wa dini ilhali wanaabudu mizimu. Anatusawiria jamii iliyojaa uozo. Pia pale Salima anapopotea mtunzi anatumia takriri ya kutuhakikishia kuwa sasa Salima amezongwa na madawa ya wachawi hao, na kutukatisha tamaa ya kuwa Salima anaelekea kwenye hatima yake. Anatuzulia hisia za huruma na kuona nguvu za madawa ya uchawi.

Nadharia tete ya nne ni kwamba mtunzi amateua vipengele vya fani ambavyo vinakidhi muktadha. Nadharia tete hii ina uzito unaostahili. Binti Hanifu anapomtoa mhanga dada yake, anaingiwa na wasiwasi na woga. Anawashauri wenzake wamtoe pale kembani kabla ya wanakijiji kutambua yaliyokuwa yakitendeka. Binti Ramadhani naye anaanza kujuta kwa nini anamletea majonzi mtoto wake Ramadhani Kiponda kwa kutaka kumwulia mkewe. Anapatwa na kiwewe na majuto. Anaamua kujitoa kundini iwapo wenzake hawatakubali kumrudisha nyumbani mwathiriwa. Lakini Shambi anamwambia; *maji yakimwagika, hayazoleki kama taka* (125). Katika hali hii ya hofu na kubabaika, mtunzi anatumia methali hii ili kuwakatisha tamaa baadhi ya wachawi hawa. Pia anatumia tashibihi *kama taka* kutusawiria kilinge wanamojikuta wachawi hawa. Anawaonyesha kuwa hali waliyonayo imepea. Afadhali watafute njia nyengine ya kuwawezesha kudhibiti hali hii.

Pia, katika kuwazuzua wanakijiji, Binti Ramadhani anatumia kejeli: *nitie kwanza ubani, ndipo tutaenda* (168). Binti Ramadhani anajua kuwa Salima ashakufa. Anajitia kimbelembele ili wasitambulikane. Mbinu hizi na nyengine zinatuonyesha dhamira za wahusika hawa katika kufaulisha harakati zao katika mazingira haya ya Uislamu hasa

wakati huu wa mwezi mtukufu wa Ramadhani. Kwa hivyo vipengele hivi na vingine kama sitiari, mbinurejeshi, n.k vinakidhi muktadha wa kutaka kuwazuzua wanakijiji.

Nadharia tete ya tano ni kwamba, kwa kutumia fani mtunzi amefaulu kuisawiri jamii anamoishi ya wahusika wema na waovu katika mazingira ya kidini dhidi ya mazingira ya kijumla. Huu ni mwezi mtukufu wa Ramadhani, lakini hapo hapo tunapata wachawi wenye dhamira ya kupingana na dini. Shambi mwenyewe anasema; *sikizeni nisemayo...tufanye mji zinguo*. Hiki ni kipengele cha litifati. Tunashuhudia Shambi akionyesha ukatili wake. Wachawi hawa hawaheshimu imani za kidini za watu kama Salima. Mtunzi anatusawiria ile falsafa ya wema ukipingana na uovu.

Pia Binti Jizi anaposema; *yatakimbia majeshi* ( 20), anatumia sitiari kusisitiza nguvu walizonazo wachawi hawa. Hajali nguvu za Mungu. Kwa hivyo mtunzi anatuangazia mitazamo mbalimbali ya jamii. Wengine ni watu wa Mungu kweli kweli na wengine wana imani mseto. Hata katika mateso yake Salima anawanyenyekea wachawi hao hasa dada yake. Anamwambia; *nawe utaangamia*. Huu ni utabiri. Anatumia mbinu elekezi. Huyu anawakilisha watu wema. Yeye ni mtu wa Mungu, na kwa kutumia kipengele hiki mtunzi anatusawiria jamii anamoishi kuwa ingawa huu ni mwezi mtukufu, wapo wasiothamini sana mambo ya dini.

## 4.3 MAPENDEKEZO

Katika sehemu ya upeo na mipaka ya kazi hii tumesema hatutachunguza maudhui ila tu pale yanaposaidia kuangazia fani. Hata hivyo katika utenzi huu swala la maudhui halijashughulikiwa kwa undani. Kwa hivyo tungependa wahakiki wenzetu waliangalie swala hilo kwa kina.

## MAREJELEO


Abdallah, A (1973): *Sauti ya Dhiki*, O.U.P, Nairobi.

(1973): *Ushairi wa Kiswahili: Na Uhuishwe, Usiuliwe*; Makala ya Kiswahili vol 37/22(173:50), TUKI , Dar-es-Salaam.

Abdulaziz, M.H (1968): *A Note on the Form of the Language of the poem katika Leinhardt (mhr): The Medicineman*; Clarendon press, U.K.

(1979): *Muyaka: 19th century Swahili popular Poetry*; Kenya Literature Bureau, Nairobi.

Abedi, K.A (1963): *Diwani ya Amri Kaluta Abed,* E.A.B.L, Nairobi.

(1993): *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*; Nairobi.

Abrams, M.H (1957): *3rd Ed. A glory of Literary Terms*; Holt, New York.

Achebe, C (1973): Shujaa Okonkwo; Heinemann Educational Books, Nairobi.

Adagala, K na Kabira, W.M (Mhr 1985): *Kenyan Oral Narrative, A selection*; East African Educational Publishers Ltd, Nairobi.

Akilimali, S. (1973): *Diwani ya Akilimali,* East African Literature Bureau, Nairobi.

Akivaga, S.K na Odaga, A.B (1982): *Oral Literature, A school Certificate Course*; Ujuzi Educational Publishers Ltd, Nairobi.

Allen, J.W.T (1971): *Tendi;* Heinemann; Nairobi.

Allington, P.V (2005): *The Victorian web- Literature History and Culture in the Age of Victoria*; Lakehead University, Canada.

Arege, T.I.M (1998): *Ushairi Huru wa Kiswahili*; *Mchango wa Kezilahabi*, Tasnifu ya Uzamili. (Haijachapishwa).

Aristotle (1934): *The Poetics*; J.M Dent & Sons Ltd, New York.

Bakari, M (1978): *The State of the Art; Swahili Literature in the 19th Century*; Assembly of Kenya Annual Conference.

Bashir, A (Mhr 1972): *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*; Heinemann Educational Books (EA) Ltd, Nairobi.

Bukenya, A
Gachanja, M na
Nandwa, J (1997): *Oral Literature a Senior Course*; Longhorn Publishers (K) Ltd, Nairobi.

Buliba, A
Njogu, K
Mwihaki, A (2006): *Isimujamii, Msingi na Nadharia*; J.K.F, Nairobi

Camus, A (1953): *The Rebel*; Hanish Hamilton, London.

Chesaina, C (1991): *Oral Literature of the Kalenjin*; East African Educational Publishers, Nairobi.

Cohen, R. (1974): *New Directions in Literary History:* Routeledge and Kegan Paul, London.

Coset, L.A (1963): *Sociology Through Literature*: Prentice – Hall International Inc. London.

Cuddon, J.A (1979): *A Dictionary of Literacy Terms*; Andre Deustch Ltd, London.

Daiches, D. (1956): *Critical Approaches to Literature,* Longman, London.

Demetz, P. (1967): *Marx, Engles and the Poets,* University of Chicago, U.S.A.

Diyanni, R (1994): *Literature; Reading Fiction, Poetry and Drama and the Essay;* MC Graw-Hill, New York.

Eagleton, T (1976): *Marxism and Literary Criticisms*; London, Methuen.

Fanon, F (1977): *The Wretched of the Earth*; (trans. by Constance Farrington), Grove Press inc. New York.

Fugard, A (1960): *Nongogo*; Guernsey Press, London.

(1974): *Sizwe Bansi is Dead*; Oxford University Press, London.

Gachanja, M na Bukenya, A.S (1996): *Oral Literature, A Junior Course*; Longhorn Publishers (K) Ltd, Nairobi.

Green, N.N (1960): *Jean- Paul Sartre: The Exstentialist Ethic*; University of Michigan Press, U.S.A.

Grill, R (1995): *Mastering English Literature*; Macmillan Press, Hampshire.

Gugelberger, G (Mhr 1985): *Marxism and African Literature*; Oxford University Press, London.

Haji, I.A, Muhammed, S.A, Hamadi, K.A na Omar, M.M (1981): *Msingi ya Nadharia ya Fasihi;* Taasisi ya Kiswahili ya Lugha za Kigeni/ Wizara ya elimu, Zanzibar.

Hamilton R. G (1982): *Research in African Literature*; Vol.13, No.3 University of Texas, USA.

Harries, L (1962): *Swahili Poetry*; Oxford University Press, New York.

Hichens, W (1941): *Swahili Prosody*; Swahili Journal of the East African Committee, Vol. 33.

Hoffernan na Johnson (1987): *Literature: Art and Artifact*; Harcourt Brace Jounovch, London.

Hornby, A.S (1989): *Oxford Advanced Learners Dictionary*; Oxford.

Ionesco, E (1962): *The chairs; Reading*; Cox and Wyman Ltd, London.

Jeyifo, B (1980): *West African Review*; Issue 9, 2006.

Lambert, H.E (1971): *Diwani ya Lambert;* East African Literature Bureau, Nairobi.

Leech, G.N (1969): *Linguistic Guide to English Poetry*; Longman Group Ltd, England.

Kabira, W.M (1983): *The Oral Artist*; East African Educational Publishers, Nairobi.

Kahigi, K.K. (1975): *Ushairi Mtazamo wa Kisayansi, Makala ya Kiswahili.* Vol. 45/1/Uk. 40.

Kahigi, K.K na Mulokozi, M.M (1976): *Malenga wa Bara,* East African Literature Bureau, Dar-es-Salaam.

Karauri, M.A (1966): *Travelling gods*; Karma Publishing Co., Nairobi.

Kariara, J na Kitonga, E (1976): *An Introduction to East African Poetry;* Oxford University Press, New York.

Kazungu, E.K (1982): *Deviation and Foregrounding in Chosen Literary Swahili Texts* (Tasnifu).

Kezilahabi, E (1972): *The Development of Swahili Poetry* (18th -20th century Makala ya Kiswahili vo. 42/2 (1972:67)

(1974): *Kichomi*; Heinemann Educational Books, Nairobi.

(1983): *Uchunguzi Katika Ushairi wa Kiswahili*; *Makala ya Semina ya Kimataifa ya waandishi wa Kiswahili*; Tuki, Dar-es-salaam.

(1988): *Karibu Ndani*; Dar-es Salaam University Press, Dar-es Salaam

Kieti, M Goughlin, P (1990): *Barking, You'll Be Eaten!;* Phoenix Publishers Ltd, Nairobi.

Killam, C.D (Mhr 1973): *African Writers and African Writing;* Heinemann, London.

Kingei, G (1987): *Mwongozo wa tamthilia ya Mashetani;* English Press Ltd, Nairobi.

(2000): *Mwana Kupona*; Sasa Sema Publishers, Nairobi.

Kitsao, J. (1975): *A Stylistic Approch Adopted for the Study of Swahili Prose Texts* (Tasnifu) ya Phd. Haijachapishwa.

Knappert, J (Mhr 1964): *Four Swahili Epics*; Supplement to Journal 35/2.

(1979): *Four centuries of Swahili Verse;* Darf Publishers Ltd; London.

Kuvuna, S.M
Mvati, M.N na
Maliachi, P.A (1992): *Nuru ya Ushairi; Mwongozo na Uchambuzi*; Kenya Literature Bureau, Nairobi.

Lambert H.E (1971): *Diwani ya Lambert,* East African Literature Bureau, Nairobi.

Leech GN (1969): A Linguistic Guide to English Poetry; Longman Group Ltd, England.

Lienhardt, P (Mhr 1968): *The Medicine Man;* Clarendon Press, Oxford.

Liyong, T (Mhr 1972): *Popular Culture of East Africa*; Longman Publishers (K) Ltd , Nairobi.

Luvai, A.I (1988): *Boundless Voices, Poems of Kenya*; East African Educational Publishers, Nairobi.

Luvai, A.I na
Makokha, K. (Mhr 2000): *Echoes Across the Valley*; East African Educational Publishers, Nairobi, Kampala, Dar-es-salaam.

Mathooko, P.M (2007): *Isimujamii, Msingi na Nadharia*; Birds Printers and Stationery, Nairobi.

Mayoka, J.M (1986): *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*; Tanzania Publishing House, Dar-es-Salaam.

Mazrui, A. (1988): *Chembe cha Moyo;* East African Educational Publishers, Nairobi.

Mbarwa, H.R (1989): *Your Oral Literature*; Eagle H. Publishers, Nairobi.

Mbatiah, M (2001): *Kamusi ya Fasihi;* Standard Textbooks Graphics and Publishing, Nairobi

Miruka, O (1994): *Encounter with Oral Literature*; East Africa Educational Publishers, Nairobi.

Mlamali, M (1980): *Al-Inkishafi*; Longmans, Nairobi.

Mnyampala, M.E. (1964): *Fasihi Johari ya Mashairi,* Halmashauri ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, Dar-es Salaam.

(1965): *Diwani ya Mnyampala*, E.A.L.B, Nairobi.

(1965): *Waadhi wa Ushairi,* E.A.B.L, Nairobi.

(1970): *Ngonjera ya Ukuta 1,* Oxford University Press, Dar-es. Salaam.

(1971): *Ngonjera ya Ukuta 2;* Oxford University Press Dar-es-Salaam.

(1981): *Kisa Cha Mrina Asali na Wenzake Wawili,* East African Literature Bureau, Nairobi.

Mohamed, S.A (1984): *Kina cha Maisha;* Fotoform Ltd, Nairobi.

(2000): *Kitumbua Kimeingia Mchanga;* Oxford University Press, Nairobi.

(2001): Mwongozo wa *Kilio cha Haki:* Fotoform Limited, Nairobi.

(2002): *Jicho la Ndani*; Longhorn Publishers, Nairobi.

Msokile, M (1993): *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*; East African Educational Publishers, Nairobi.

Mulokozi, M.M (Mhr 1999): *Tenzi Tatu za Kale*; TUKI, Dar-es-Salaam.

Mungai, F.K (2005): *Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa).* Nairobi University.

Mvati, M.N
Ngure, A (2003): *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*; Phoenix Publishers Ltd, Nairobi.

Mwita, L.C (2003): *Mwongozo wa Walenisi;* Fotoform Limited, Nairobi.

Nazareth, P (1978): *The Third World Writer: His Social Responsibility*; Kenya Literature Bureau, Nairobi.

Njogu, K. na
Chimerah, R (1999): *Ufundishaji wa Fasihi; Nadharia na Mbinu*; Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Njogu, K
Momanyi, C na
Mathooko, M (Mhr 2006): *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*; Twaweza Comunications, Nairobi.

Ogutu, B.O na
Roscol, A.A (1974): *Keep my Words, Luo Oral Literature*; Ujuzi Educational Publishers Ltd, Kampala.

Okpewho, I (Mhr 1985): *The Heritage of African Poetry*; Oxford University Press, New York.

Oxford (2004): *Kamusi ya Kiswahili Sanifu;* Oxford University Press, Nairobi.

P'Bitek, O (1972): *Song of Lawino*; Kenya Litho Ltd, Nairobi.

(1974): *The Horn of my Love*; East African Educational Publishers, Nairobi.

(1986): *Artist the Ruler*; General Printers Ltd, Nairobi

Robert, S. (1947): *Pambo la Lugha;* Oxford University Press, Nairobi.

(1959): *Insha na Mashairi;* Thomas Nelson and Sons, Tanzania.

(1968): *Kielezo Cha Fasili*; Printpak, Tanzania.

(1969): *Ashiki Kitabu Hiki:* Printpak, Tanzania.

(1969): *Mwafrika Aimba*; Thomas Nelson and Sons, Tanzania.

Roberts, S. na
Jacobs, M. (1972): *Literature: An Introduction to reading and writing*; Printire Hall, New York.

Rubadiri, D na
Cook, D (Mhr 1971): *Poems from East Africa*; East African Educational Publishers, Nairobi.

Senkoro, F.E.M(1982): *Fasihi*; Press and Publicity, Dar-es-Salaam.

Syambo, B. na
Mazrui, A (1992): *Uchambuzi wa Fasihi;* East African Educational Publishers, Nairobi.

Taylor, W. (1894): *African Apherisms:* Songs from Swahili Land, London.

Tuki (1990): *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha;* Tuki, Dar-es-salaam.

Vuzo, A (1986): *Mwongozo wa Nyota ya Rehema,* Heinemann Kenya Limited, Nairobi.

Wa Mberia, K (1997): *Mchezo wa Karata*; Marimba Publications Ltd, Nairobi.

(2000): *Bara Jingine*; Marimba Publications Ltd, Nairobi.

Wamitila, W. K. (2002): *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*; Phoenix Publishers Ltd, Nairobi.

(2003): *Kamusi ya Fasihi; Istilahi na Nadharia*; FocusBooks, Nairobi.

(2003): *Kichocheo cha Fasihi; Simulizi na Andishi*; Focus Books, Nairobi.

Wa Mutiso, K (1985): *Hurafa na Uyakinifu katika Hamziya*; Tasnifu; M.A (Haijachapishwa), Nairobi.

(1986): *Mizani Yangu:* Kenya Literature Bureau, Nairobi.

(1996): *Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry*; Tasnifu Ph. D (Haijachapishwa), Nairobi.

(2002): *The Epic of Princess Fatuma* (Mswada) Haijachapishwa.

(2003): *The Epic of All Secrets* (Mswada) Haijachapishwa.

Wa Thiong'o, (1981): *Writers in Politics*; General Printers Ltd, Nairobi

(1982): *Shetani Msalabani*; East African Educational Printers, Nairobi na Kampala.